# UTAMBULISHO WA JINSIA KATIKA *MAUMBILE SI HUJA* NA *PARADISO*

NA

ATIENO JACQUELINE

C50/76755/2014

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2019

## UNGAMO

Tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kingine chochote.

Atieno Jacqueline Sahihi Tarehe

C50/76755/2014 ………. ……….

(Mtahiniwa)

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi mteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi Tarehe

………………………… …………………….

Dkt. Amiri Swaleh

(Msimamizi)

Sahihi Tarehe

………………………… …………………….

Bw. Samson Ongarora

(Msimamizi)

## TABARUKU

Ninatabaruku kazi hii kwa babangu mpendwa Johnson Alwala Mumbo na mamangu Pheobe Auma Alwala kwa kunilea na kuniauni kila nilipohitaji msaada wao wakati wa masomo yangu. Ninaitabaruku pia kwa mume wangu Carilus Oyieke Nyagweth kwa kunitia moyo nilipokuwa masomoni hasa wakati wa kufanya utafiti huu. Tabaruku kuu zaidi ni kwa wanangu Joe Onyango na Javiermitch Ogutu kwa kunipa hamasa katika masomo yangu.

**SHUKRANI**

Shukrani zangu za dhati zimwendee Maulana kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kufikia kiwango hiki katika masomo yangu.

Kazi hii imefanikishwa kutokana na ukarimu na juhudi za watu kadha. Ninatoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Amiri Swaleh na Bw. Samson Ongaroro kwa kuniongoza, kunikosoa na kunipa ushauri wakati wa utafiti wangu. Ninawashukuru kwa kunirekebisha kwa uangalifu na kuwa na subira nami. Mola awabariki. Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wangu wote katika Idara ya Kiswahili niliowahi kuwa chini ya ufundishaji wao; Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Zaja Omboga, Prof. Iribe Mwangi, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Prof. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri na Bw. Leo Sanja kwa kuchochea fikra zangu. Mchango wenu kiusomi kwangu huwezi kupuuzwa kamwe.

Ninawashukuru wanafunzi wenzangu Raymond Owalla, Florence, Lilian, Clarice, Rose, Pauline, Peter, Veronica, Nina, Dominic, Kithinji, Nancy na Silas tuliokuwa nao katika kipindi cha masomo yangu. Shukrani zangu za dhati pia zimwendee mume wangu Carilus Nyagweth kwa kunishika mkono na kunitia moyo wakati wa masomo yangu. Ninamshukuru Judith Ododa kwa ushauri wake. Ninawashukuru pia Evans Omondi na John Nyagweth kwa kuniauni kila nilipowahitaji na kunifaa kwa njia moja au nyingine.

Ninatoa shukrani zangu kwa wazazi wangu, Johnson Alwala Mumbo na Pheobe Auma Alwala kwa malezi na ushauri wenu. Ninawashukuru kaka na dada zangu; George Oduor Alwala, Moses Alwala, Elizabeth Achieng Alwala na Judith Akinyi Alwala; hamkuchoka kunitia moyo na kunishauri. Siwezi kusahau kuwashukuru Rose Atieno, Mitchel Bavon, Noel Nyageth, Philip Nyagweth, Johnson Junior, Tabitha Oduor na baba Milando kwa kunitakia mema. Mola awajalie baraka tele.

# IKISIRI

Lengo la utafiti huu limekuwa ni kuchunguza na kuchanganua utambulisho wa jinsia katika kazi za John Habwe za *Maumbile si Huja* na *Paradiso*. Mada hii imechaguliwa kutokana na uelewa kuwa kazi za kifasihi huibua utambulisho wa jinsia tofauti. Dira ambayo imetuongoza kufanya utafiti huu ni nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Tumechagua nadharia hii kuchunguza na kuchanganua utambulisho wa jinsia kwa kuchunguza uhusiano wao katika mazingira ya Kiafrika kwa kuwa imeandikwa kwa msingi wa Kiafrika. Nadharia hii huonyesha jinsi asasi za jamii za Kiafrika huchangia katika dhuluma za kijinsia. Pia, nadharia hii hutoa mapendekezo ya namna ya kupigania ukombozi, usawa na haki ya jinsia katika jamii. Malengo ambayo tumeshughulikia ni kubainisha jinsi asasi za jamii kupitia tamaduni zake zinavyoathiri mazingira ya utambulisho wa jinsia, kuangazia namna jinsia za kike na kiume zinavyoathirika kutokana na changamoto zinazopitia katika harakati za kutaka kujitambua na kutambulishwa na kudhihirisha mabadiliko ya mielekeo ya jamii kupitia fasihi kama nyenzo muhimu inayochangia mabadiliko hayo. Mbinu ambayo tumetumia katika utafiti huu ni ile ya kukusanya matini za data ya utafiti kutoka vitabuni maktabani. Matokeo ya utafiti wetu ni kuwa, asasi za jamii kama vile, ndoa, dini, utamaduni, uchumi, siasa na uongozi huchangia dhuluma za jinsia. Aidha, tumeona kuwa kuna njia anuwai zinazoweza kutumiwa kuleta ukombozi na usawa wa jinsia. Vile vile, tumegundua kuwa harakati za jinsia kutaka kujitambua na kutambuliwa na jamii zinachangia mabadiliko katika mielekeo ya jamii kutokana na mabadiliko katika majukumu ya jinsia kama yanavyowekewa msingi na utamaduni wa Kiafrika.

## YALIYOMO

**UNGAMO** .......... ii
**TABARUKU** .......... iii
**SHUKRANI** .......... iv
**IKISIRI** .......... v

## SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Tatizo la Utafiti .......... 2
1.3 Maswali ya Utafiti .......... 2
1.5 Sababu za Kuchagua Mada .......... 3
1.6 Upeo na Mipaka .......... 4
1.7 Msingi wa Kinadharia .......... 4
1.7.1 Nadharia ya Ufeministi .......... 5
1.7.1.1 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika .......... 6
1.7.1.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika .......... 8
1.9 Mbinu za Utafiti .......... 15
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli .......... 16
1.9.2 Ukusanyaji wa Data .......... 16
1.9.3 Uchanganuzi wa Data .......... 16
1.9.4 Uwasilishaji wa Data .......... 17
1.10 Hitimisho .......... 17

## SURA YA PILI

## UTAMBULISHO WA JINSIA KATIKA ASASI ZA JAMII

2.1 Utangulizi .......... 18
2.2 Ndoa .......... 18
2.2.1 Ndoa katika Maumbile Si Huja .......... 21
2.2.2 Ndoa Katika Paradiso .......... 22
2.3 Dini .......... 25
2.3.1 Dini Katika Maumbile Si Huja .......... 26
2.3.2 Dini Katika Paradiso .......... 27
2.4 Utamaduni .......... 32

2.4.1 Utamaduni Katika Maumbile Si Huja ..... 32
2.4.2 Utamaduni Katika Paradiso ..... 34
2.5 Elimu ..... 36
2.5.1 Elimu Katika Maumbile Si Huja ..... 36
2.5.2 Elimu Katika Paradiso ..... 37
2.6 Uchumi ..... 38
2.6.1 Uchumi Katika Maumbile Si Huja ..... 38
2.6.2 Uchumi Katika Paradiso ..... 39
2.7 Siasa na Uongozi ..... 40
2.7.1 Siasa na Uongozi Katika Maumbile si Huja ..... 40
2.7.2 Siasa na Uongozi Katika Paradiso ..... 41
2.8 Hitimisho ..... 42
SURA YA TATU
CHANGAMOTO WANAZOPITIA JINSIA KATIKA KUTAFUTA UTAMBULISHO
3.1 Utangulizi ..... 43
3.2 Kiburi na Ubinafsi ..... 43
3.2.1 Kiburi na Ubinafsi Katika Maumbile Si Huja ..... 43
3.2.2 Kiburi na Ubinafsi Katika Paradiso ..... 45
3.3 Kutowajibika ..... 49
3.3.1 Kutowajibika Katika Maumbile Si Huja ..... 49
3.3.2 Kutowajibika Katika Paradiso ..... 51
3.4 Umaskini ..... 52
3.4.1 Umaskini Katika Maumbile Si Huja ..... 52
3.4.2 Umaskini Katika Paradiso ..... 53
3.5 Watoto na Malezi ..... 54
3.5.1 Watoto na Malezi Katika Maumbile Si Huja ..... 55
3.5.2 Watoto na Malezi Katika Paradiso ..... 55
3.6 Kushikilia Mila na Desturi Chakavu za Kiafrika ..... 57
3.6.1 Kushikilia Mila na Desturi Chakavu za Kiafrika Katika Maumbile si Huja ..... 57
3.6.2 Kushikilia Mila na Desturi Chakavu za Kiafrika Katika Paradiso ..... 58
3.7 Dhuluma na Ukatili ..... 59

3.7.1 Dhuluma na Ukatili Katika Maumbile Si Huja ........................................................ 59
3.7.2 Dhuluma na Ukatili Katika Paradiso ........................................................................ 60
3.8 Hitimisho ....................................................................................................................... 62

**SURA YA NNE**

**MABADILIKO YA MIELEKEO KATIKA JAMII KUHUSU UTAMBULISHO WA JINSIA**

4.1 Utangulizi ....................................................................................................................... 63
4.2 Mabadiliko ya Mielekeo ya Jamii Kuhusu Utambulisho wa Jinsia Katika Maumbile Si Huja ........................................................................................................................ 63

**SURA YA TANO**

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1 Utangulizi ....................................................................................................................... 79
5.2 Muhtasari wa Utafiti ...................................................................................................... 79
5.3 Matokeo ya Utafti .......................................................................................................... 80
**MAREJELEO** ................................................................................................................... 83

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inatoa taarifa za awali kuhusu vipengele vya utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti na hitimisho. Utafiti huu umeshughulikia utambulisho wa jinsia kwa kuchambua na kuchanganua kazi za mwandishi John Habwe za *Maumbile si Huja* na *Paradiso.* Tumechanganua kazi hizi kwa mwelekeo wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika tukiangazia uhusiano wa jinsia katika mazingira wanamoishi na majukumu waliyotwikwa na jamii kwa msingi wa utamaduni wao. Katika utafiti huu, istilahi 'utambulisho' imetumiwa kumaanisha sifa na matumaini ya pamoja yanayowabainisha watu au kundi la watu walio na sifa sawa zinazowatambulisha katika kipindi maalum.

Kama anavyosema Mlacha (1991) kwamba, uchambuzi na uchanganuzi wa kazi za fasihi unaweza kufanywa kwa kuzingatia vipengele anuwai kwa kutegemea kusudi la mchanganuzi.

Msokile (1992) anasema kuwa wahusika kama kipengele cha fani ya lugha wana uwezo wa kuathiri yanayosimuliwa na kuendeleza matukio kwa hivyo, wanachangia katika kuendeleza masimulizi ya kifasihi. Bal (1997) anasema kuwa wahusika wanashabihiana na binadamu na kwa sababu fasihi imeandikwa na binadamu ni mwafaka kuwashirikisha. Wahusika si watu halisi bali ni viumbe wanaobuniwa na msanii kutokana na mwigo na kumbukumbu kwa lengo la kuakisi masuala ya kijamii. Msanii anaweza kujenga wahusika wake kwa kutumia mbinu tofautitofauti kama vile mbinu ya matendo, matamshi, uzungumzaji nafsi na mazungumzo miongoni mwa wahusika pamoja na uwasilishaji dhahiri.

Harakati za kutaka utambulisho zinachangia migogoro baina ya waja kutokana na mabadiliko ya mielekeo ya jamii kwa msingi wa majukumu yao. Tumeona ni vyema kushughulikia jinsia za kike na kiume kwa kuwa wanaume ni washikadau katika harakati za kutafuta ukombozi wa wanawake kwa kuegemea mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Utafiti wetu umeangazia namna ambavyo mwandishi mwanamume amefaulu katika kuwasawiri mwanamke na mwanamume kwa kutambulisha nafasi yao bayana katika jamii.

Baadhi ya waandishi wameshiriki katika vita vya ukombozi wa jinsia kwa namna tofautitofauti. Licha ya kudhihirisha matatizo wanaokumbana nao wanajamii, wanaonyesha kwamba kuna uwezekano wa matatizo haya kutatuliwa. Waandishi kama hawa huchochea wanajamii watatue matatizo yanayowakumba kwa kutafakaria suluhu yao mbali na kuchangia jamii mpya iliyo na wanajamii wanaopigania ukombozi na maendeleo yao.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Tatizo la utafiti ni kuangazia utambulisho wa jinsia katika kazi za fasihi za mwandishi John Habwe za *Paradiso* na *Maumbile si Huja*. Harakati za kupigania ukombozi, haki na usawa wa jinsia zimeendelea kwa muda mrefu, kutoka wakati wa kuasisi vuguvugu la Ufeministi linalopinga usawiri duni na dhaifu wa mwanamke katika jamii. Japo harakati za vuguvugu hili zimezalisha matunda kwa kiwango fulani, bado pana haja ya kuimarisha zaidi.

Kutokana na dhana kuwa harakati hizi zinahusu jinsia ya kike kwa sababu ndiyo inayoathirika moja kwa moja, watafiti wengi wa fasihi wameshughulikia masuala ya wanawake ya kupigania ukombozi, haki na usawa pasi na kushirikisha wanaume kama washikadau katika harakati hizo. Waandishi wamejaribu kutumia kazi za sanaa ili kubadili mtazamo huu. Kwa sababu hii, utafiti huu umeshughulikia masuala ya utambulisho wa jinsia za kike na kiume kwa kuangazia uhusiano wao katika mazingira wanamoishi.

Utamaduni, mila na desturi za Kiafrika zinaaminika kuwa chanzo cha dhuluma na unyanyasaji ambao wanawake hupitia mikononi mwa wanaume. Wanawake wamejitolea mhanga ili kujikomboa kutokana na utamaduni dhalimu. Wanaume bado wameshikilia utamaduni uliopitwa na wakati kutokana na hali ya mazoea, jambo ambalo limechangia migogoro na kuathirika kwa uhusiano kati yao.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

(i) Asasi za jamii zimeathiri vipi mazingira ya utambulisho wa jinsia kupitia tamaduni zake?

(ii) Jinsia zimeathirika vipi kutokana na changamoto zinazopitia kufuatia harakati za kutaka

kujitambua na kutambuliwa na jamii?

(iii) Fasihi kama nyenzo muhimu imechangia vipi kupatikana kwa mabadiliko katika mielekeo ya jamii?

## 1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu una madhumuni yafuatayo;

(i) Kubainisha jinsi asasi za jamii kupitia tamaduni zake zinavyoathiri mazingira ya utambulisho wa jinsia.

(ii) Kuangazia namna jinsia za kike na kiume zinavyoathirika kutokana na changamoto zinazopitia kufuatia harakati za kutaka kujitambua na kutambuliwa na jamii.

(iii) Kudhihirisha mabadiliko ya mielekeo ya jamii kupitia fasihi kama nyenzo muhimu inayochangia mabadiliko hayo.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Tafiti kadha za hapo awali zimeshughulikia masuala ya wanawake ya ukombozi, unyanyaswaji na dhuluma wanazopitia katika jamii za Kiafrika na kupuuza masuala ya wanaume. Hivyo tafiti hizi zinaonekana kuwa na pengo ambalo linastahili kujazwa na watafiti wengine wa fasihi ya Kiswahili. Ili kujaza pengo hili, tumechagua mada hii kwani inashughulikia masuala ya jinsia kama yanavyojitokeza katika mazingira halisi ya Kiafrika.

Jamii imepuuza jinsia ya kiume kutokana na fikra kuwa ina uwezo wa kujitetea na kukabiliana na changamoto inayokumbana nazo. Jambo hili limechangia hali yao ya upweke kwani hakuna anayewafikiria wala kuwatetea kama inavyofanyiwa jinsia ya kike. Watetezi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika wanaopigania ukombozi wa wanawake, haki na usawa pia, wananuia kuwapa wanawake mwelekeo mbadala kwa msingi wa utamaduni wa kimapokeo ilhali wanaume wamesalia kufuata mwelekeo wa utamaduni wa kimapokeo kwa kukosa mwelekeo mbadala kama wanawake jambo ambalo linaathiri uhusiano wao zaidi.

Tofauti na kazi nyingine za fasihi ambazo wasanii wamewachora wanawake kwa njia hasi, utafiti wetu umedhihirisha upekee wa mwandishi Habwe kwa kuwachora wanawake kutegemea mitizamo na tajiriba zao wala si kuwachora kutokana na tajiriba au matarajio ya wanaume. Pamoja na haya hakuna ushahidi kwamba kumewahi kuwa na utafiti uliofanywa kuhusu utambulisho wa

jinsia katika *Maumbile Si Huja* na *Paradiso* kwa kuegemea mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti wetu umejikita katika kazi mbili za John Habwe

a) *Maumbile si Huja* (1995)

b) *Paradiso* (2005)

Tumezichanganua kwa lengo la kutathmini mchango wa mwandishi katika kuwaangazia mwanamke na mwanamume ili kuzindua jamii kuhusu changamoto wanazokumbana nazo katika harakati za kutaka utambulisho kwa msingi wa utamaduni wa Kiafrika kupitia asasi za ndoa, dini, siasa, elimu, uchumi na utamaduni. Tumechanganua namna ambavyo mwandishi amewachora wahusika wake na kufafanua mtagusano wao katika mazingira halisi ya Kiafrika. Msanii amewatumia wanawake kama wahusika wakuu na kuwachora kama viumbe walio na uwezo wa kujiamulia mambo na kujitegemea. Tumechanganua uhusiano wa jinsia na kuchunguza mabadiliko ya mielekeo ya jamii kwa msingi wa utamaduni wa Kiafrika katika asasi tofautitofauti za jamii.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Msokile (1993) anasema kuwa nadharia ni mawazo, mwongozo, mpango au maelezo yaliyowekwa kusaidia kutekeleza jambo fulani. Kulingana na Wamitila (2008) nadharia ni maarifa ya kitaalamu na kimsingi anayostahili kufahamu msomaji au mhakiki kabla ya kuanza shughuli ya kuchanganua kazi yoyote ya fasihi. Hivyo basi, nadharia ni maarifa anayostahili kuwa nayo mhakiki kabla ya kujihusisha na kazi yoyote ya uhakiki. Nadharia humwezesha mhakiki kuwa na uelewa mpana wa kazi za fasihi. Nadharia humwongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uchambuzi wa data yenyewe. Utafiti wetu umeongozwa na kuwekewa msingi na nadharia ya Ufeministi hususan Ufeministi wa Kiafrika ambayo imetuwezesha kuchanganua masuala ya uhusiano wa wanaume na wanawake katika harakati zao za kutafuta utambulisho. Nadharia hii

imetuwezesha kuangazia jinsi msanii amewasawiri wahusika wake kwa kuwapa majukumu kulingana na uwezo wao na kubainisha uhusiano wao katika mazingira wanamoishi.

### 1.7.1 Nadharia ya Ufeministi

Nadharia ya Ufeministi ni ya mtazamo wa kike unaokinzana na mikabala ya kiumeni inayoonekana kuwapendelea wanaume na kuwanyanyasa wanawake. Waasisi wa Nadharia ya Ufeministi ni pamoja na Wollstonecraft (1972) katika kitabu chake cha *A Vindication of the rights of women* kinachotetea haki za mwanamke kwa kuonyesha dhahiri mambo wanayopitia. Wollstonecraft anapendekeza kuundwa kwa jamii mpya iliyo na usawa. Yeye ni miongoni mwa wasanii ambao ni watetezi sugu wa haki za jinsia. Anasema kuwa elimu ni muhimu katika harakati za ukombozi wa jinsia. Anapendekeza kuwa wasichana wapewe elimu ili wawe na nafasi sawa na wavulana katika kupigania haki zao. Wolf (1929) katika *Room of One's Own* pia anapigania haki za mwanamke. Wolf anasema kuwa, ili mwanamke awe huru ni lazima awe na elimu na pesa ili aweze kujitegemea na kujiimarisha kimaendeleo. Nadharia hii inapinga asasi yoyote inayomdhulumu mwanamke na kumpendelea mwanamume. Wafuasi wa nadharia hii wanapigania usawa pasi na kuzingatia maumbile.

Ufeministi umepiga hatua kwa kuungwa mkono na watu wengi. Masuala ya Kifeministi yalianzishwa na wanawake wa rangi nyeusi waliokuwa wakipigania haki zao kutokana na ukandamizwaji chini ya utawala wa Ufalme wa Waingereza. Wanawake hawa walinyimwa haki za kibinadamu kwa kutengwa na kufanywa watumwa kutokana na rangi yao. Hii ndiyo ilikuwa sababu ya wanaharakati kutambua umuhimu wa kupigania uhuru wa jinsia na kupelekea kusaili miundo ya kitamaduni iliyoasi haki za jinsia kwa kuegemea rangi na utabaka. Mawazo haya ndiyo yalichangia zaidi harakati za kupigania usawa wa jinsia.

Nadharia ya Ufeministi imedhihirisha mitazamo kadha inayochangia kuwepo kwa matapo mbalimbali ya Ufeministi kwa misingi ya itikadi na maeneo kama anavyosema Muffin (1991) kuwa mambo yanayoathiri wanawake yanatofautiana kimaeneo. Muffin amefafanua Nadharia ya Ufeministi kulingana na maeneo na kuigawa katika matapo manne: Ufeministi wa Kifaransa, Ufeministi wa Kimarekani, Ufeministi wa Kiingereza na Ufeministi wa Kiafrika. Kwa muhtasari, Ufeministi wa Ufaransa unakusudia kufafanua lugha inavyotoa maana ya mtumizi na hutumiwa

kama zao la taasumbi za kiume. Ufeministi wa Kiafrika umejikita katika shughuli za kuangazia utamaduni wa Kiafrika unaomkandamiza mwanamke na kumtukuza mwanamume. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa mkabala wa kiitikadi unahusu mitazamo mitatu mikuu ya Ufeministi: Ufeministi huru, Ufeministi wa Kijamii na Ufeministi wa Kimapinduzi. Ufeministi huru unapigania usawa wa kijinsia, Ufeministi wa Kijamii unapigania kuwashirikisha wanaume katika majukumu yote ya nyumbani yakiwemo ulezi wa watoto ilhali Ufeministi wa Kimapinduzi unapinga ukandamizwaji wa mwanamke mikononi mwa mwanamume. Maelezo haya yanapigwa jeki na utafiti wetu unaoegemea mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kuwa ndiyo nadharia inayoangazia vigezo vinavyozinyima jinsia usawa, ukombozi na mwelekeo mwafaka wa kukabiliana na changamoto zinazotokana na harakati za kutafuta usawa na ukombozi.

Isitoshe, Steady (1981) anasema kuwa Ufeministi wa Kiafrika umejikita katika kuangazia majukumu ya jinsia kwani yanategemeana na kukamilishana kwa malengo ya kuendeleza jamii husika. Ufeministi wa Kiafrika unanuia kuleta ukombozi wa Waafrika kwa kushirikisha wanaume kama washikadau katika harakati za kupigania kubadilishwa kwa utamaduni wa Kiafrika unaowakandamiza wanawake au kutupiliwa mbali kabisa.

### 1.7.1.1 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

Waasisi wa Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni pamoja na Steady (1981) anayeshughulikia masuala yanayowaathiri wanawake wa Kiafrika. Nadharia hii inapinga utamaduni unaobagua jinsia kwa msingi wa majukumu na kupigania usawa kwa kumchora mwanamke kama kiumbe wala si kiumbe jinsia. Ufeministi wa Kiafrika unazitambua jamii za Kiafrika zinazotawaliwa na wanawake mashujaa na kupigania ukombozi wa watu wote wa Afrika na wala si wanawake tu.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetufaa kushughulikia masuala ya jinsia kwa msingi wa Utamaduni wa Kiafrika kama inavyotokea katika kazi teule kwa kuwa inachunguza utamaduni unaomtweza mwanamke na kumtukuza mwanamume. Vichocheo vya unyanyasaji, dhuluma na ubaguzi wa mwanamke vinatokana na athari za ukoloni mamboleo kupitia majukumu ya jinsia. Nadharia hii kupitia mihimili yake inatambua vipengele vya utamaduni wa Kiafrika vinavyochangia ubaguzi wa jinsia ya kike na kutoa mapendekezo ya suluhu kwa masaibu haya.

Wafuasi wa nadharia hii wanashinikiza kuwashirikisha wanaume katika harakati za kupigania ukombozi wa wanawake. Wanasisitiza kuwa ili Ufeministi wa Kiafrika uweze kufanikisha malengo yake ni muhimu kushirikisha jinsia za kike na kiume. Jambo ambalo ni tofauti na matawi mengine ya Ufeministi kwa mfano, Ufeministi wa Kimagharibi, ambapo wanawake hawana nia ya kuwashirikisha wanaume katika harakati za kutafuta ukombozi. Msimamo wa wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika unakosoa msimamo wa Ufeministi wa Kimagharibi unaoshikilia kwamba, mwanamume ndiye adui mkubwa wa mwanamke na kamwe mwanamume hawezi kushirikishwa katika harakati za kutafuta ukombozi wa mwanamke. Nadharia ya Ufeministi wa Kimagharibi inaunga mkono ndoa za jinsia moja kitendo kinachopingwa vikali na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inayopigania ndoa za jinsia tofauti zinazojengwa kwa mapenzi, heshima na uelewano.
Steady anafafanua nadharia hii kwa msingi wa sifa zifuatazo;

a) Kuleta usawa wa kijinsia kwa kupigania jamii iliyo na msingi wake katika majukumu ya kijinsia na kupinga majukumu yanayotokana na maumbile hasa ya kike yaliyopitwa na wakati na kuchukiwa na wanawake wengi.
b) Kujenga hisia na mshikamano wa wanawake kama kundi linalobaguliwa na kudhalilishwa.
c) Kutumia fasihi kama nyenzo za kuchunguza na kudhihirisha hali halisi anamoishi mwanamke katika jamii.
d) Kubadilisha maono ya wanawake kama wanavyojichukua na kuimarisha uhusiano wao kama wanawake.

Steady anasisitiza kuwa, nadharia hii inaangazia hali za jamii za Kiafrika kwa msingi wa tamaduni zao zinazochangia unyanyasaji wa jinsia ya kike. Anasema kuwa mwanamke wa Kiafrika ni mtetezi wa usawa wa kijinsia akilinganishwa na mwanamke wa Kimagharibi. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kama vuguvugu la mabadiliko inasisitiza wanaume kushirikishwa katika harakati za kupigania haki na usawa wa kijinsia. Tumetumia Ufeministi wa Kiafrika kama Ufeministi unaojihusisha na utambuzi wa vizuizi vinavyonyima jinsia usawa, haki na ukombozi na inayotupa njia za kukabiliana na vizuizi hivi ili kuondoa dhuluma za kijinsia zinazopatikana katika mazingira ya Kiafrika.

Ufeministi wa Kiafrika umetuwezesha kuangazia changamoto zinazopitia jinsia katika harakati za kutaka utambulisho na namna zinavyokabiliana na changamoto hizo. Tumechunguza uhusiano wa jinsia na kudhihirisha mabadiliko ya mielekeo ya jamii kwa msingi wa utamaduni wa Kiafrika. Kimsingi lengo letu kuu ni kuangazia harakati za ukombozi wa jinsia ya kike kutokana na utamaduni wa kimapokeo kwa kuegemea mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kutambua na kutambulisha jinsia kama inavyojitokeza katika kazi tunazochanganua kwani zinaakisi maisha halisi ya Kiafrika.

### 1.7.1.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

Fasihi inachangia pakubwa katika harakati za kushughulikia masuala ya jinsia kwa kuangazia majukumu na nafasi yake katika jamii. Mihimili ya nadharia hii imetuwezesha kudhihirisha umuhimu wa usawa wa jinsia kwa kuangazia uwezo wa mwanamke kujiamulia mambo na kujitegemea wala si kama kiumbe dhaifu na mtegemezi wa mwanamume. Tumeweza kuthibitisha mchango wa mwanamke katika maendeleo ya jamii kutokana na uwezo wake kiuchumi na ushirikiano wake na wengine. Kwa jumla nadharia hii imetuwezesha kuangazia changamoto wanazopitia jinsia katika asasi za jamii kwa kutafuta utambulisho na kubainisha mabadiliko ya mielekeo ya jamii yalivyowekewa msingi na utamaduni wa Kiafrika. Mihimili ambayo tumetumia ni pamoja na;

a) Usawa wa kibinadamu

Dhamira kuu ya nadharia hii ni kuleta usawa wa kijinsia. Inanuia kujenga jamii mpya ambayo imetenga majukumu kwa kutegemea jinsia wala si maumbile. Mhimili huu umetuwezesha kushughulikia dhana hii ya usawa na harakati zilizochangia kufanikisha matakwa hayo katika vitabu teule. Ni vyema kufahamu kuwa utamaduni na uana huchangia pakubwa migogoro inayopatikana katika jamii yoyote. Ili pawe na usawa, wahusika katika kazi za fasihi huchorwa wakivutana na kupigania nafasi zao kwa sababu za kutaka kujitambua na kutambuliwa na jamii kama inavyojitokeza katika kazi tulizoteua.

b) Uhusika na Wahusika

Wahusika wana majukumu muhimu katika kazi za fasihi kufanikisha malengo ya mwandishi na kupitisha ujumbe uliokusudiwa. Hivyo basi, ni muhimu kufanya uteuzi mwafaka wa wahusika kulingana na matendo yao, maelezo ya wahusika wengine na maelezo ya msimulizi ili kusitokee maana kinyume na matarajio ya msanii. Uteuzi wa wahusika unastahili kuzingatia mazingira na muktadha wa matukio. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inatilia mkazo usawiri wa wahusika wa kike walio na sifa kielelezo. Wanawake wanaojitegemea kimawazo na kiuchumi, ambao wamebobea kielimu, wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali uongozini na ambao wamejitosa katika uwanja wa siasa uliochukuliwa kuwa ni uwanja wa wanaume tu. Kando na kutumia wahusika wa kike, mwandishi ana uhuru wa kuwashirikisha wahusika wa kiume wanaofuata utamaduni wa kimapokeo unaokandamiza wanawake na ambao wanajaribu kujikwamua kutokana nao kwa nia ya kuendeleza harakati za kupigania haki na usawa wa kijinsia. Mhimili huu umekuwa na manufaa kwetu kwani umetusaidia kudhihirisha namna watu wanajitahidi katika harakati za kupata utambulisho chanya katika jamii.

c) Umoja wa wanawake

York na wenzake (1991) wanasema kwamba kundi la wanawake wanaopitia changamoto ndilo linalopata ari ya kutaka kupigania haki kwa ushirikiano wao. Nadharia hii inakusudia kuleta mwamko mpya kwa mwanamke tofauti na anavyojiona na kujichukulia. Vilevile, inanuia kuimarisha uhusiano wake na watu wengine akiwamo mwanamke mwenzake. Kwa sababu matatizo anayoyapitia mwanamke mmoja si yake peke yake bali ni ya kundi zima la wanawake. Ni vyema kuzingatia umoja wa wanawake na kupinga kauli kwamba mwanamke hawezi kushirikiana na watu wengine hata na mwanamke mwenzake. Mhimili huu umetufaa kwa kuangazia hali ya mwanamke wa Kiafrika anayejitegemea na mpenda ushirikiano na wenzake kwa nia ya kuwashirikisha katika harakati za kutaka utambulisho wa jinsia.

d) Usanii

Kwa kuwa lengo la Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ni kufafanua, kueleza na kuzindua jamii kuhusu hali halisi ya mwanamke na mwanamume wa Kiafrika, vipengele vyote vya fasihi hutumika kwa njia mwafaka ili kufanikisha dhamira hii. Uteuzi wa wahusika, maelezo yao pamoja na lugha inayotumika huwa ya kipekee na huandikwa kwa njia ya wazi ili yaeleweka kwa

urahisi. Mhimili huu umetuwezesha kuchambua lugha aliyotumia mwandishi pamoja na mbinu ya uteuzi wa wahusika pamoja na taswira yao ili kutathmini mazingira ya utambulisho wa jinsia katika asasi za ndoa, dini, utamaduni, uchumi na elimu.

e) Utamaduni

Tumeshughulikia Utamaduni wa Kiafrika. Mhimili huu umetuwezesha kupatia jinsia zote utambulisho kwa kuegemea vipengele vya utamaduni vya mavazi, watoto na malezi, urithi, ndoa na mahari

f) Dini

Mhimili huu umetuwezesha kuchanganua utambulisho wa jinsia kwa msingi wa dini za Kiislamu na Kikristo kwakuwa ndizo zimeenea zaidi katika nchi za Kiafrika. Dini imekukuwa ikitukuza jinsia ya kiume kwa kuitambua kama kichwa cha familia.

## 1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Lugano (1989) katika tasnifu yake,'Usawiri wa Wanawake Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii' katika vitabu vinne vya Kezilahabi vya *Rosa Mistika*, *Kichwa Maji*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka* kwa misingi ya Kimaksi. Kezilahabi amewachora wanawake kama viumbe tegemezi wa mwanamume, chombo cha anasa na kama chanzo cha maovu yote katika jamii. Maudhui aliyoshughulikia yametufaa kwa kuangazia michango yao katika utambulisho wa jinsia katika mazingira wanamoishi. Tofauti na yeye tumeshughulikia utambulisho wa jinsia ya kike na kiume kwa kuegemea nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilhali yeye amejishughulisha na jinsia ya kike tu kwa msingi wa nadharia ya Ki- Marx ilhali.

Mosoti (1993) amehakiki maudhui katika tamthilia nne za Emmanuel Mbogo, *Giza Limeingia Tone la Mwisho*, *Watoto Wetu* na *Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Ametumia Nadharia ya Uyakinifu wa Kijamii. Baadhi ya maudhui ambayo amehakiki ni pamoja na dhuluma, ukombozi, usaliti, ubinafsi na nafasi ya mwanamke katika jamii. Kazi hii imetufaa kwa kutuelekeza namna ya kuchunguza utambulisho ya jinsia kwa kuangazia nafasi ya jinsia katika jamii na changamoto zinaopitia katika harakati za kutaka utambulisho ikiwemo dhuluma na ubinafsi kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

Ndung'u (1996) amehakiki fani na maudhui katika kazi za Katama Mkangi za *Ukiwa*, *Mafuta* na *Walenisi* kwa msingi wa nadharia ya Umitindo. Kazi hii ni tofauti na yetu kwani tumetumia

nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kuwapa jinsia utambulisho katika kazi za John Habwe za *Paradiso* na *Maumbile Si Huja.* Utafiti huu umekuwa wa manufaa kwetu kwa kutupa mwelekeo wa namna ya kuchanganua fani za wahusika, lugha na maudhui katika kazi tulizoteua.

Musyoka (1996) amechunguza fani katika tamthilia nne za Kitsao ambazo ni *Uasi*, *Malimwengu Ulimwenguni*, *Bibi Arusi* na *Tazama Mbele*. Amechanganua vipengele vya fani kwa madhumuni ya kubainisha ufaafu na udhaifu unaopatikana katika uumbaji wa viambajengo vya fani katika usambamba wa msingi na kaida za utanzu wa tamthilia. Musyoka ametumia nadharia ya Umuundo kufafanua fani kama umbuji wa kipekee unaohusiana na mtindo wa mwandishi. Kwa kifupi ametathmini umbuji wa msanii na jinsi fani inavyoathiri na kuchangia kuimarisha usanii wa kazi husika. Utafiti huu umetupa mwelekeo wa kuchanganua fani hususan inavyotumika kujenga maudhui kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

Magoma (1997) amehakiki 'mwamko wa mwanamke' katika tamthilia nne za Peninah Muhando*; Hatia*, *Heshima Yangu*, *Nguzo Mama* na *Lina Ubani*. Hata ingawa utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa umechanganua utamaduni, itikadi, mila, mapenzi na ndoa, mwanamke na elimu, taasubi za kiume pamoja na siasa na mwanamke, umetufaa kwa kutupa mwongozo wa kuchanganua changamoto zinazopitia jinsia katika harakati za kutaka utambulisho kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

Magare (2002) amehakiki tamthilia ya S. A Mohammed *Amezidi* kwa kutumia nadharia ya Udhanaishi akizingatia kipengele cha ubwege. Amechanganua *Amezidi* kama kazi ya kibwege kwa kuzingatia yaliyomo (maudhui) na fani. Magare amechanganua fani ya wahusika na uhusika, mazingira, lugha katika mawasilianao na ploti ili kudhihirisha namna ambavyo fani hizi zimechangia ubwege katika kazi husika. Kazi hii ina manufaa kwetu kwani imetupa mwelekeo wa kuchanganua wahusika na uhusika, maudhui na lugha kama vipengele vya fani vinavyotumiwa kuwatambua wahusika katika kazi za Habwe za *Maumbile Si Huja* na *Paradiso* kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika .

Mwita (2005) anasema kuwa kutokana na mfumo wa ubabadume uliojikita katika jamii ya Wakuria, hali halisi ya mwanamke inaonekana kuwa ya dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji. Mwanamke amechorwa kama kiumbe tegemezi asiye na uwezo wa kujiamulia mambo kwani

kufanya hivyo ni mwiko katika jamii hiyo, hali ambayo imeenea katika jamii nyingine nyingi za Kiafrika. Japo tunakubaliana naye kwa kiasi fulani, mambo yamebadilika sana kutokana na uhamasishaji kwa umma kuhusu masuala ya wanawake. Hata ingawa kazi yake ni tofauti na yetu, imetusaidia kushughulikia masuala ya wanawake katika mazingira ya Kiafrika kwani inahusu jamii ya Kiafrika 'Dhima ya Ichingero ya Wakuria Katika Kusawiri Taswira ya Mwanamke.'

Maina (2005) anasema kuwa kitendo cha mwanamke kulipiwa mahari anapoolewa humfanya kuwa mali ya mumewe na hili ni tatizo kubwa. Gibbe anavyonukuliwa na Maina (2005) anasema kitendo hiki kinamnyima mwanamke uhuru wa kunena kwani'amenunuliwa'. Gibbe anasema kuwa dhana 'olewa' ina maana ya 'kumilikiwa'. Jambo hili si rahisi kufutika akilini mwa wanajamii na linapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika. Isitoshe, dhana hii inachangia kugandamizwa na kudhulumiwa kwa mwanamke katika ndoa kwani akimwacha mumewe, wazazi wake watalazimika kurudisha mahari aliyolipa mumewe. Tendo hili ni la aibu kwa mwanamke huyu na ukoo wake mzima. Kauli hii inajitokeza Maina anapohakiki nafasi ya mwanamke katika tenzi mbili za Shaaban Robert, *Utenzi wa Hati* na *Utenzi wa Adili*a kwa msingi wa Nadharia ya Ufeministi. Kazi hii imetupa mwelekeo mwafaka wa kuchanganua masuala ya wanawake kwa msingi nadharia sawa na yake ya Ufeministi wa Kiafrika.

Katola (2006) katika utafiti wake wa dhuluma dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili kwa msingi wa Ufeministi wa Kiafrika, anasema kwamba, baadhi ya asasi za kijamii ndizo zinazotumiwa kumdhulumu mwanamke na zinastahili kutupiliwa mbali la sivyo zifanyiwe marekebisho. Kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika anapinga ulipwaji mahari kwa kuwa humfanya mwanamke kuwa mali ya mwanamume na humnyima mwanamke nafasi ya kumiliki chochote. Mwanamke ananyimwa uhuru wa kutoa maoni au uamuzi. Mwanamke wa Kiafrika anastahili na kuridhika na yale anayopatiwa na mumewe pasi na kulalamika. Tofauti na utafiti wetu, tumetumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kuzitambua jinsia ya kike na kiume kama zinavyojitokeza katika mazingira halisi kinyume na fikra kuwa jinsia ya kike ni dhaifu na isiyo na uwezo wa kujiamulia mambo.

Maobe (2011) ametafitia 'Ukombozi wa Mwanamke' katika kazi za John Habwe za *Maumbile si Huja* na *Fumbo la Mwana*. Anazungumzia dhuluma anazopitia mwanamke maishani mwake kama vile ndoa ya lazima, ubaguzi katika uongozi, ubaguzi kielimu miongoni mwa dhuluma nyingine.

Maobe anasema kuwa japo mwanamke anapitia changamoto kadha, ameonyesha ukakamavu, ukomavu na ujasiri katika harakati za kupigania ukombozi, haki na usawa na kushirikisha jinsia ya kiume katika harakati zake za kutafuta ukombozi. Japo utafiti huu pia umefanywa kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, unatofautiana na wetu kwani tumewapa jinsia utambulisho kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hata hivyo, utafiti huu umetupa mwelekeo wa kuchanganua baadhi ya maudhui kama vile ya ndoa na dhuluma kama zinavyojitokeza katika kazi teule.

Muhando (2011) ametafiti kuhusu 'Nafasi ya Dini Katika Ndoa' kwenye*Utengano* na *Paradiso.*' Mtafiti huyu ameshughulikia nafasi ya dini za Kikristo na Kiislamu katika ndoa kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani ameipa uzito suala la ndoa katika dini ilhali sisi tumeangazia namna ambavyo jinsia inapatiwa utambulisho katika asasi ya dini tofauti na asasi ya ndoa. Utafiti huu umetupa mwanga na mwelekeo wa kuchanganua masuala ya dini za Kikristo na Kiislamu pamoja na ndoa za Kiafrika yanavyozipa jinsia utambulisho tukiegemea mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

Mirikau (2011) katika utafiti wake 'Taswira ya Mwanamke' katika tamthilia za Wamitila K.W *Seserumbe*, *Pango* na *Wingu la Kupita* amezungumzia dhuluma anazopitia mwanamke katika asasi za jamii kama vile unyanyasaji katika ndoa kwa kupigwa na kuzalishwa watoto wengi, wanaume kuchukulia wanawake kama vyombo vya anasa, ukeketaji miongoni mwa dhuluma nyingine. Japo mwanamke anapitia changamoto hizi, Mirikau anampa hadhi kwa kummiminia sifa za ujasiri, usomi, ukarimu, ukombozi na utetezi wa haki za wanyonge. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwani ameshughulikia jinsia ya kike peke yake ilhali sisi tumechanganua utambulisho wa jinsia ya kike na kiume kwa kuegemea nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Hata hivyo, utafiti huu umetupa mwelekeo wa kushughulikia changamoto jinsia zinazopitia katika harakati za kutaka utambulisho.

Maingi (2011) ameshughulikia Upembezwaji wa Wanawake kama Udokezi wa Nafasi ya Mwanamke katika *Utenzi wa Fatuma*. Mwanamke amenyimwa uhuru wa kutoa maoni na maamuzi katika jamii. Maingi ametumia fani ya lugha kubainisha nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kuchora picha ya Fatuma kabla ya kuolewa, wakati wa posa na maisha yake katika ndoa duniani na mbinguni. Tofauti na utafiti wetu, amehakiki utanzu wa shairi kwa kuchanganua na

kuchunguza nafasi ya jinsia ya kike ilhali sisi tumetathmini utambulisho wa jinsia ya kike na kiume katika mazingira wanamoishi. Utafiti huu umekuwa wa manufaa kwetu kwa kutujuza jinsi ya kuchanganua changamoto wanazopitia jinsia za kike na kiume katika harakati za kutaka kutambuliwa na kujitambua katika jamii.

Obure (2012) ametafiti kuhusu ' Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike' katika kazi za *Tumaini* na *Rosa Mistika*. Anaangazia udhalilishaji na udunishaji wa wasichana katika jamii kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Dhuluma hizi ni pamoja na kupigwa, kubakwa, kupachikwa mimba kupitia mapenzi ya uwongo, kunyimwa nafasi ya elimu, kutahiriwa miongoni mwa dhuluma nyingine. Japo utafiti huu ni tofauti na wetu, umetuwezesha kufafanua dhuluma zinazopitia jinsia katika harakati za kutaka utambulisho kwa kuegemea nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika.

Onyoni (2012) ametafiti juu ya 'Usawiri wa Wahusika wa jinsia ya kike' katika tamthilia za *Mama Ee* na *Natala'* . Ametumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kuchanganua jinsi wanaume wanavyowagandamiza na kuwadhulumu wanawake kwa kutumia vipengele vya fani vya wahusika, mandhari na lugha kama inavyotumiwa kuwasawiri wanawake. Hata ingawa utafiti huu ni tofauti na wetu kwani, sisi tumetambua na kutambulisha jinsia kwa msingi wa Ufeministi wa Kiafrika, umetufaa kwa kutupa mwelekeo wa kuchanganua wahusika na uhusika katika harakati za kutaka utambulisho.

Timammy na Swaleh (2013) katika makala yao wamechambua na kutathmini uhusika na athari zake kwa utambulisho wa jinsia katika *Maumbile si Huja* kwa msingi wa nadharia ya Uhakiki wa Jinsia na Umitindo. Kazi hii imekuwa na manufaa kwetu kwani imetupa mwelekeo wa kuchanganua maudhui na fani hususan wahusika, kwa kuwapa utambulisho kwa msingi wa utamaduni wa Kiafrika na kuonyesha uhusiano wao katika mazingira yao kwa kuegemea mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika katika kazi tulizoteua za *Paradiso* na *Maumbile si Huja*. Utafiti huu umetupa mwanga wa kuchanganua baadhi ya maudhui na kudhihirisha mtindo wa mwandishi wa kutambua wahusika kama watu walio na uwezo sawa katika kutekeleza majukumu yao.

Karinge (2013) ametafiti juu ya 'Usawiri wa Ndoa katika *Unaitwa Nani* ?' Ameshughulikia ndoa na changamoto zake kama vile itikadi za jamii, ukosefu wa imani katika ndoa pamoja na udanganyifu. Karinge ameangazia harakati za kutunza ndoa na jamii kwa jumla. Hata ingawa mada hii ni tofauti na yetu, imetupa mwelekeo wa kuchanganua na kuchunguza changamoto zinazopatikana katika asasi ya ndoa na namna ya kukabiliana na changamoto hizi. Japo Karinge ametumia nadharia ya Sosholojia, sisi tumetumia nadharia za Ufeministi wa Kiafrika kutambua na kutambulisha jinsia kupitia asasi za kijamii ikiwemo ndoa. Mihimili ya nadharia yake imetuwezesha kutathmini uhusiano na ushirikiano wa jinsia katika mazingira wanamoishi.

Kipyegon (2013) katika tasnifu yake ameshughulikia'Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke Katika tamthilia za *Natala* na *Kifo Kisimani.*' Kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mtafiti anamsawiri mwanamke kama kiumbe tegemezi, mlezi na kama chombo cha kufurahisha mwanamume. Kipyegon amechanganua changamoto anazokumbana nazo mwanamke katika kujaribu kupigania usawa na ukombozi. Hata ingawa utafiti huu ni tofauti na wetu kwani sisi tumetambua na kutambulisha jinsia, umetufaa kwa kutupa mwelekeo wa kuchanganua changamoto zinazopitia jinsia katika harakati za kutaka utambulisho.

Chacha (2013) ameshughulikia 'Taswira ya mwanamke katika tamthilia za *Nguzo Mama* na *Mama Ee*' kwa kuangazia shida za unyumba, ubaguzi wa jinsia ya kike, dini, uhusiano wa jinsia ya kike, wahusika kati ya masuala mengine kwa msingi wa Ufeministi wa Kiafrika. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa sisi tumetambua na kutambulisha jinsia katika *Paradiso* na *Maumbile si Huja* kwa msingi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa kutupa mwelekeo wa kuchanganua kipengele cha fani cha wahusika na kuangazia uhusika na changamoto zinazotokana na harakati za kutaka utambulisho.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni jumla ya njia zote tumetumia katika utafiti huu kuanzia uteuzi wa sampuli, ukusanyaji na uchanganuzi wa data hadi uwasilishaji wa data hizo. Uchunguzi wetu umekuwa wa maktabani. Mwanzo, tumeteua sampuli zetu zilizokuwa matini lengwa za kutathmini mazingira ya utambulisho wa jinsia ambazo zilihitajika katika utafiti wetu. Tumeteua kazi za mwandishi John Habwe za *Maumbile si Huja* na *Paradiso*. Baadaye tumesoma, tukadondoa na kuorodhesha

masuala yanayohusu tabia na mienendo ya wahusika katika harakati za kutaka utambulisho kwa kuzingatia mwelekeo wa jamii kama ulivyowekewa msingi na utamaduni wao. Tumedondoa na kuchanganua maudhui waliyobebeshwa wahusika kama yalivyoonyeshwa na mwandishi wa kazi teule.

### 1.9.1 Uteuzi wa Sampuli

Tumeshughulikia vitabu viwili vya John Habwe vya *Maumbile si Huja*(1995) na *Paradiso*(2005). Tumesoma vitabu hivi kwa lengo la kukusanya data za kutambua na kutambulisha jinsia katika kazi hizi. Data ambayo tumeshughulikia imechaguliwa kimakusudi ili kupata matini toshelezi.

### 1.9.2 Ukusanyaji wa Data

Data ya kimsingi ambayo imetumika katika utafiti huu imekusanywa maktabani kwa kujikita katika *Maumbile si Huja* na *Paradiso.* Kazi hizi zimechaguliwa kimaksudi kuzingatia utambulisho wa jinsia katika asasi za jamii za Kiafrika. Wahusika wanaopatikana katika kazi hizi ni Waafrika wanaoishi katika mazingira ya Kiafrika na mwandishi ni Mwafrika anayeelewa masuala ya Kiafrika. Vilevile, tumepata data nyingine kutoka kwenye tafiti za hapo awali, majarida na kwenye mtandao.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data umefanywa ili kutambua na kutambulisha jinsia katika mazingira yao halisi. Tumetathmini namna ambavyo mwandishi amewapa wahusika wake utambulisho kwa msingi wa Utamduni wa Kiafrika kupitia asasi za jamii kwa kuongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Pia, tumeangazia athari za changamato zinazopitia jinsia kutokana na harakati za kutaka utambulisho na mabadiliko katika mielekeo ya jamii kama ilivyowekewa msingi na utamaduni wa Kiafrika.

### 1.9.4 Uwasilishaji wa Data

Data ambayo tumekusanya kutoka katika kazi teule, majarida na kazi mtandaoni, tumezichanganua na matokeo tumewasilisha kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti wetu. Maelezo haya yanahusu utambulisho wa jinsia katika asasi za jamii, athari za changamoto jinsia zinakumbana nazo kutokana na harakati za kutaka utambulisho na mabadiliko katika mielekeo ya jamii kwa msingi wa Utamaduni wa Kiafrika.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa kinadharia na mbinu za utafiti.

Utafiti wetu wa 'Utambulisho wa Jinsia' umejikita katika kazi za mwandishi John Habwe za *Maumbile Si Huja* na *Paradiso*. Kazi hizi zimekuwa mwafaka kwetu kwa kuwa zinaakisi mazingira ya Kiafrika mbali na kuandikwa na mwandishi wa Kiafrika anayeelewa masuala ya Kiafrika. Utafiti wetu umehusisha jinsia ya kiume kama washikadau katika harakati za kupigania usawa na ukombozi wa jinsia za kike na kiume.

Kwa kuegemea mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, tumeweza kushughulikia masuala ya wanawake na wanaume wa Kiafrika kwa kina. Tumewafuata kwa makini wahusika wakuu wa kike na kiume na kutathmini uhusiano wao katika mazingira wanamoishi.

# SURA YA PILI

## UTAMBULISHO WA JINSIA KATIKA ASASI ZA JAMII

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumetathmini mazingira ya utambulisho wa jinsia katika asasi za jamii zikiwamo ndoa, dini, elimu, siasa, mifumo ya uchumi na utamaduni. Asasi hizi zimeangaziwa zaidi na mwandishi wa vitabu teule na ndizo tumetumia kufafanua hoja zetu kwa lengo la kuangazia maisha halisi ya binadamu katika mazingira anamoishi.

## 2.2 Ndoa

Ndoa ni muungano wa hiari kwa watu wa jinsia tofauti wanaunganishwa kama mume na mke kufuatia makubaliano yao kisheria na yanaweza kuvunjwa tu na kisheria. Ndoa ni taasisi inayopatikana katika kila jamii ulimwenguni na kwa sababu hii huwa na mielekeo anuwai inayotofautiana kulingana na tamaduni za takribani ya jamii za ulimwenguni.

Kwa kuwa fasihi inaakisi jamii, ndoa tunazochanganua ni mifano ya ndoa katika jamii za Kiafrika. Jamii nyingi za Kiafrika zinathamini ndoa kiasi cha kuichukulia kuwa ni jambo la lazima. Kwa kuwa ndoa za Kiafrika zina mitazamo kadha inayotokana na tamaduni za Kiafrika, dini na mifumo ya sheria za nchi mbalimbali, fafanuzi zetu nazo zimeegemea misimamo ya tamaduni za Kiafrika, dini za Kiislamu na Kikristo ambazo ndizo zimeenea zaidi katika mataifa ya Kiafrika. Ili muungano wa ndoa utambuliwe ni sharti uzingatie kanuni zilizowekwa kwa misingi ya dini, utamaduni au sheria za nchi husika.

### a) Ndoa ya kitamaduni

Strobel (1979) anasema kuwa ndoa humnyanyasa mwanamke kwa kumpa nafasi chini ya mwanamume ambaye ni kiongozi wa familia au mji wake. Mwanamume ndiye mmiliki wa mali yote ya familia akiwemo mwanamke na watoto wao. Wamitila (2002) anasema ndoa ni mojawapo ya asasi ya kitamaduni inayojengwa kwa imani na uwezo wa mwanamume. Jamii inamtambua mwanamume kuwa nguzo katika ndoa na ndiye wa kutoa mwelekeo na kuheshimiwa. Utamaduni wa Kiafrika unamdhalilisha mwanamke kwa kumnyima uhuru wa kutoa maoni ila kufuata amri na mwelekeo wa mumewe hata kama haufai. Kila jamii ina utamaduni wake na ndivyo ilivyo mielekeo tofauti ya ndoa. Ndoa ni sehemu muhimu sana ya utamaduni wa jamii za Kiafrika kwani

inapanua jamii na kuendeleza ukoo kupitia watoto. Ndoa za Kiafrika hukamilika watoto wanapozaliwa na iwapo mtoto au watoto watakosekana, mipango ya kupata mtoto nje ya ndoa hufanywa kwa nia ya kufanikisha lengo la jamii la kupanua familia. Ndoa za kitamaduni zina vipengele vinavyomnyima mwanamke uhuru wa kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya vipengele hivi ni ukosefu wa uhuru wa kujiamulia kuwa mke au mzazi. Jamii inamlazimisha mwanamke kuolewa na kupata watoto pasi na kujali matakwa yake.

Utamaduni wa Kiafrika unaunga mkono ndoa za wake wengi ilmuradi mwanamume husika awe na uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya familia hiyo kama anavyotarajiwa na jamii. Mwanamume mwenye wake wengi hupendelewa zaidi katika uongozi kwa kudhaniwa kuwa kiongozi bora jambo ambalo linachangia baadhi ya wanaume Waafrika kuoa wake zaidi ya mmoja.

Utamaduni wa Kiafrika unatambua ndoa kama asasi inayojenga uhusiano mpya baina ya familia za pande mbili husika. Uhusiano huu hujengwa kupitia sherehe za harusi, kutembeleana na kupeana zawadi pamoja na sherehe za posa na ulipwaji mahari. Matukio haya huhakikisha kila familia imehusishwa katika ndoa hiyo kwa njia moja au nyingine. Jambo la muhimu ni kutambua jamii katika harakati za ndoa.

Hegedorn (1983) anadai kuwa vipengele vyote ambavyo vinachangia kuundwa kwa mfumo wa jamii ni muhimu kama vinatekeleza majukumu yanayolingana na matarajio ya jamii husika. Ndoa ni asasi inayostahili kuwa mazingira bora ya watoto kuzaliwa na kulelewa. Wanandoa na familia zao hupata utambulisho maalumu katika jamii kwa sababu binadamu hukamilika anapooa au kuolewa na kupata watoto kwani anapoaga, anaendelea kuishi kwa sababu watoto wake wanaishi. Mzazi aliye na watoto wengi huwa na hadhi ya juu akilinganishwa na mzazi aliye na watoto wachache katika jamii.

**b) Ndoa ya Kikristo**

Mungu alimuumba Adamu kwanza kisha Hawa kutoka ubavuni mwake na kuwaunganisha kama mume na mke. Mungu anampa mamlaka Adamu juu ya Hawa, Hawa akiwa msaidizi wa Adamu (Mwanzo 2:18, 24). Kusudi la Mungu kwa wanandoa ni uzazi kupitia mapenzi. Tofauti na ndoa

za kitamaduni ambapo wanandoa si lazima wapendane ndiposa waoane, ndoa za Kikristo zinasisitiza mwanamume kupenda mwanamke kama nafsi yake na mwanamke kumheshimu mumewe na kuwa mnyenyekevu. Njogu (1997) anasema kuwa ndoa inastahili kujengwa kwa mapenzi ya dhati wala si kwa pupa na ubinafsi unaochangia majonzi. De Genova (2008) anasema kuwa uhusiano kati ya Mungu na binadamu unaweza kumsaidia kuboresha uhusiano wake na binadamu mwenzake. Kwa hivyo mume au mke anastahili kumwona mwenzake kama zawadi kutoka kwa Mungu ili kuweza kukamilishana.

Ndoa ya Kikristo si mkataba wa jamii bali agano la roho linalounganisha watu wawili, mke na mume (Waefeso 5:31-33). Wachungaji wanaombea wanandoa baraka baada ya makubaliano ya wazazi wa pande zote mbili. Kulingana na madhehebu mengi ya Kikristo na yasiyo ya Kikristo, raida humpa bwana harusi nafasi ya kwanza kusema kama ana lolote kwa sababu za nadhiri kwa Mwenyezi Mungu mbele ya hadhira kisha bibi harusi.

Mwanamke anastahili kuwa msaidizi wa mwanamume kwa unyenyekevu na uvumilivu ilhali mwanamume anastahili kumpenda mkewe kama nafsi yake. Mungu ananuia kuleta umoja kati ya wanandoa, wasiwe tena watu wawili. Mungu ana wito kwa wanandoa kwamba, wasiwe tena watu wawili, miili miwili tofauti ila washikane kama mwili mmoja na walivyokuwa wanamtumikia na kushirikiana kabla ya ndoa, waendelee kumtumikia katika ndoa.

### c) Ndoa ya Kiislamu

Kama ilivyo dini ya Kikristo, dini ya Kiislamu pia inatoa mwelekeo wake katika ndoa. Jambo la muhimu kwa wanandoa ni kufanya uchaguzi bora wa mchumba ili kuwe na ndoa ya kudumu na yenye furaha. Katika Uislamu kama ilivyo katika Ukristo, mwanamume amepewa uwezo na mamlaka ya kuongoza taasisi ya ndoa. Ni jukumu la mwanamume kujenga taasisi hiyo akishirikiana na kusaidiana na mkewe kwa kila jambo. Mchumba anastahiki kushikilia sifa nzuri ya mwenzake na kupuuza kasoro kama anavyohimiza Mwenyezi Mungu.

Kuwa mwanamume bora wa Kiislamu hakutegemei utajiri, hadhi wala ubora wa haiba bali unyenyekevu, kuwa tayari kushirikiana na watu wa familia akiwamo mkewe. Dini ya Kiislamu

inatambua mwanamume mwenye huruma, upendo, mtafakuri, anayejali, asiye na kashfa na wala asiwe mtu wa kutoa amri hapa na pale. Kwa kuwa maisha mazuri ya ndoa yanahitaji imani katika mafunzo ya kidini na tabia nzuri, ni vyema kuwe na jihadi dhidi ya ujeuri, kiburi, ubinafsi, majivuno, ghadhabu na umimi. Iwapo mizozo inaweza kutokea katika ndoa isiyoweza kutatuliwa, dini ya Kiislamu kama jambo la mwisho inapendekeza talaka au hata kumwacha bibi au bwana katika hali hiyo hiyo. Dini ya Kiislamu inatambua ndoa ya wake zaidi ya mmoja kinyume na dini ya Kikristo inayotambua ndoa ya mke mmoja mume mmoja:

### 2.2.1 Ndoa katika *Maumbile Si Huja*

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unapinga wazo kuwa mwanamke anastahili kuvumilia changamoto anazokumbana nazo na kuangaza madhila anayopitia mwanamke katika ndoa. Nadharia hii inapendekeza kuwa mwanamke anayedhulumiwa na mumewe awe huru kuingia katika ndoa nyingine au kuishi bila kuolewa. Juma anaoa Amina kwa msingi wa kidini na kitamaduni. Ndoa hii inatambuliwa kupitia changamoto kama vile ukosefu wa mapenzi na heshima kwa sababu ya Juma kupenda mali yake kuliko mkewe kama inavyojitokeza katika mawasiliano kati yao:

> "Njoo hapa wewe. Mbona umejikunyata kama yatima? Umekosa nini? Mali?" Juma alisalia huku kabadili raha yake ya muda na kuwa kama ndume aliyehasiwa. (uk. 3)

Dini inamtambua mwanamke mvumilivu na mnyenyekevu ilhali mwanamume kama kichwa cha familia, anatarajiwa kumpenda na kumheshimu mkewe. Utamaduni wa Kiafrika pia unapendelea mwanamume kwa kumtambua kama kichwa cha familia anayestahili kutoa mwongozo na mwelekeo katika familia. Mwanamke anastahili kufuata mwelekeo huu hata kama haufai. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika unaendeleza hoja kwamba, mwanamke anayeonyeshwa mapenzi na heshima hunyenyekea na kuvumilia akilinganishwa na mwanamke asiyependwa wala kuheshimiwa na mumewe na kupinga utamaduni wa kitaasubi unaomnyima mwanamke uhuru wa kupenda na kupendwa. Kutokana na ukosefu wa mapenzi katika baadhi za ndoa, wanawake wanakosa uvumilivu wala unyenyekevu kwa upande wa mwanamke. Amina anatambuliwa kama mwanamke anyayenyanyaswa na jamii kwa kumshinikiza kudumisha ndoa yake na kupuuza mchango wa mumewe katika kudumisha ndoa iyo hiyo kama anavyosema Amina:

> Ndugu mpenzi, mali si kitu. Kitu ni kuheshimiana na kuvumiliana katika raha na taabu. Sina uhuru. Kama njiwa nimo kizimbani. Jamii imenitia kibandani, utamaduni wa Kitaasumbi umenishindilia humo na nguvu za mwanamme zinanikalisha humo. Natafuta mpenzi wa kunivua matesoni. Nikivuliwa nitaimba wimbo wa uhuru. (uk. 46)

Utamaduni wa Kiafrika unampa mwanamke majukumu ya kutekeleza kazi zote za nyumbani. Mwanamume wa Kiafrika anastahili kujihusisha na kazi zinazozalisha mali ili kumwezesha kukimu na kukidhi matakwa ya familia yake. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza kwamba, si haki mwanamume kumlimbikizia mwanamke majukumu yote ya nyumbani ikiwamo kukimu na kukidhi mahitaji yao yeye akizembea na kulishwa mbali na kulazimisha mkewe kumpe huduma nyingine kama mkewe kama anavyoelezea mfanyibiashara:

> "…….. Mwanamke huyu alikuwa mkosewa na mmewe akawa mkosa. Maana alimpiga kwa kuwa hakumpikia na hakuwa amenunua chakula. Hao ndio wanaume wazembe. Kazi yao ni gumzo na ulaghai mtaani. Wanashinda kutwa kucha wakicheza dhumna vichochoroni na kunywa kahawa tungu la deni. Wakirejea makwao wataka pilau, wataka dengu na wataka samaki. Wanataka wake zao wageuke wazinzi…." (uk. 49)

Ndoa ni asasi inayopatikana katika kila jamii za ulimwengu. Mbaabu (1985) anasema kwamba, ndoa halali ni ile iliyounganishwa kwa msingi wa kanuni za kidini au kitamaduni. Utamaduni wa Kiafrika unapendekeza ushirikishaji wa familia za pande mbili katika mjadala wa ndoa na sherehe kama za ulipwaji wa mahari. Ndoa inatambuliwa kwenda kinyume na utamaduni wa Kiafrika kwa kutofuata taratibu zozote kama ilivyo ndoa ya Sauda na Kinyua. Wao wanakutana mjini Mombasa baada ya Sauda kutoroka nyumbani kwa kutotaka kuozwa na kisha wanaanza kuishi kama mume na mke bila kushirikisha familia zao katika mjadala wa ndoa kama anavyoelezea Sauda:

> "..nilitoroka nyumbani na kuja huku. Sasa nilipokuwa nikifanya biashara ya kuuza nikapatana na Kinyua akawa msena wangu na tunaishi pamoja," Sauda akayakamilisha maelezo yake. (uk. 50)

### 2.2.2 Ndoa Katika *Paradiso*

Asasi ya ndoa hutambuliwa na jamii kama ile inayoleta mahusiano mapya katika jamii inayojengwa kwa kuhusisha familia katika harakati za ndoa kama ulipaji wa mahari na harusi. Ndoa huipa familia hadhi na kuiweka katika ramani ya kijamii, kisheria na kidini. Mwandishi amewasawiri baadhi ya wanandoa wanaoishi kwa uelewano, heshima na mapenzi kama mume na

mke bila kuoana kwa kufuata kanuni zozote za ndoa. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza kuwa ndoa ni mkataba wa wanandoa kutokana na mapenzi kati yao wala si ya kifamilia. Ndoa ya Mango na wakeze Waislamu inatambuliwa kwenda kinyume na mielekeo ya kijamii kwa kutoshirikisha familia zao na kuoana kwa mapenzi hata ingawa, wana imani tofauti kama wanavyosema:

> "Kama ni kafiri ni wangu si wako…. Zuhra alisema" (uk36)
> "Kwani Sakina huyo mnayemmbughudhi si mtu….Mango ni wangu.
> Huko kanisani yuko kwa roho yake kwa ajili ya siku zake za baadaye.
> Simwachi ng'o." (uk 38)

Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza mwanamke aliye na sifa kielelezo kwa mfano, uwezo kiuchumi, akili tambuzi na uwezo wa kujiamulia mambo. Mwanamume anadhaniwa kuwa ndiye antakayekidhi mahitaji ya familia yake kama anavyotarajiwa na jamii. Mwandishi anadhihirisha hali mbadala kwa kuwasawiri wanaume wanaopuuza majukumu waliyotwikwa na jamii kwa msingi wa utamaduni wa Kiafrika. Mzee Mango anatambuliwa kupuuza majukumu yake kama baba na mzazi kwa kutotosheleza hisia za wakeze wala kukimu mahitaji ya familia yake kubwa. Mwandishi anawasawiri wakeze Mango kama wanawake wanaojitahidi kudumisha ndoa zao kwa kuvumilia na kujibidiisha ili famila zao zisikose mahitaji yao ya kimsingi kama anavyosema mwandishi:

> Wake wengine wa Mango waliishi Bunyala wakitegemea uvuvi katika ziwa Viktoria. Walinunua na kuuza samaki.... Kutokana na mauzo yao walilipa karo shuleni na kutimiza mahitaji mengine ya familia.… Kama ni Mango kuja nyumbani ataletwa na mkasa kama wa matanga au kwa nadra likizo ya Krismasi au labda masuala ya mashamba ambayo yeye mume ilikuwa lazima kuwapo. (uk. 1)

Ndoa za Kiafrika hujengwa kwa msingi wa watoto. Lawama humwendea mwanamke mtoto anapokosekana na mwanamume hupaswa kuoa mke mwingine ili amzalie watoto. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza ndoa iliyojengwa kwa msingi wa mapenzi na uelewa kwamba watoto ni baraka kutoka kwa Mungu. Mwandishi anaangazia ndoa ambazo zimejengwa kwa msingi wa uelewano na mapenzi ya dhati bali si watoto kama vile ndoa ya Kyalo na Salome. Kyalo anatambuliwa kama nguzo ya familia yake kwa mapenzi, uaminifu na imani kinyume na bali si kwa watoto kinyume na matarajio ya jamii kuwa anastahili kuoa mkewe akishindwa kupata watoto au hata kumtaliki. Mwandishi anamsawiri Salome kama mwanamke anayetatizwa na hali yake ya utasa na kukosa imani kwa Mungu. Salome anatambuliwa kutenda kinyume na matarajio ya jamii

na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika unaopigania wanawake kuwa na sifa vielelezo kwa kushiriki mapenzi nje ya ndoa kwa nia ya kutaka kuhifadhi ndoa kama anavyosema mwandishi:

> Kila siku tangu kisa cha kufumaniwa yeye na kasisi alikuwa akimhimiza mume wake Kyalo aoe. Mumewe lakini alikaidi. Alimwambia kama haukuwa mpango wa Mungu amjaalie watoto kupitia kwake hakutaka kuoa tena. (uk. 70)

Asasi ya ndoa inapatikana katika kila jamii na inastahili kuhalalishwa kupitia taratibu za kidini, kisheria au kitamaduni. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza mwanamke kuwa mwaadili na heshima. Baadhi ya wanandoa wanatambuliwa kuchangia kuzorota kwa maadili kwa kukiuka kanuni za kufunga ndoa kama ilivyowekewa msingi na utamaduni, dini na sheria za nchi husika. Ndoa ya Joshua na Lona inatambuliwa kwenda kinyume na matarajio ya jamii kwa kutofuata taratibu zinazokubalika. Ndoa hii inatambuliwa kuchangia kuzorota kwa maadili kwa kuwa wanandoa hawa wanashiriki mapenzi nje ya ndoa na hatimaye kuoana bila kufuata mielekeo ya kijamii wala kutafuta uungwaji mkono na familia zao kwa kile wanachokiita uhuru wa kupenda na kupendwa kama inavyojitokeza katika mawasiliano kati yake na mamake:

> “ Mwanangu sikai. Nimekuja kukujulia hali. Kubwa zaidi lililonileta ni kujua imekuwaje umetoka katika ndoa..”
> “ Hiyo ndoa mama sitaki,” Lona alimkata mama mtu kauli.
> “ Sasa huyu kijana mdogo uliyemganda ndiye atakayekufanya nini? Mama alimwuliza Lona
> “Huyu ndiye mwanamume wa kisawasawa.”
> “ Si ndugu yako katika Kristo?” Mama aliuliza tena.
> “Hata ndugu katika Kristo angeweza kuwa mume. Kuna ubaya?” Lona alisema kwa kurambua…. (uk.35)

Ndoa ya kudumu inahitaji wanandoa kuomba msamaha na kusameheana kosa linapotokea. Jambo hili hurahisishwa kukiwa na mapenzi na heshima inayochangia mawasiliano bora. Kunapokuwa na mapenzi na heshima ni nadra uzinzi kutokea na ukitokea, huwa rahisi kuomba msamaha na kusamehe. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza kuwa ni jukumu la kila mwanandoa kudumisha maadili kwa uaminifu na uwazi katika harakati za kudumisha ndoa yake. Salome na mumewe Kyalo wanajibiidiisha kuhifadhi ndoa yao japo Salome anatenda kinyume na matarajio ya kijamii kwa kushiriki mapenzi nje ya ndoa kwa lengo la kutafuta mtoto, mumewe anatambuliwa

kuhifadhi ndoa yao kwa kumsamehe baada ya kumfumania kama inavyojitokeza katika mawasiliano kati yao:

> "Utanisamehe Kyalo?" Salome aliuliza."
> "Sitakusamehe." Kyalo alisema….
> "Kwa sababu nilikusamehe usiku ule"
> "Asante," Salome alisema akifuta machozi ambayo yalimpa kiwi na kuizuia kumwangalia mume wake vizuri.
> " Niliingizwa mtegoni…….yote kwa ajili ya mtoto" (uk 59)

Kutokana na fikra kuwa mtu haishi pekee yake, jamii inatambua ndoa kama asisi inayojenga uhusiano mpya na kupanua familia. Uhusiano huu hujengwa kuanzia wakati wa harusi na katika ndoa kwa kushirikisha familia katika mipango yote. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza kuwa mwanamke anastahili kuingia katika ndoa inayotambuliwa na jamii kwa kufuata mielekeo inayokubalika na jamii. Baadhi ya ndoa zinatambua kufuata mielekeo inayokubalika na jamii na kushirikisha familia zao katika shughuli za ndoa kama anavyoelezea msimulizi kuhusu ndoa ya Michael:

> Hatua ya pili kwa insi kutekeleza, yaani kuoa, ilifikia Michael. Harusi ya Michael ilikuwa Valley Road Pentecostal Church……..Mango na Zuhra pamoja na Sakina wote walikuja kushuhudia harusi ya Michael.….Baada ya muda mfupi…... Nikaha ilikuwa tayari. (uk. 116)

## 2.3 Dini

Baadhi ya mataifa ulimwenguni kama Kenya, yana mfumo unaoruhusu uwepo wa dini zaidi ya moja. Dini za Kiislamu na Kikristo ndizo zimeenea zaidi miongoni mwa jamii za Kiafrika na ndizo tunazoshughulikia katika utafiti huu. Dini ni asasi inayotarajiwa kuwapa watu mwelekeo mwema unaojengwa kwa imani na Mungu kama tegemeo kwa kila jambo. Kupitia sala na imani binadamu anapata mahitaji yake yote. Kutokana na mapenzi ya dhati kwa Mwenyezi Mungu, binadamu ana uwezo wa kubariki wenzake na kuwa kielelezo kwa watu wengine.

Kwa mujibu wa dini hizi, dhambi ni kitendo kinachofanywa kinyume na sheria za Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammad anasema kwamba, dhambi ni kitendo ambacho hakuna mwanadamu anayependa kusikia wala kufanya hapa duniani. Hata ingawa binadamu huzaliwa bila dhambi na hupewa mwelekeo wa kujiepusha na dhambi, wao huishia kutenda dhambi lakini hurudia kuwa

sawa kwa njia ya toba kwa Mwenyezi Mungu kisha hupewa nafasi ya pili maishani kwa kuwa Mungu ni msamehevu.

Hawa na Adamu ni mwili mmoja kwa kuwa Hawa ameumbwa kutoka ubavuni mwa Adamu. Jambo hili ndilo msingi wa mapenzi kati ya wanandoa. Mungu anawapa Adamu na Hawa adhabu kwa kula tunda walilokanywa wasile. Hukumu ya Adamu ni kukimu na kukidhi mahitaji ya jamaa yake kwa kufanya kazi ngumu. Hukumu ya Hawa ni kuwa na uchungu anapojifungua (Mwanzo 3:7 na 16). Mtume Paulo katika Biblia kitabu cha Waefeso 5: 22-24, anasema kuwa wanawake wawatii waume zao na wanaume wawapende wake zao. Dini inatambua mwanamke mwerevu kama yule aliye na uwezo wa kutunza familia yake.

Ujio wa dini za Kikristo na Kiislamu katika bara la Afrika umechangia mabadiliko katika majukumu ya jinsia kinyume na ilivyowekewa msingi na utamaduni wa Kiafrika. Baadhi ya madhehebu yanawatambua wanawake kwa kuwapa nyadhifa mbalimbali uongozini kwa mfano, makanisa ya Kianglikana, Kilutherani na *Assemblies of God.* Hata hivyo, kuna mengine ambayo hayawatambui wanawake kama viongozi bora kwa mfano, kanisa la Kikatoliki haliruhusu mwanamke kuwa kasisi na dini ya Kiislamu hairuhusu mwanamke kushikilia wadhifa wa juu wa ushehe.

### 2.3.1 Dini Katika *Maumbile Si Huja*

Dini inamtweza mwanamke kwa kumpa nafasi chini ya mwanamume na kumtukuza mwanamume kwa kumtambua kama kichwa cha familia. Dini inatambua mwanamume anayependa mkewe kama nafsi yake na mwanamke mnyenyekevu na mwenye heshima kwa mumewe. Kwa mujibu wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mwanamke anayependwa na mumewe hunyenyekea na humheshimu mumewe kinyume na mwanamke asiyependwa. Hata hivyo, kuna baadhi ya wanandoa wanaoficha matendo yao maovu kwa kufunga pingu za maisha kwa msingi wa kidini. Juma ni baadhi ya wanaume wanaotambuliwa kufunga ndoa kwa kufuata mwelekeo wa kidini lakini hawana mapenzi kwa wake zao ila mali waliyo nayo jambo ambalo linachangia wake zao kuishi maisha ya upweke kama inavyojitokeza katika mawasiliano kati ya Juma na mkewe Amina:

> "Njoo hapa wewe. Mbona wajikunyata kama yatima? Umekosa nini? Mali?" Juma alisalia huku kabadili raha yake ya muda na kuwa kama ndume aliyehasiwa.
> "Mimi na yatima naona tu sawa….. (uk. 3)

Dini inatarajia waumini wenye imani kwa Mwenyezi Mungu. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika pia inatarajia mwanamke awe na sifa kielelezo kama usalihina na awe mwenye imani. Amina, mwanamke Mwislamu anatambuliwa kutenda kinyume na haya kwa kutafuta usaidizi wa mganga wa kienyeji ili aweze kupata mtoto wa kike. Mwanaume pia anatambulishwa kama mshirikina na ndiye mganga anayetajika kama anavyosema Amina:

> "……Usiseme haya tu bali tutafute mganga mweledi ambaye anasifika katika shughuli za bao. Mfano wa yule mzuzaji Pemba aitwaye Khalid bin Maji Mazuri; ni mtu mashuhuri katika madawa." (uk.100)

Dini ina jukumu la kupatia jamii mwelekeo mwema. Kutokana na kitabu Kitakatifu cha Biblia, mwanamke anastahili kunyenyekea na kumtii mume wake na kwa kuwa Mungu aliumba mwanamke ili kumsaidia mwanamume katika shughuli zake duniani, mwanamke anapewa nafasi ya pili chini ya mwanamume. Jambo hili linapingwa na wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika wanaopigania usawa kwani hakuna jinsia bara kuliko myingine. Wanaume wanatambulishwa kufanikisha kauli hii kwa kuchangia katika harakati za kupigania usawa wa jinsia kama anavyosema Kinyua:

> "Mimi sijui dini nyingine isemavyo lakini kulingana na dini ya Kikristo, wote, wanaume kwa wanawake wanapaswa kuwa sawa katika Agano Jipya. (uk 82)

### 2.3.2 Dini Katika *Paradiso*

Dini huwapa waumini utambulisho wa uaminifu kwa Mungu na katika ndoa. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza kuwa mwanamke anastahili kuwa na sifa kielelezo kwa maneno na matendo. Kwa kuwa ndoa inastahili kudumu milele, ni muhimu kwa wachumba kudadisi kama kweli wanapendana kabla ya kufunga pingu za maisha kwa sababu talaka nyingi hutokana na upungufu wa mapenzi, kutoweza kuvumiliana na uasherati. Mwandishi anawasawiri viongozi wa dini kama wanafiki kwa kutenda kinyume na mafunzo yao ya dini. Kasisi Musa na Salome, viongozi katika kanisa la *New Jerusalem* wanatambuliwa kama wanafiki kwa kushiriki

mapenzi nje ya ndoa ilhali wao ndio wanaostahili kuwaongoza wakristo wengine katika njia za Bwana kama anavyofikiria Kyalo:

> Kyalo alimwona Musa kama afiriti. Alimwona kama kasisi laghai aliyepoteza kondoo alopewa kuwatunza na kuwaangalia….Kyalo alishangaa kama huwezi kumwamini mhubiri utamwamini nani? Kama kanisa sio mahali pa usalama watu watakimbilia wapi? (uk 59)

Vile vile, mhubiri Michael anatambulishwa kama mnafiki kwa kutofuata mafunzo ya dini. Michael anashiriki mapenzi nje ya ndoa na Patricia, rafikiye Lydia. Michael anajutia makosa yake na kuomba msamaha kwa Mungu na baada ya kupata suluhu na mkewe, anamwacha Patricia na mwanawe bila kutimiza ahadi alizompa. Michael anatambuliwa kama mtu ambaye hana msimamo kwa kujiingiza katika ndoa bila kufanya uamuzi mwafaka kwani hajui anampenda nani kati ya Patricia na mkewe. Michael hajui afuate maagizo ya Biblia au hisia za kimwili kama anavyosema mwandishi:

> Michael alikuwa amempa ahadi za urongo. Michael alikuwa ashamwambia angemwoa awe wake wa uvumba na udi.... Michael hakuelewa afanyeje. Kama angemkubali basi angekuwa akirudi katika uzinzi na usherati. Lau angemkataa ingekuwa ni kuvunja ahadi na kumkosea Patricia siyo tu kama rafiki na mwanamke bali pia kama kiumbe cha Mungu. (uk.177)

Kasisi Joshua anatambulishwa kama mnafiki kwa kutumia jina la Mungu kwa manufaa yake binafsi. Kwa muda wote Joshua, ndugu katika Kristo alipewa makao katika nyumba ya Lona na mumewe Mganga baada ya kufika mjini bila kazi wala kisomo, alikuwa na uhusianao wa kimapenzi na mke mwenye nyumba, Lona kama anavyosema mwandishi:

> Baadaye, Lona na Mganga walianza kudhaniana. Kila mmoja akawa hamwamini mwenzake….Kumbe kwa miaka hii yote kumi Lona alokaa na Joshua, Joshua alikuwa mume mwenza wa Mganga. Mganga hakujua lolote. (uk. 34)

Dini inawapa waumini utambulisho wa imani thabiti kwa Mungu. Mungu anatarajia binadamu amtegemea kwa kila jambo na katika hali yoyote. Binadamu amepuuza haya na kuweka imani yake kwa mali, wanawe, jamaa zake na kwa waganga wa kienyeji. Sakina mwanamke Mwislamu

anatambuliwa kutokuwa na imani kuwa Mungu ana uwezo wa kuponya Michael mwanawe mzee Mango baada ya daktari kushindwa kumtibu kama anavyosema mwandishi:

> Sakina aliwaza jambo la kufanya asipate jawabu. Aliona ni kweli kama daktari ameshindwa basi na njia ya pekee ilikuwa kumpeleka huyo mtoto kwa mganga akaangaliwe. (uk 13)

Mwandishi anawasawiri viongozi wa dini kuwa watu wasiosema ukewli mbali na kuwa washirikina. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza kuwa mwanamke anastahili kuwa kielelezo katika jamii. Wanawake wanatambuliwa kuwa wanafiki kwa kutenda kinyume na mafunzo ya kidini. Lona, mkewe kasisi Joshua, anatambuliwa kuwa mshirikina kwa kutafuta msaada kutoka kwa mganga wa kienyeji ili kumdhibiti mumewe kwa mapenzi ya uongo kama anavyosema mwandish:

> Angelina alichukua manywele akayafungia katika karatasi ya plastiki laini kisha akachukua nguo ya Askofu Joshua akaifungia ndani ya chupa na akampa Lona. (uk 109)

Matakwa ya Mwenyezi Mungu kupitia mafunzo ya dini ni kuwajenga watu kiroho. Baadhi ya viongozi wa madhehebu mbalimbali wanatilia maanani injili ya pesa pasi na kushughulikia nyoyo za waumini. Mahubiri katika baadhi ya madhehebu yanahusu upandaji wa mbegu, miujiza na utajiri. Sababu za waja kwenda kanisani ni kupata mali na suluhu kwa matatizo yao kinyume na matakwa ya Mwenyezi Mungu ya kuabudiwa na kutukuzwa katika hali zote. Binadamu wanatambuliwa kukimbilia kunako miujiza na wanakopata suluhisho ya matatizo ya kiuchumi, magonjwa miongoni mwa matatizo mengine kama anavyosema mtangazaji katika kanisa la New Jerusalem:

> Tangazo jingine ndugu zangu na dada zangu katika Yesu ni kwamba matoleo yenu yamepungua…. Kitabu cha Malaki kinasema matoleo ni lazima kwa muumini….Kumbuka zaka ni mbegu na fungu la kumi ni amri kutoka kwa Mungu. Kila mtu apandacho ndicho avunacho…. Kumbuka mtakapotoa Bwana atawarudishia zaidi. Mtajenga nyumba, mtanunuia magari na kuwa na pesa tele kuliko watu wa dunia. (uk. 54)

Mbali na kuchangia ufisadi, viongozi wa dini wanajitajirisha kwa kujihusisha na ulanguzi wa mihadarati. Baadhi ya viongozi wa kidini wanatambulishwa kama wanafiki kwa kutumia jina la Mungu kwa manufaa yao binafsi. Kasisi Joshua, Lona na Boribori ni badhi ya viongozi wa kanisa

wanatambuliwa kama walanguzi wa dawa za kulevya kanisani mbali na kutambuliwa kama watu wanaotoa rushwa kinyume na matarajio ya jamii kama anavyoelezea mwandishi:

> Katika mambo aliyoungama Boribori ni kuwa ulanguzi huu ulianza na Joshua. Mkewe Joshua, marehemu Lona, ndiye aliyekuwa mharakati wa shughuli hii. Sasa yeye Boribori alipoungana ikabidi ahusike kama sababu ya kukaa hapo... (uk. 208)
>
> Boribori alidondoka shilingi milioni moja. Aliitoa kama chai kwa jaji Moriasi. (uk. 212)

Jamii inatambua dini kama asasi inayochangia umoja na upendo. Hata hivyo, kutokana na tamaa ya uongozi na matoleo katika madhehebu mbalimbali, dini imekosa umoja na upendo na badala yake wivu na ugomvi ndio umekithiri miongoni mwa viongozi na washirika. Mwandishi anawasawiri wahusika wake hasa wa kiume kuwa ndio wanaoendeleza sifa hii mbaya.Tonje na Mango wanatambuliwa kama viongozi wa kidini wanaoeneza chuki, wivu na tamaa ya matoleo kanisani jambo linalochangia ugomvi na utengano kama yanavyojitokeza katika mawasiliano kati ya Zuhra na Michael:

> Yeye na babako hawaonani uso kwa uso. Kila mmoja yuko na mambo yake." Zuhra alieleza.
> Wanagombania nini?" Michael aliuliza.
> Wanagombanea washirika na zaka. (uk. 45)

Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wamefanikiwa kuboresha uhusiano wa wanawake kinyume na fikra kuwa wanawake hawawezi kushirikiana kutokana na wivu uliokithiri miongoni mwao. Kinyume na ilivyodhaniwa, wanaume wanatambuliwa kueneza chuki na wivu. Wanaume ambao ni viongozi wa kidini ndio wanaoendeleza kadhia hii. Kasisi Joshua anatambuliwa kumwonea wivu Michael kutokana na uwezo wake wa kutenda miujiza kwa jina la Mwenyezi Mungu. Tabia hii inaathiri uhusiano wao kama anavyosema msimulizi:

> Aliposimama umati wa watu ulivuma ndani ya kanisa na hemani. Michael alikuwa na mvuto mkubwa kwa waumini wa kanisa hili. Jambo hili wakati mwingine lilimletea Joshua wivu mpaka akavimba shingo kama pili anayemeza mbuzi. (uk. 55)
>
> Michael alipozidi kuvuma katika midomo ya watu alikuwa akitia kitumbua chake mchanga na viongozi wengine. Kila aliposikia miujiza iliyomkuza, Askofu Joshua aliudhiwa, moyo ukamwelea…. (uk. 67)

Dini inamtambua binadamu anayefuata amri za Mwenyezi Mungu kwa kuzingatia mafunzo ya Biblia. Matendo yaliyo kinyume na amri hizi ni dhambi na hukumu ipo siku ya kiama. Binadamu wanaotenda haki na kufuata sheria za Mungu, dini inawapa ahadi ya maisha baada ya kifo katika paradiso. Waumini wengi wamegubikwa na hofu kuhusu maisha baada ya kifo kwa kukosa uhakika wa kuingia paradiso kama alivyoahidi Mwenyezi Mungu. Ufeministi wa Kiafrika unatambua mwanamke kama jinsia jasiri asiyeogopa chochote. Apondi anatambuliwa kama mwanamke jasiri asiyeogopa kifo kutokana na imani kuwa kuna maisha baada ya kufa. Apondi anatambuliwa kama mwanawake anayemtegemea Mungu bali si mumewe. Kama baba alivyo kwa mwanawe ndivyo Mungu kwa waja kama anavyosema Apondi:

> "Kwangu mimi, kuishi ni Yesu na kufa ni Baraka zaidi. Maana nikifa nitakwenda kumwona Baba na nikiishi nitaendelea kumtumikia." Hakutishwa na harufu ya mauti. (uk.90)

Kinyume na matarajio ya kijamii mwandishi anamsawiri Michael kama mkristo asiye na uhakika kuhusu maisha baada ya kifo. Kinyume na inavyodhaniwa kuwa wanaume ni watu jasiri wasio ogopa lolote, Michael anatambulishwa kushtuliwa na kifo cha mamake kwa kuhofia maisha baada ya kifo. Imani yake inayumbishwa kwa kukosa matumaini ya kuonana na mamake katika maisha ya baadaye kama anavyoelezea mwandishi:

> Simu ya kifo ya mamake Michael ilimshtua si haba. …Kwa jinsi Michael alikuwa amesimama katika mwamba wa uinjilisti ungeona asingeweza kutishwa lakini aliyumbishwa kama tiara hewani. (uk.90)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza kuwa wanawake wawe vielelezo katika jamii. Jamii inatarajia wazazi hasa mama kuchangia katika kukuza maadili kwa kuwa mfano mwema kimavazi, mazungumzo, mapenzi na ndoa. Mwandishi anawasawiri wanawake kama watu wasio na maadili kinyume na matarajio ya wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika na jamii kwa jumla. Lona anatambuliwa kama mwanamke asiye na maadili kutokana na mavazi yake yasiyo ya heshima na ambayo hayaambatani na umri wake kama anavyosema mwandishi.

> Michael alisema akitazama skati ndefu ya huyu mama iliyopasuliwa kuwili hadi mapajani, kiasi cha kwamba imletee hizaya. Michael alishangaa ni kwa nini mama huyu alivaa hivyo katika umri wake wa miaka sitini. Isitoshe, atavaaje hivyo akija kumwona? (uk.69)

## 2.4 Utamaduni

Mbaabu (1985) anasema kwamba utamaduni unahusu asili na jadi za jamii, mila na desturi zao kimavazi, vyakula, tabia na imani. Hii ina maana kwamba utamaduni ni mtindo wa maisha ya watu wanavyoishi, wanavyokula na wanavyovaa. Kila jamii barani Afrika ina utamaduni wake unaoitambulisha na kuitofautisha na jamii nyingine na kuipa mwelekeo. Kupitia tamaduni hizi jamii inapata mwelekeo thabiti unaostahili kuzingatiwa ili kuzuia mikwaruzano. Utamaduni wa Kiafrika unaonekana kumkweza mwanamume na kumtweza mwanamke. Utamaduni wa Kiafrika unampa mwanamume uhuru wa kujiamulia idadi ya wanawake wa kuoa na kumnyima mwanamke uhuru wa kujiamulia kupenda, kuwa mke au kupata watoto. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inanuia kuleta uhuru wa kijinsia kwa kupigania usawa wao.

### 2.4.1 Utamaduni Katika *Maumbile Si Huja*

Katika jamii nyingi za Kiafrika mahari hupelekwa kama ishara ya shukurani kwa familia ya msichana anayechumbiwa kwa malezi aliyopata. Lakini mahari sasa inachukuliwa kuwa malipo kwa ajili ya kuoa. Mara nyingi hudhaniwa kuwa mbadala wa msichana anayeolewa. Mwanamke aliyelipiwa mahari huchukuliwa kama mali ya mumewe na hana haki ya kumiliki kitu chochote. Baada ya mahari kulipwa, mwanamke anastahili kuvumilia mambo yote na talaka si jawabu. Mwandishi anawasawiri wazazi kama ndio wanaochangia dhuluma dhidi ya wana wao wa kike kutokana na hali yao ya umaskini kwa kuweka kiwango cha mahari wanayohitaji. Wanaume wa Kiafrika wanatambuliwa kutenda kinyuma na matarajio ya jamii kwa kupinga dhana ya ulipwaji mahari kama anavyosema Omar:

> "Siku za kufanya hivyo zimekwenda ndugu…..Hii ilikuwa ni kwa
> sababu baba zao walipenda mali mengi na walikuwa kama waliouzwa.
> Zamani hizo wasichana walikuwa ni vyombo badala ya kuwa
> wenza."(uk.80)

Watoto huthaminiwa kwa sababu ya kuendeleza kizazi cha jamii husika. Baadhi ya jamii za Kiafrika zinatilia maanani uwezo wa mwanamke wa kupata watoto na kupuuza uwezo wa mwanamume akidhaniwa kuwa binadamu asiye na kasoro. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanapinga mila na desturi za Kiafrika zinazomdhalilisha mwanamke kwa kutumia kigezo cha uzazi. Mwandishi anasawiri wanaume wanaopinga kauli hii kwa kutambua udhaifu wa jinsia ya kiume katika mambo ya uzazi. Kutokana na nia ya jamii za Kiafrika kutaka kuendeleza familia

zao na kudumisha hadhi ya mwanamume, mwanamke anatambuliwa kunyanyaswa kwa msingi wa utamaduni wa Kiafrika unaomshinika kutafuta mtoto nje ya ndoa ili kusitiri udhaifu wa mumewe kama anavyosema Kinyua:

> "Katika jamii yenye kudunisha mwanamke, ni vigumu sana kwake yeye kusema wazi kuwa mme aliye naye si mme. Yeye huishi tu hata mmewe kwa ajili ya kutojitambua akamfukuzia mbali kwa kuwa tasa. Mke wa pili anapoolewa, jamii humfunza kunga za kutumia ili kupata vijukuu. Mara mwanamme huanza kujidai na kusema eti mke wa kwanza aliyemwoa ni mbaya kumbe ni mwongo. Ajabu ni kwamba mke- tasa hujifungua na akapakata vijukuu naye,' (uk.79)

Utamaduni wa Kiafrika unaipendelea jinsia ya kiume na kuidhalilisha jinsia ya kike kwa kuifikiria kuwa kiumbe kisichoweza kutenda chochote kizuri. Kuanzia utotoni, mila na desturi za Kiafrika kupitia malezi zinamdhalilisha mtoto wa kike na kumtukuza mtoto wa kiume kuwa bora. Mtoto aliye na upungufu wowote hulinganishwa na mamake bali aliye na uwezo hulinganishwa na babake. Mwandishi anasawiri wanaume kama wakereketwa wa kupigania usawa wa jinsia kwa kupendekeza mapadiliko katika malezi ya watoto. Kinyua anatambuliwa kupigania usawa wa kijinsia kwa kupendekeza kubadilishwa kwa mazingira ya malezi kama anavyoelezea:

> "Nafikiria ndugu yangu kile ambacho kinafaa kubadilishwa ni malezi ili yazingatie watoto wote wawili, msichana na mvulana. Watoto wa kike wameonewa kwa karne na karne… Mara ukasikia akipigwa na lundo la matusi 'mjinga kama mamako na kadhalika'. Nafikiria hii ni kwa sababu ya utamaduni. (uk.81)

Utamaduni wa Kiafrika unapendekeza urithi kama njia ya kupitisha mali kutoka mtu kwa mmoja hadi mwengine. Radcliffe - Brown (1955) anasema kuwa urithi huweza kufanywa mtu akiwa hai au baada ya kuaga dunia. Wanaohusishwa katika mikakati hii wanaweza wakawa watu wa familia au jamaa zao. Baadhi ya vitu vinavyorithiwa ni uongozi, mali na mwanamke kutokana na fikra kuwa yeye ni mali ya mumewe kwa sababu ya mahari aliyolipiwa. Jambo ambalo linapingwa na wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kwa kuwa mwanamke ni binadamu si chombo. Mbali na wanawake kuathiriwa na tendo hili la urithi, baadhi ya wanaume wanatambuliwa kuathirika na tendo hili la urithi kinyume na matarajio ya jamii kama anavyosema mzee Mgeni:

> "…..Baba alihama kwa sababu Mombasa haikuwa janibu tena. Ajabu ni kwamba hakunichukua ili kwenda naye. Nikabaki na mamangu…..Nyumba yetu ilianza kunyongwa na kusongwa na mikono ya ufukara. Ama kwa kweli babangu hakutaka kunirithisha kama mwanawe." (uk. 10)

### 2.4.2 Utamaduni Katika *Paradiso*

Baadhi ya vipengele vya utamaduni ni pamoja na mila na desturi za kijamii. Kila jamii ina mila na desturi zake zinazoitambulisha na jamii nyingine. Jamii ya Wanyala inatambuliwa kutokana na kufuata mila na desturi za utamaduni wa Kiafrika kwa kuoa wake wengi. Jamii za Kiafrika zinatambua mwanamume aliyeoa wake wengi kama kiongozi bora kwa kuiongoza familia yake kubwa. Jambo hili linawapa baadhi ya wanaume wa Kiafrika ari ya kuoa wake zaidi ya mmoja kama anavyosema mwandishi:

> Mango alisikiliza sana desturi za kwao. Kule mwanamume mwenye mke mmoja ni kama mtu mwenye chongo. Hakutambulika katika shughuli za pale kwao Budalangi. Hasa wanaume kwa jina hilo na maana wasemapo haikuwa ruhusa kwake kusema. (uk.8)

Mila na desturi za jamii za Kiafrika zinamdhalilisha mwanamke kwa kumfikiria kuwa kiumbe aliye na akili dhaifu na asiyeweza kushauri mtu, mtu hapa akiwa ni mwanamume. Mwandishi amefanikisha wazo la wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kuwa wanawake wana akili tambuzi kama walivyo wanaume na kama binadamu yeyote ana uhuru wa kutoa au kutafuta ushauri panapohitajika kwa kuwasawiri waja kama watu wanaoshauriana panapotokea tatizo. Mango anatambuliwa kutafuta ushauri kutoka kwa mkewe, Apondi mwanawe Michael anapotatizwa na ugonjwa kama anavyosema mwandishi:

> Alikuwa mithili ya mja aliyetapia uhai wake katika bahari iliyochafuka. Alijisikia anataka kulia kwa kushindwa kujua jambo la kufanya….Ni katika mseto huu wa mawazo alipomkumbuka mamake Michael. Alihuhitaji sana ushauri wa Apondi. (uk. 7)

Mavazi ni zao la jamii kama ilivyo jamii ya Waislamu ambayo inasisitiza aina ya vazi la buibui kwa wanawake na kanzu kwa wanaume. Mbali na mavazi haya kutozingatia hali ya anga, ni vigumu kutambua msichana au mwanamke kutoka kwa mwengine. Jamii za Kiafrika kwa msingi wa tamaduni zao zinamnyima mwanamke uhuru wa kuvaa. Jamii ya Waislamu inamwona msichana na mwanamke asiyejifunika kwa buibui kuwa mpotovu kwani huaminiwa kuacha sehemu zake za mwili nje ili zionekane na wavulana ilhali mvulana ana uhuru wa kuvaa atakavyo bila kuhukumiwa. Ufeministi wa Kiafrika unapinga dhana hii kwani, wanawake wanastahili

kupewa huru wa kuvaa bora yawe ni mavazi ya heshima si kulazimishwa kujifunika buibui hadi nyuso zao na kuacha macho tu ya kuona kama anavyosema Apondi:

> "….Wanawake wengine walijifunika ninja kabisa nyuso zisionekane ila macho tu ya kuona njia na watu. Ama kila watu na desturi zao. Sasa utajuaje mwanao ukikutana naye barabarani?" (uk. 12)

Jamii nyingi za Kiafrika huwatambua wafu kama wenye uwezo wa kubariki au kulaani kutokana na uhusiano wao na waliohai. Jambo hili huzifanya jamii nyingi kuthamini maiti kiasi cha kufanya matambiko kwa ajili ya kutuliza hasira zake ikiwa alifariki katika hali zisizo nzuri kwa mfano, kufa katika hali ya upweke au kufa nyumbani bila kupelekwa hosptalini baada ya kuugua kwa muda mrefu. Tofauti na fikra kuwa wanawake ndio wanaoathiriwa zaidi na tamaduni hizi za Kiafrika, wanaume pia wanaathirika. Mango anatambuliwa kuathiriwa na tamaduni za Kiafrika kwa kulazimishwa na jamaa yake kulala na mfu faraghani mbali na kulazimishwa kunywa busaa na kula nyama wakati wa matanga lhali yeye ni mhubiri kama anavyoelezea mwandishi:

> Mango alihitajika baadaye afungiwe na marehemu mkewe katika chumba mbali na mtu mwingine yeyote.…Alifungiwa na marehemu mkewe kwa chumba kwa saa moja nzima..Baadye....wazee wakamweleze kuwa walifahamu ni mtu wa Mungu na kwa hivyo hangekunywa tembo…Lakini walimwambia afungue kwa kuonja kidogo… (uk.93)

Baadhi ya tamaduni za Kiafrika kupitia mila na desturi zake, zinanuia kuelekeza jamii katika kudumisha heshima na kukuza maadili mema. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza jamii iheshimu jinsia ya kike. Baadhi ya jamii za Kiafrika zinatambuliwa kuwapa heshima wanawake kwa mfano, jamii ya Wanyala anatambuliwa kuonyesha heshima kwa mama mkwe. Heshima hii inadhihirishwa na mkaza mwanawe kwa kutoshirikiana naye wala kukaa mahali moja kwa muda mrefu. Michael anatambuliwa kama mwanaume anayechangia ukuzaji wa maadili na heshima katika jamii kwa kufuata mila na desturi za kwao za kutoshirikiana na mama mkwe kwa muda mrefu kama anavyoelezea mwandishi:

> Michael baadaye aliondoka kwa mujibu wa mila za kwao Budalangi. Ni haramu kukaa na mavyaa yako kwa muda mrefu. Kisa na maana unaweza kumkosea mama mkwe heshima na ukifanaya hivi utakosa radhi zake. (Uk. 174)

## 2.5 Elimu

Kulingana na Wollstonecraft (1972) elimu ni kitu cha thamani na ndio msingi wa mambo yote mazuri maishani mwa binadamu. Kukosa elimu ni kama kukosa mwelekeo maishani. Baadhi ya jamii za Kiafrika humnyima mtoto msichana haki ya kupata elimu kutokana na fikra kuwa hana uwezo kimasomo na kama ana uwezo, yeye huolewa katika familia nyingine ambayo hufaidika kutokana na masomo yake. Kwa hivyo, jamii huonelea ni heri msichana aolewe ili familia yake ifaidike kupitia mahari.

### 2.5.1 Elimu Katika *Maumbile Si Huja*

Baadhi ya jamii za Kiafrika zinazingatia masomo ya mtoto wa kiume na kupuuza masomo ya mtoto wa kike. Msichana hutunzwa vizuri ili kuiletea familia yake mali kupitia mahari, jambo ambalo linapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaopigani usawa wa jinsia katika masomo. Mtoto wa kike anatambuliwa kunyumwa haki yake ya kupata elimu wala kupewa uhuru wa kujichagulia mchumba. Sauda anatambulishwa kama msichana anayedhalilishwa na utamaduni wa Kiafrika kwa kuozwa kwa kunyimwa nafasi ya kusoma mbali na kuozwa kwa lazima ili kakaye apate karo kama anavyoeleza:

> "Mimi nilikuwa nikisoma katika darasa la nne….Mwalimu mkuu alitufukuza shuleni ili tutafute karo. Mimi na ndugu yangu Hassan tulikwenda nyumbani kumshtakia baba yangu hali yetu. Tulipofika nyumbani baba yangu akanieleza eti alitaka kunioza kwa Mzee Ramadhan. Mimi nilikatalia mbali pendekezo hilo lisilo mantiki. Hii ndiyo sababu nilitoroka nyumbani..."(uk. 50)

Utamaduni wa Kiafrika unashikilia kuwa kazi za mwanamke zinatofautiana na zile za mwanamume kutokana na viwango vyao vya elimu. Haya ni kwa mujibu wa Buchert (1994) anayesema kwamba, mwanamke anafundishwa kuwa mlezi bora wa familia na watoto ilhali mwanamume anafundishwa kuwa kiongozi bora kwa hali na mali. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inasisitiza kuwa ili kuwepo na maendeleo katika jamii, mwanamke anastahili kuelimishwa kwa kuwa yeye pia ni mhusika katika shughuli za kujenga jamii. Mwandishi amewasawiri baadhi ya wahusika wake wa kike kuwa na uwezo kielimu kwa kubobea katika sekta hiyo kinyume na fikra kuwa wanawake hawana uwezo kimasomo kama anavyoeleza Suleiman:

> "…….Nilisikia kuwa mke mmoja alikosana na mmewe na wakateta mpaka kijiji kikajaa sauti zao. Bibi huyu alikuwa amemimina masomo kweli kweli. Bwana huyo naye alikuwa amebukua kama kadhi mzima…." (uk. 80)

Kimsingi elimu inatarajiwa kuwa daraja ya kupata ajira. Kwa kuwa nafasi ya mwanamke ni jikoni na kazi yake ni ya kinyumbani isiyohitaji elimu, jamii inapuuza elimu ya mtoto wa kike na kutilia manani elimu ya mtoto wa kiume kwa kudhaniwa kuhitaji ajira ili waweze kukimu familia zao. Iqbal anatambuliwa kama mwanamume anayepuuza ajira na kuanzisha biashara inayomsaidia kukidhi mahitaji yake kama anavyosema mwandishi:

> Kwanza nduguye alikwenda kusoma sheria nchini Misri. Aliporudi akafanya kazi ya uanasheria….Uanasheria aliutupilia mbali na kushughulika na duka lake la elektroniki. Duka hilo lilimpa kula, kuishi na kumpa kufungua miradi mingine ya kuzalisha mali. (uk 38)

### 2.5.2 Elimu Katika *Paradiso*

Taylor (1985) katika makala ya 'Women: A World Report' anaeleza jinsi mtoto msichana huwasaidia wazazi wake kiuchumi pamoja na mumewe baada ya kuolewa. Hata hivyo, Taylor anasema kuwa mchango wa mwanamke huwa hautambuliwi na jamii. Kutofaulu kwa watoto wa kike katika elimu kunachangiwa na ndoa za mapema pamoja na kunyimwa nafasi ya kusoma nyumbani kwa kufanyishwa kazi wakati wavulana hutengewa muda wa kusoma. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapendekeza jamii iliyo na usawa kwa kuzingatia elimu ya mtoto wa kike. Watoto wa kike wanatambuliwa kubobea katika elimu kwa kusoma hadi vyuo vikuu kinyume na fikra kuwa wasichana hawana uwezo kimasomo. Lydia anatambuliwa kama mwanamke aliyebobea katika masomo kwa kusoma hadi chuo kikuu na kuajiriwa kama mwalimu katika Shule ya Upili ya Alliance kama anavyosema mwandishi:

> Lydia alikuwa amemaliza masomo yake katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Lydia alikuwa mwalimu wa Alliance Girls….. (uk.83)

Jinsia ya kike inatambuliwa kubobea katika sekta ya elimu kama inavyochangiwa na Ufeministi wa Kiafrika. Patricia anatambuliwa kama mwanamke aliye na uwezo katika masomo kwa kufuzu na kufunza masomo Fizikia na Hisabati yanayoaminiwa kuwa ya wanaume kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> “Naam, Patricia ulisema unafundisha nini Alliance?” Michael aliweka ulalo.....
> “Nafundisha Fizikia na Hesabu.”
> “Ala! Mbona hivyo?” Michael aliuliza.
> “Yaani ninashangaa msichana aweza kufundisha masomo magumu kama hayo,” Michael alisema (uk.100)

## 2.6 Uchumi

Wanawake wa Kiafrika wanakumbana na changamoto nyingi kutokana na uwezo wao duni kiuchumi. Kohen (1993) anadai kuwa jamii inawanyanyasa wanawake kwa kuwapa kazi ngumu za kibaguzi shambani na nyumbani, zinazozalisha mapato madogo kama kupika, kuosha na kulea watoto ilhali wanaume wanajishughulisha na kazi zinazozalisha mapato makubwa. Jambo hili linawafanya wanawake kuwa wategemezi wa wanaume kwa kuwa mhitaji hana chaguo ila kukubali matakwa ya mfadhili wake. Udhaifu huu wa wanawake unawapa hadhi wanaume na kuchukuliwa kuwa wenye uwezo.

### 2.6.1 Uchumi Katika *Maumbile Si Huja*

Utamaduni wa Kiafrika umetengea waja wake majukumu kulingana na maumbile. Kazi zinazotengewa wanaume ni za nje zinazohitaji nguvu nyingi ilhali wanawake wametengewa kazi za nyumbani zisizohitaji nguvu nyingi. Wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza kuwa jinsia itengewe majukumu kulingana na uwezo na tajiriba yao. Mwandishi amefanikisha mawazo haya kwa kusawiri watu wasiobagua kazi kwa msingi wa maumbile. Jinsia zinatambulishwa kufanya kazi bila kujali maumblie wala hadhi bora mapato kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> “Haya Issa. Nimetaka uwe mfanyakazi wangu mpya. Umekuja badala ya Kinyua…..Nataka uwe na bidii kazini kama Said,” Juma alieleza kisha akaita, “Said?”(uk 17)…..“Hii ndiyo kazi yenyewe.”
> “Katafute ufagio tuendelee,” akahimizwa. Isaa akamtazama Said kwa muda fulani na akaondoka kwenda kutafuta ufagio. (uk.18)
>
> Lori la manispaa ya Nairobi lilikuwa limebeba wanawake watatu. Mmoja mrembo sana alikuwa akishughulika na usukani. Hawa wawili ambao walikuwa wamejifunga maleso viunoni walitoka na kolego za mchanga. Kando kidogo kulikuwa na jalala. Jalala hili lilikuwa na kimo cha ndovu….Wanawake hawa walipomaliza kushughulika na kuondoa hii takataka inzi walitawanyika na mara wakaona vitoto chokora pia vimeshughulika. (uk. 85)

Tamaduni nyingi za Kiafrika zinamtambua mwanamume aliye na uwezo wa kukimu na kukidhi mahitaji ya familia yake kutokana na uwezo wake kiuchumi. Wanaume Waafrika wanadhaniwa kuwa wamiliki wa nyenzo kuu za kuzalisha mali kutokana na ushawishi wao mkubwa wakilinganishwa na wanawake. Mwandishi anathibitisha haya kwa kuwasawiri baadhi ya wahusika wake wa kiume wanaofanya biashara kubwakubwa zinazozalisha mapato makubwa kwa mfano, mzee Juma kama anavyoelezea mwandishi:

> Juma alikuwa na pakacha la vyombo baharini. Alitumia vyombo hivi kwa shughuli za biashara. Merikebu zake zilileta marobota ya nguo na vitambaa vya thamani baada ya kila mwezi. (uk. 19)

Uhusika wa mwanamke katika harakati za kujenga jamii unadhihirishwa na mwandishi kwa kuwasawiri wanawake na wanaume kama watega uchumi. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanafanikiwa katika harakati za kumkomboa mwanamke kiuchumi. Mwanamke aliye na uwezo kiuchumi huwa na uhuru wa kujiamulia mambo kwa kuwa si mtegemezi wa mwanaumme bali ni mshiriki wake katika harakati za maendeleo ya jamii kama anavyoelezea mwandishi:

> Kinyua aliishi na Kibamba Sauda….Kinyua aling'ang'ana na vibarua na wenzake bandarini kwa kupakua na kupakia mizigo. Sauda aliuza mchicha. Maisha yakaendelea. (uk 44)

### 2.6.2 Uchumi Katika *Paradiso*

Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanakataa kauli kuwa wanawake hawana uwezo wa kutega uchumi kama wenzao wa kiume. Wanawake wanatambuliwa kuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya familia zao kutokana na uwezo wao wa kiuchumi kama anavyosema mwandishi:

> Wake wengine wa Mango waliishi Bunyala wakitegemea uvuvi katika ziwa Victoria. Walinunua na kuuza samaki kwa masurufu yao ya kila siku. Kutokana na mauzo ya samaki walilipa karo shuleni na kutimiza mahitaji mengine ya familia. (uk. 1)

Mwandishi anaonyesha mchango wa wanawake katika harakati za kutega uchumi na kukuza jamii. Ufeministi wa Kiafrika unapigania jamii iliyo na imani kwa mwanamke kama jinsia inayoweza kutegemewa kiuchumi. Nadharia hii inasisitiza kuwa wanawake wana uwezo wa kutunza na kuendeleza biashara zao zinazowapa mahitaji ya kila siku ili waweze kujitegemea mbali na kusaidia jamii. Mango anatambuliwa kama mwanamume aliye na imani na mwanamke katika

harakati za kutega uchumi na kutunza mali ya familia kinyume na inavyodhaniwa kuwa wanaume hawana imani na wanawake kwa hivyo wanawake ni watu wa kupewa tu mahitaji yao ya kila siku. Haya ni kwa sababu wanawake wamedhihirisha sifa za uaminifu na uwezo wa kuzalisha mali na kuendeleza familia kama. Sakina anatambulishwa kama mwanamke mkarimu, mwaminifu, aliye na uwezo wa kuzalisha mali ili kukidhi mahitaji ya familia ndiposa mumewe Mango anampa nusu ya mapato yake ya ustaafu ili aanzishe nayo biashara kama anavyoelezea mwandishi:

> Nusu ya malipo ya Mango bandarini yalipewa Sakina. Sakina alianzisha kiduka cha kuuza kanda za video. Ni mwanamke aliyejua kuteka uchumi. Mango hakuwa na wasiwasi. (uk. 38)

## 2.7 Siasa na Uongozi

Kutoka siku za ukoloni baadhi ya vyeo katika uwanja wa siasa vimetengewa wanaume. Wanawake wa Kiafrika ni nadra kujitosa katika uwanja wa siasa mbali na kushikilia wadhifa wowote. Hii ni kutokana na fikra kuwa uwanja wa siasa unahitaji pesa nyingi na wanawake hawana pesa mbali na kukosa uongozi mwema.

### 2.7.1 Siasa na Uongozi Katika *Maumbile si Huja*

Uongozi unaodhihirishwa katika kazi hii ni wa kitabaka. Waarabu wamechukuliwa kuwa na hadhi wakilinganishwa na Waafrika hivyo basi, watu wengi wanatia juhudi ili kujitambulisha na Waarabu. Migawanyiko kitabaka inaendelezwa na ukoloni mambo leo na Waafrika wenyewe. Waafrika ambao wametambuliwa na Uarabu wanadhaniwa kuwa bora zaidi kama anavyosema Ayisha:

> “ Siyo lakini, nilizoeshwa kudai Uarabu ili kuishi.”(uk. 14)

Kwa muda mrefu wanawake Waafrika wameonyeshwa kama jinsia isiyoshiriki katika mazungumzo yanayohusu masuala ya siasa ila wanaume wanaodhaniwa kufahamu mambo yanayohusu siasa za nchi zao na nchi nyingine. Wanawake wanatambuliwa kuwa wasikilizaji wa wanaume au kupuuza yanayosemwa. Kwa kuwa wanawake ni washikadau katika harakati za kuleta maendeleo katika jamii, wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza washirikishwe katika uongozi na siasa za nchi husika. Wanaume wanatambuliwa kuwa katika mstari wa mbele

kupigania usawa wa jinsia kwa kuwashirikisha wanawake katika masuala ya kisiasa kama yanavyojitokeza katika mawasiliano kati ya mzee Mgeni na mkewe Ayisha:

> "Mama watoto, aliita Mgeni…..Wajua anasema nini huyu kijana ambaye alikuwa hapa?….Anasema eti amepigana na mwenzie kwa kutaka mpendeza tajiri wake…Tajiri atakufaaje kuliko mwenzako mnayefanya naye kazi?"….. "Yule Mwarabu ni mbaya? Mimi nadhani wewe nami tunayo damu ya Kiarabu mbona wamkashfu?" Ayisha aliuliza….. "Hata kama nina chembechembe za Uarabu maadam naishi janibu hizi na Waafrika wako radhi kunikubali kama ndugu yao kuliko walivyo Waarabu, mimi naona fahari kusema mimi ni Mwafrika….," alisema Mzee Mgeni..(uk14)

### 2.7.2 Siasa na Uongozi Katika *Paradiso*

Jamii inaonyesha jinsia ya kiume kama ndiyo iliyo na usemi serikalini kwa sababu ya nyadhifa zao katika siasa kutokana na ushawishi wao mkubwa. Kutokana na juhudi za wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika mambo sasa yamebadilika na mwandishi ameweza kufanikisha haya kwa kuwasawiri wanawake kama viongozi ambao wameboboea katika siasa kutokana na ushawishi wao serikalini na uwezo wao mkubwa kiuchumi. Lona anatambulishwa kama mwanasiasa, mwanamke kiongozi aliye na ushawishi serikalini kama anavyosema mwandishi:

> Hakuna tena kilichomtisha Lona…. Alidhibiti uchumi...Sasa alidhibiti siasa za nchi. Maana hata rais wa nchi alimfahamu. Si muhali kumwona akitumika siku za holidei akiomba au kama amekaa na wakubwa wa serikali huku kajipamba lile joho. (uk.131)

Juhudi za wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kupigania usawa wa kijinsia umefanikiwa kwani jinsia za kike na kiume zinasawiriwa kushikilia nyadhifa mbalimbali za uongozi katika asasi za kijamii ikiwemo dini kinyume na inavyodhaniwa kuwa jinsia ya kike haifai katika uongozi. Baadhi ya madhebehu yanasawiriwa kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume kutawala vitengo tofauti tofauti fauka ya kuwa makasisi wakuu kwa mfano, kanisa la New Jerusalem. Lona anatambuliwa kama mwanawake kiongozi wa dini kama anavyosema mwandishi:

> Lona sasa ndiye aliyechukua mahali pa Michael. Alikuwa mmoja wapo katika makasisi wa New Jerusalem. (uk. 79)

## 2.8 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia utambulisho wa jinsia katika asasi mbalimbali za jamii za Kiafrika zikiwamo ndoa, utamaduni, dini, elimu, siasa na uchumi. Dini kama ilivyo utamaduni ina mwelekeo wake katika ndoa. Hata ingawa asasi hizi zinadhaniwa kumnyanyasa mwanamke na kumpendelea mwanamume, utafiti wetu unaonyesha kuwa wote wanaume kwa wanawake wanaathirika sawa kutokana na hali ya mazoea na nia ya waja kupigania nafasi zao katika jamii.

Mwandishi ameonyesha kuwa wanawake ni viumbe sawa na wanaume na wanaweza kutekeleza majukumu waliyotwikwa na jamii si kwa msingi wa maumbile, bali kwa uwezo na tajiriba walizo nazo kama binadamu. Mwandishi anawasawiri wanaume kama washikadau wakuu katika harakati za kuleta usawa wa jinsia kwa kupigania ukombozi wa wanawake kutokana na tamaduni zinazowadhalilisha. Kutokana na harakati za jinsia za kiume na kike kutekeleza majukumu yao na kupigania usawa, jinsia hizi zinaathirika hasa jinsia ya kiume kutokana na mazoea ya kutimiza mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetuwezesha kushughulikia masuala yanayohusu jinsia ya kike kwa kuchunguza na kuchanganua uhusiano wao na jinsia ya kiume katika mazingira wanamoishi. Kwa kuegemea mihimili ya nadharia hii ya Ufeministi wa Kiafrika, mwandishi ameweza kuzisawiri jinsia za kike na kiume kwa kutumia matendo na mawazo yao, mawazo ya wahusika wengine na yale ya msimulizi.

# SURA YA TATU

## CHANGAMOTO WANAZOPITIA JINSIA KATIKA KUTAFUTA UTAMBULISHO

### 3.1 Utangulizi

Katika sura ya hii ya tatu tumechunguza na kuchanganua kazi za mwanadishi John Habwe za *Maumbile Si Huja* na *Paradiso* kwa malengo mawili; mwanzo, kuangazia changamoto wanazopitia wanawake na wanaume katika harakati za kutafuta utambulisho na pili, kudhihirisha athari zinazotokana na changamoto hizi kupitia asasi za dini, ndoa, elimu, utamaduni, siasa na uchumi. Utafiti wetu umefanywa kwa kuegemea mihimili ya Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na tuwezesha kuangazia jinsia za kike na kiume kwa pamoja.

### 3.2 Kiburi na Ubinafsi

Arege (2006) anasema ubinafsi ni hali ya mtu kuchukua hatua fulani au kufanya mambo yanayotosheleza masilahi yake binafsi pasi na kujali masilahi ya watu wengine. Ubinafsi una maana ya mhusika kutojali hisia au matakwa ya wahusika wengine kulingana na matendo yake ilhali kiburi ni hisia ya mtu kujiona kuwa bora zaidi kuliko watu wengine. Sifa hizi mbili huchangia migogoro na kuathiri uhusiano wa watu.

#### 3.2.1 Kiburi na Ubinafsi Katika *Maumbile Si Huja*

Mwandishi anamsawiria Juma, mwanamume Mwislamu, kama mbinafsi na mtu mwenye kiburi hali inayopingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kwa wanandoa. Ndoa ya Juma haujajengwa kwa msingi wa mapenzi hata ingawa wamefunga ndoa kufuatia mielekeo ya utamaduni na dini ya Kiislamu. Juma anajitambulisha kuthamini mali yake kuliko mkewe mbali na kushikilia utamaduni unaomnyanyasa mwanamke kwa kumnyima usemi jambo ambalo linaathiri uhusiano wao kama inavyojitokeza katika mazungumzo baina yao:

> "Njoo hapa wewe. Mbona wajikunyata kama yatima? Umekosa nini? Mali? Juma alisalia huku kabadili raha yake ya muda na kuwa kama ndume aliyehasiwa.
> "Usiniletee taasumbi za kike na siasa za kijinga zisizo na msingi wowote," Juma alionya na kusimama ili kuranda chumba chake cha fahari. (uk.3)

Mwandishi anaonyesha wanaume wanaoathiriwa kutokana hali ya ubinafsi na kiburi. Wafanikazi wa Mzee Juma ni mfano mwafaka, wanaathiriwa kwa kukosewa heshima, kuitwa majina ya kuchukiza na kuwafokea bila sababu. Hali hii inaathiri uhusiano wao kama anavyosema Kinyua:

> "Mimi sitaki kufokewa na mtu kwa kuwa yeye ni tajiri wangu;... Nastahiki heshima kama mwanadamu mwingine. Nitamkabili akinigeuza kinyago cha kuchezea. Hulka yangu siku zote ni kuwa na taadhima kwa yule mwenye roho ya utu. Lakini mtu akitaka kufanya maisha yangu yajae majonzi kwa kuwa eti yeye ni mkubwa sitakubali. Mkubwa ana haki gani ya kuninyanyasa eti kwa kuwa amebarikiwa? (uk 6)

Utamaduni wa Kiafrika unaopendekeza mtoto wa kike kuchaguliwa mchumba bila kuzingatia umri wala mapenzi unadhihirisha ubinafsi, mila chakavu na ubabedume kwa wazazi wanaofaidika kwa mahari anayolipiwa binti yao pasi na kuzingatia hisia zake. Ubinafsi huu wa upande wa wazazi unamwathiri mtoto wa kike kwa kumnyima uhuru wa kujichagulia mchumba jambo ambalo linapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaopigani uhuru wa jinsia ya kike wa kujichagulia mchumba kwa wakati unaofaa. Mwandishi anatambua msichana Sauda kati ya wasichana wanaoathiriwa na kipengele hiki cha utamaduni wa Kiafrika kwa kuachishwa shule jambo ambalo linaweza kuchangia wao kutoroka nyumbani wasijue wanakokwenda ili kuepuka kuolewa na wanaume wasiowapenda kama anavyosema Sauda:

> "Niliamua kukimbia .....Walitaka kuniuza ili ndugu yangu apate karo ya skuli…Mbona mimi Sauda niuzwe lakini asiuzwe Hassan?...Kidawa na Malaika waliuziwa vikongwe....Mimi sitaki. ...Mbona mimi Sauda niuzwe lakini asiuzwe Hassan? (uk.40)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapendekeza kujengwa kwa jamii yenye usawa wa kijinsia uaotokana na uhuru wa kupenda na kupendwa, elimu, uchumi na uongozini. Ili kuwe na usawa, mwanamke anastahili kuwa na uwezo wa kutega uchumi ili asiwe mtegemezi wa mwanamume. Ufeministi wa Kiafrika unapigania mwanamke mwenye maadili anapojiamulia mambo kwa kuwa yeye ndiye nguzo ya familia. Mwandishi anasawiri wanawake wanaopigania usawa pasi na kuzingatia maadili kutokana na ubinafsi kwa kutojali hisia za wengine na athari ya matendo yao yanayoweza kuleta talaka au kifo. Amina anajitambulisha kama mwanamke wenye kiburi na mbinafsi kama inavyojitokeza katika mawasiliano haya:

> " …Mimi na niitwe jeuri. Labda Said utanikosoa na kusema mimi si mwanamke mwenye taadhima…...." (uk. 46 )
> "Amina wangu nimekukosea nini?...Kumbe Said kama kunguru angojea kunidonoa. Ama ni kweli kikulacho ki katika nguo yako."
> "...Said ni kufu yangu japo ni hafukasti. Ni bora kuliko Uarabu wa jina tu. Ni mwanamume wa kweli..." (uk.75)
> Juma alikuwa kapoteza mawili – mpenzi na mali. (uk 83)

Ndoa ni zao la utamaduni linalochangia dhuluma kwa mwanamke kwa kudhaniwa kuwa mali ya mumewe kutokana na tendo la ulipwaji wa mahari. Jambo hili linadhihirisha kiburi na ubinafsi wa wanaume wanaotumia kigezo hiki kuwanyanyasa wanawake. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanapinga ulipaji wa mahari kama njia moja wapo ya kuwakomboa wanawake kutokana na tamaduni zinazowadhulumu. Mwandishi anawasawiri wanaume wanaothirika zaidi kwa kushikilia mila na desturi za kale na potovu kuwa mwanamke anastahili kumtumikia baada ya kumlipia mahari kama anavyoelezea mwandishi:

> ....Siku walipogombana mme aliweza kumweleza mkewe kuwa alikuwa kampa babake shilingi elfu sabini na kenda. Hiyo ndiyo sababu alimtuma 'kanifulie chupi, kanipikie hiki, nifanyie hivi' na kadhalika......Mwanamke huyu aliingia katika chumba cha kulala na akatokeza na pochi...Alimwandikia mmewe hundi ya shilingi sabini na tisa elfu isipungue hata shilingi moja. Mme yule kuona hivyo alihangaika na kuduwaa na kuzirai hatimaye. Ubwana wake wote ulidondoshwa na fedheha ikamtafuna utumbo. (uk 80)

### 3.2.2 Kiburi na Ubinafsi Katika *Paradiso*

Kiburi na ubinafsi umekithiri katika asasi ya ndoa kutokana na utamaduni wa kimapokeo unaopingwa na Ufeministi wa Kiafrika. Utamaduni wa Kiafrika unampa hadhi mwanamume aliyeoa wake wengi akilinganishwa na yule aliyeoa mke mmoja. Utamaduni wa Kiafrika unamtambua mwanamume aliye na uwezo wa kukidhi mahitaji ya familia yake bila kupuuza hata moja. Mwandishi anawasawiri wanaume wanaooa wake wengi lakini hawana uwezo wa kukidhi mahitaji yao kama inavyotarajiwa na kuwatwika wake zao majukumu amabayo si yao kwa msingi wa mila na tamaduni za Kiafrika. Mzee Mango anatambuliwa kuoa wake wengi kutokana na ubinafsi wake wa kutaka kutambulika japo hana uwezo wa kukimu familia hiyo kubwa kama anavyosema mwandishi:

> Mango alikuwa na watoto kumi na mmoja.....Kama ilivyo desturi ya kwao Bunyala, alioa wake watano... Wake wengine wa Mango waliishi Bunyala wakitegemea uvuvi katika ziwa Victoria. (uk1)
> Mango alisikiliza sana desturi za kwao. Kule mwanamume mwenye mke mmoja ni kama mtu mwenye chongo. Hakutambulika katika shughuli za pale kwao Budalangi. Hasa mwanamume kwa jina hilo na maana wasemapo haikuwa ruhusa kwake kusema. (uk.8)

Kwa muda mrefu jamii imemdharau mwanamke kwa kuwaona kama jinsia dhaifu isiyo na akili tambuzi. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasema kuwa unyanyasaji na udhalilishawaji wa mwanamke unaendelezwa na hali ya ubabedume inayomdhania mwanamke kutokuwa na uwezo wa kutoa maoni yanayoweza kuisaidia jamii. Mango anatambuliwa kupuuza ushauri wa mkewe kwa kuwa yeye si mwanamume kutokana na hali yake ya kiburi na ubinafsi. Hali hii inaathiri uhusiano wao na mkewe anaamua kujinyamazia ili mumewe afanye atakalo kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati yao:

> "Upasuaji wa aina gani? Atakuwa mwanamume baada ya huo upasuaji? Maana kama hawezi kuwa mwanamume ni wa kazi gani?....Ninataka ushauri toka kwa wanaume." Alisema huku akitembea kidogo kwa mikogo.
> "Wanaume watakueleza haya nikuelezayo," Zuhura alimtendekeza
> "Wewe si mume kwa hivyo, usinishauri," Mango alisema. ........
> "Haya," Zuhura alimwacha kifaru afanye atakavyo. Kwani mwana wake akitaka kumuua shauri ni lake. (uk. 4)

Jamii inawatambua wanawake kama watu wasioweza kushirikiana kwa sababu ya wivu unaochangiwa na ubinafsi na kiburi. Utamaduni wa Kiafrika unamtarajia mwanamke awe mnyenyekevu na anayetii mumewe kusudi kuwe na umoja hasa katika ndoa za wake wengi. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inahimiza ushirikiano wa wanawake kama sifa moja wapo inayochangia maendeleo katika jamii. Wanawake wanatambuliwa kupuuza ushirikiano kutokana na ubinafsi wa kutaka kuitawala familia zao. Zuhura anajitambulisha kama mwanamke mbinafsi na mwenye kiburi kwa kukabiliana na mwanamke mwenzake anayemdhania kuwa mpenzi wa mumewe kama inavyojitokeza katika mazungumzo yao:

> "Huyu ni wangu fundi." Zuhra alimtangazia mwenzake.
> "Umekosea babu," Sakina alimrekebisha
> "Kwa nini?" Zuhra alimwuliza huku akijifinya kiuno.....
> "Kwa sababu huyu ni dereva wangu. Mbona anakuacha na kuja huku?"
> "Ni nani asiyejua madawa yako?" Zuhra alimwuliza mwenzake....
> "Wewe zuzu hujui kumwangalia mwanamume. Uzuri uliojaliwa ni wa kazi gani? Nipe niutupie mbwa wa jirani wale."
> "Tafuta wako mume wewe hawara,"Zuhra alisema..... (uk 9)

Mwanamke Mwafrika anadhihirisha kiburi na ubinafsi katika harakati za kutaka kujikomboa kutokana na utamaduni unaomnyanyasa. Ufeministi wa Kiafrika unapigania uhuru wa mwanamke wa kupenda na kupendwa hata hivyo, mwanamke anastahili kuimarisha maadili na heshima. Mwandishi anawasawiri wanawake wa Kiafrika wanaojiingiza katika mahusiano yasiyo ya heshima kutokana na ubinafsi wao. Lona anatambuliwa kama mwanamke mbinafsi na mwenye kiburi kwa kutojali hisia za jamii anapoamua kuacha ndoa yake ya kwanza. Uamuzi huu unaathiri uhusiano wake na familia yake akiwamo mamake mzazi na mumewe Mganga kama inavyojitokeza katika mazungumzo yao:

> "Ndiyo ni mimi niliyempenda na ni mimi niliyemkataa. Sitaki kuulizwa maswale mengi," Lona alisema kwa madaha.
> "Mama, nimekuja katika nyumba hii kwa hesima yako. Lona ana hiari kupenda yeyote. Mimi nafikiria sina chuki naye. Nitamwacha. Sitachukua chochote. Hata na mtoto nitamwachia." Mganga alisema. Mganga aliposimama kuondoka mamake Lona akasimama pia naye. Waliondoka pamoja. Baadaye kila mmoja alishika njia yake. Lona hakushughulika na yeyote. Alibakia ndani ya nyumba na Joshua ambaye muda huo wote alikuwa anasoma Biblia...(uk.35)

Kiburi na ubinafsi ni chanzo kikuu cha maangamizi katika familia. Mwandishi anazisawiri familia zinazoathirika kutokana na hali ya ubinafsi unaochangiwa na tamaa ya wanajamii. Familia ya bwana Amuko inatambuliwa kuathirika kwa magonjwa kutokana na tamaa ya Amuko kutaka mali. Mwandishi anamsawiri Amuko kama mwanamume tena mzazi mbinafsi kwa kumtoa nduguye kafara mbali na kumnajisi bintiye ili apate mali. Matendo haya yanaifanya familia yake kuathiriwa kwa magonjwa na ukosefu wa amani miongoni mwa athari nyingine kama anavyoelezea mwandishi:

> Chanzo cha maradhi haya yalionyeshwa kuwa Amuko alikuwa amemtoa ndugu yake kafara kwa minajili ya kupata mali. ……Amuko alikuwa amemvua binti yake mbichi nguo na kulala naye. Binti yake Asami hakuwa amemjua mwanamume mwingine. Baba yake ndiye aliyemtangulia. (uk.41)

Viongozi wa dini wanatambuliwa kuendeleza ubinafsi kwa kutumia jina la Mungu kwa manufaa yao wenyewe kinyume na matarajio ya kijamii. Makasisi wanaotarajiwa kuwaongoza kondoo wa Bwana ndio wanaowapotosha zaidi kwa kuwashirikisha katika matendo maovu kama uasherati. Mwandishi anamsawiri Musa, kasisi katika kanisa la New Jerusalem kama kiongozi wa dini

anayeshiriki mapenzi na washirika anaostahili kuelekeza katika njia za Mangu kwa kuwajenga kiroho na kuvutia wengine kwa Mungu kama anavyosema mwandishi:

> Kyalo alimwona Musa kama afriti. Alimwona kana kasisi laghai aliyepoteza kondoo alopewa kuwatunza na kuwaangalia. (uk.59)

Dini inapendekeza ndoa kati ya mke mmoja na mume mmoja kwa msingi wa mapenzi na uelewano. Mwandishi anaonyesha ndoa ambazo zimejengwa kwa mapenzi ya wongo kutokana na ubinasfi wa wanandoa. Mwandishi anamsawiri Lona kama mwanamke mwenye ubinafsi kwa kutumia ushirikina ili kumdhibiti mume wake kwa mapenzi ya wongo kama inavyojitokeza katika mawasiliano haya:

> "Mume wako huyo nimekupa. Hataweza kwenda popote. Atakuwa hapo nyumbani akifanya kila jambo utakalopenda afanye. Utamtumikisha upendavyo....." Angela alisema (uk.109)

Ndoa ya Michael inatambuliwa kuathiriwa kutokana na ubinafsi wake wa kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Japo utamaduni wa Kiafrika unaunga mkono ndoa ya wake zaidi ya mmoja, unatambua ndoa zinazofungwa kwa msingi wa utamaduni husika. Utamaduni wa Kiafrika unampendelea mwanamume kwa kumpa uhuru wa kupenda na kumnyima mwanamke uhuru huo. Michael anatambuliwa kama mwanamume anayeshikilia Utamaduni unaompa uhuru wa kupenda kwa kushiriki mapenzi nje ya ndoa jambo ambalo linaathiri uhusiano wake na mkewe kama anavyoelezea mwandishi:

> Pole pole Michael alianza kuona uhusiano wake na Lydia ukiingia baridi. Michael alikinai kuwa Lydia hakumkosea lolote. Alimheshimu, kwanza, kama mumewe na pili kama mhubiri wake. Hata hivyo, moyo wa Michael ulianza kumwambia tu hafai. (uk. 150)

Nadharia ya ufeministi wa Kiafrika inahimiza jinsia ya kike iweze kujitambua ili itekeleza majukumu yake bila kutegemea jinsia ya kiume kinyume na inavyofikiriwa na jamii za Kiafrika kuwa mwanamke ni kiumbe tegemezi. Mwandishi anamsawiri Awinja kama mzazi tena mlezi mwema kwa kutafuta njia ya kusuluhisha changamoto wanayopitia Lydia na Michael katika ndoa yao. Mango anatambuliwa kama mzazi mwenye kiburi kwa kupuuza juhudi za Awinja mzazi mwenzake kwa kuwa yeye ni mwanamke kama anavysema Mango:

> “.......Biblia katika Mithali Nne inasema mwanamke mjinga huvunja
> nyumba yake kwa mikono yake,” Mango alisema. (uk. 159)

Mwanamke wa Kiafrika kwa muda mrefu amenyimwa uhuru wa kupenda na kupenda, jambo ambalo linapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika. Hata hivyo, hali hii inatambuliwa kuathiri wanaume zaidi wakilinganishwa na wanawake kutokana na kiburi na ubinafsi wa wanawake wa kuwanyima wanaume uhuru wa kupenda mbali na kuoa wake wengine. Mwandishi anamsawiri Lydia kama mwanawake mbinafsi kwa kujipendekeza kwa Michael ili amuoe baada ya kumwona kuwa mume bora kuliko wanaume wengine ambao amewahi shirikiana nao kimapenzi. Ubinafsi wake unachangia kuathirika kwa ndoa yao baada ya mumewe kugundua kuwa anampenda Patricia lakini si yeye kama anavyoeleza msimulizi.

> Atamsimbika vipi hadi akubali?.....Ingawa Lydia alikuwa na rafiki
> Luseno alikuwa mlevi wa kupindukia....hakuwa mwungwana.
> Alionekana mjanja na alikuwa na marafiki wengi......Patricia,
> alimwambia kuwa Michael alionekana mume mwenye matumaini
> makubwa hata kama elimu yake ilikuwa duni. (uk110)

## 3.3 Kutowajibika

Baadhi ya migogoro katika familia hutokana na hali ya kutowajibika kwa wanajamii. Migogoro hii hutokea pale ambapo mtu hutelekeza majukumu yake au kupuuza kusaidia kutekeleza shughuli fulani. Mbali na utelekezaji wa majukumu yaliyotengewa kila jinsia kama yalivyowekewa msingi na utamaduni wa Kiafrika, kutowajibika hutokana na mtu kutokubali matokeo ya matendo yake. Baada ya mtu kutenda mambo fulani, anabaki akijutia na hataki kuhusishwa na matendo hayo, labda kutokana na matokeo yasiyotarajiwa au yanayotarajiwa lakini hayakubaliki na jamii.

### 3.3.1 Kutowajibika Katika *Maumbile Si Huja*

Dini pamoja na utamaduni wa Kiafrika unasisitiza mume kumpenda mkewe na kuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya familia yake kama mume na mzazi. Mwanamume anatarajiwa kuwa katika mstari wa mbele kwa kuonyesha mkewe mapenzi kama wanavyosisitiza wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kuwa mwanamke anayeonyeshwa mapenzi ni mvumiliu na mnyenyekevu kwa mumewe. Wanaume wanatambuliwa kwa kutowajibika ikiwa hawawapendi wake zao wala

kukidhi mahitaji ya familia zao jambo ambalo huathiri ndoa zao kwa kuwalemaza wake zao kwa majukumu ya kukidhi mahitaji ya familia zao. Mwanamke aliyelemewa na majukumu mengi huwa mwenye hasira na uchovu hali ambayo huweza kuchangia talaka au utelekezaji wa majukumu muhimu ya familia. Mwandishi anatambua ndoa ya mzee Juma kuathirika kutokana na hali yake ya kutowajibikia jukumu lake la kuwa mume. Kwa sababu ya haya, mwandishi anamtambua Amina kama mwanamke asiyeweza kuvumila changamoto anazokumbana nazo katika ndoa kinyume na matarajio ya jamii kama anavyosema Amina:

> "Sasa naona sivumilii kabisa matendo ya Juma. Usione mpenzi ukasema ni mwanamume, ni mwanamume kwa jina tu. Wala si kwa maana hasa ya hilo jina. Labda hii ndiyo sababu hatuna hata mbegu yetu.... Si mwanamme kwa jina na maana!" (uk.46)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapendekeza wanawake kuhusishwa katika shughuli za ujenzi wa jamii kwa kuwa ili kuwe na jamii imara yenye maendeleo, taifa hutegemea jinsia zote. Kutokana na kupanda kwa hali ya maisha, wanawake wahusishwe katika shughuli za kutega uchumi ili kutosheleza mahitaji ya familia zao. Wazo hili linakwenda kinyume na fikra kwamba wanawake ni wategemezi wa wanaume kwani hawana uwezo wa kutega uchumi na sehemu yao ni jikoni. Mwanamke hulemewa asiposaidiwa katika shughuli za kutega uchumi na za nyumbani. Mwandishi anaonyesha wanaume wazembe wasiowajibikia majukumu yao ya wanaume na wazazi, wamepuuza kusaidia wanawake kukimu famila zao hali inayoathiri familia nyingi kwani inachangia vita hata kifo kama anavyosema mwandishi:

> ….alimpiga kwa kuwa hakumpikia na hakuwa amenunua chakula. Hao ndio wanaume wazembe... (uk.49)

Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanapinga ulipaji wa mahari kwa sababu ndicho chanzo cha dhuluma zote za mwanamke katika ndoa na kuhimiza wanawake kutoka katika ndoa dhalimu. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inashikilia kuwa mahari ni moja wapo wa vipengele vya utamaduni wa Kiafrika unaozuia haki za wanawake kutimizwa. Mwanamke wa Kiafrika hana haki ya kutoka katika ndoa dhalimu kutokana na mahari aliyolipiwa. Ni kashfa mwanamke kutoroka ndoa yake na akitoka, wazazi wake wanalazimika kurudisha mahari aliyolipiwa. Hata Wanaume wanatambuliwa kuathirika zaidi na tendo la ulipaji wa mahari kwa kuwa wanawake sasa wanakataa kudhulumiwa kwa kufanyishwa kazi nyingi kwa sababu wamelipiwa mahari kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> …..mme aliweza kumwelezea mkewe kuwa alikuwa kampa babake shilingi elfu sabini na kenda. Hiyo ndiyo sababu alimtuma.....badala ya kuwa mke wa kumtilia mapenzi ....Akamwandikia mmewe hundi ya shilingi sabini na tisa elfu isipungue hata shilingi moja. Mme yule kuona hivyo alihangaika na kuduwaa na kuzirai hatimaye. (uk 80)

### 3.3.2 Kutowajibika Katika *Paradiso*

Utamaduni wa Kiafrika umempa mwanamume jukumu la kukimu na kukidhi mahitaji ya familia yake ilhali mwanamke amepewa jukumu la kuzaa, kulea watoto na kutunza mumewe. Mwandishi anasawiri watoto waliotwikwa majukumu ya kukimu na kukidhi mahitaji ya familia zao baada ya wazazi wao kuyatelekeza kama anavyoelezea mwandishi:

> Mango hajasahau msaada wa mwanawe Michael...Mwanawe alimwondolea soni ambayo angevikwa kwa kutotosheleza mahitaji...Michael hakumsaidia yeye Mango tu bali hata ndugu zake. Aliwavisha nguo, wengine akawalipia karo ya shule na kuwatolea masarufu mengine. (uk. 105)

Utamaduni wa Kiafrika unamhusisha mwanamke na mambo mawili; uzazi na ulezi. Mwanamke anatambuliwa kama mzazi, mlezi, nguzo na kiongozi wa familia kwa kutoa mwelekeo mwafaka. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza kuwa malezi ya mtoto ni jukumu la wazazi wote kwa hivyo, wazazi wanastahili kuwajibika katika malezi ya watoto wao. Mwandishi anamsawiri Joshua kama mzazi aliyekosa kuwajibika katika jukumu lake la ulezi kama anavyoelezea mwandishi:

> Joshua alimhusudu Nice. Ama huko kumhusudu ndiko ambako kulimharibu..... Joshua alimtendekeza hasa alipokuwa bado ni mdogo. Hata Lona alipotaka kumrudi alipokuwa titiri, Joshua alimzuia, Mwana alifura kichwa. (uk. 85)

Kwa kawaida ni jukumu la wazazi kuwalea na kikimu wana wao. Mara nyingi watoto hupata shida ya malezi baada ya kifo cha mzazi mmoja au wazazi wote au panapotokea talaka. Mwandishi anaonyesha wazazi hasa wa kike wasiowajibikia malezi ya wana wao. Patricia anatambuliwa kama mzazi anayetelekeza wajibu wake wa ulezi na kumtwika mamake mzigo huo bila kujali umri wake na athari zinazotokana na hali hiyo kama anavyosema Wanjiro:

> "Mimi nimechoka kupagazwa mizigo na wana," Mama alipasua mbarika…….Leo huyu ni mgonjwa. Kesho yule mwingine ni mgonjwa. Baba yako aliniachia mzigo wenu nyinyi na sasa nyinyi mwanilemezea mzigo siutaki." (uk. 176)

Malezi ya watoto wao huwa rahisi ikiwa wanaishi pamoja na wazazi wao kama famila. Mazingira ya ulezi yanachangia ukuzaji wa tabia ya mtoto pamoja na mwelekeo wa wazazi. Watoto ambao wanatelekezwa na wazazi baada ya kuzaliwa huathirika kwa kukosa mwelekeo wa kuishi na kutelekeza majukumu waliyotwikwa na jamii. Mwandishi anasawiri wanaume wanaotelekeza majukumu yao ya ulezi kwa kutowajibikia matokea ya mapenzi yao. Mwanamke anayezaa nje ya ndoa anatambuliwa kukosa msaidizi katika malezi ya mtoto wake ilhali mtoto hukosa mwelekeo na mapenzi ya baba mbali na mtu wa kuita baba katika maisha yao. Michael anamtambua kama mwanamume asiyewajibikia matendo yake ya ngono kwani baada ya kumpachika mimba Patricia, anawatelekeza pamoja na mwanawe kama anavyosema patricia:

> …….Japo hakutarajia uhusiano wowote na Michael baada ya muungano alifikiria Michael angemshughulikia hadi akajifungua na hatimaye kumchukua mwanawe. Michael hakushughulika na lolote. (uk. 177)

## 3.4 Umaskini

Umaskini ni hali ya kutoweza kupata mahitaji ya kimsingi ya kila siku au kupata mahitaji haya kwa kiwango cha chini kisichoridhisha. Baadhi ya mambo yanayochangia umaskini ni utamaduni uliopitwa na wakati kama mume kuoa wake wengi asioweza kukimu, kutenga majukumu kwa msingi wa maumbile, wachache kumiliki nyenzo za uzalishaji mali miongoni mwa vyanzo vingine.

### 3.4.1 Umaskini Katika *Maumbile Si Huja*

Umaskini hutokana na hali ya waja kutomudu kujipa mahitaji ya kila siku kwa kiwango kinachoridhisha. Mahitaji ya kila siku hapa ni kama chakula, mavazi, malazi, makao na matibabu. Mwandishi anasawiri wanaume wanaosalia katika hali ya umaskini kinyume na wanavyodhaniwa kumiliki nyenzo kuu za kuzalisha mali. Said anatambuliwa kuathirika na hali ya umaskini kama anavyoelezea mwandishi:

> Katika kibanda hiki mitambaa panya ilikuwa imegeuka rangi na kuwa kama malaika weusi. Hii ilikuwa kwa sababu ya mvuke wa moshi uliopiga muda hata muda…. Ama kwa kweli vifaa vya kibanda hiki viliweza kuutwaa mtima wa yeyote na kuutia patashika. (uk. 1)

Umaskini hutokana na hali ya walio wachache kumiliki nyenzo za kuzalisha mali ilhali walio wengi hukosa nyenzo hizi ila nguvu wanazouza kwa walionao ili kupata mishahara duni isiyotosha mahitaji yao. Kwa kiwango kikubwa umaskini ni zao la mfumo wa siasa kitabaka unaonufaisha wachache. Wakati wa ukoloni Waafrika waliishi katika umaskini, lakini Waafrika bado wanatambuliwa kuendelea kuishi katika hali ya umaskini hata baada ya wakoloni kuihama nchi zao kama anavyoelezea Mgeni:

> Baba alihama kwa sababu Mombasa haikuwa janibu ya wangwana tena.... Nikabaki na mamangu. Tukawa tunauza madafu hapa Mwembe Tayari ili kupata masarufu. Nyumba yetu ilianza kunyongwa na kusongwa na mikono ya ufukara. (uk. 10)

Maisha ya waja wengi yanakumbwa na dhiki kwa kukosa mahitaji ya kimsingi kutokana na umaskini. Mwandishi anatambua baadhi ya waja wanaojiingiza katika mikakati yasiyokubalika na jamii ili kujiondoa katika umasikini. Said anatambuliwa kama mwanaume anayeshiriki mapenzi na wanawake kwa nia ya kujinufaisha kifedha. Said anajipata katika njia panda, hajui la kufanya, hana chaguo, hajui aitikie wito wa tajiri wake wa kuwa mmewe au la. Hali ya Said ya umaskini unamfanya kuwa mtegemezi na kuingia katika mapenzi yasiyohalali na mwajiri wake wa kike kinyume na fikra kuwa wanawake ndio wategemezi wa wanaume kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> "Tusahahu mambo ya Juma. Juma si nani wako. Tuangalie mambo yetu sisi wawili. Wataka nini ili tuishi pamoja kama mke na mme? Amina alitua mzigo wake wa maneno.
> "Labda nitakacho ni pesa," Said akaelezea waziwazi (uk.47)

### 3.4.2 Umaskini Katika *Paradiso*

Matatizo ya waja wengi yanatokana na hali yao ya umaskini. Inakuwa vigumu kwao kupata mahitaji muhimu tena ya kimsingi kama vile chakula, mavazi, malazi ikiwamo matibabu. Umaskini hutokana na hali nyingi ikiwamo familia kubwa, ukosefu wa nyenzo za kuzalisha mali miongoni mwa hali nyingine.Michael anatambulika kuathiriwa zaidi na hali ya familia yake ya umaskini kwa kukosa matibabu na elimu kama inavyojitokeza katika nukuu hizi:

> “ Nimekuja kumshauri mzee kama atampeleka mahali aangaliwe au atafutiwe dawa,” Sakina alisema. “ Dadangu suala kubwa ni pesa.....,” Zuhra alisema. (uk.14)
>
> Michael alikuwa amerudi shuleni. Baada ya kufaulu mtihani wake wa darasa la nane hakujiunga na shule ya upili pale Kongowea. Japo alipita vizuri baba yake alikosa karo ya kumlipia hata Shimo la Tewa ambayo ndiyo shule yake ya ndoto. (uk. 21)

Hakuna mja anayeridhishwa na hali ya umaskini. Kila mtu hujitahidi kujikwamua kutokana na hali hiyo. Kwa sababu hii watu wengi hukimbilia dini kunako miujiza kama ilivyo mahubiri ya kila siku. Binadamu wanatambuliwa kuvutiwa na mahubiri ya baraka kutokana na upandaji mbegu kama anavyosema Omae, kiongozi wa huduma ya vijana pale kanisani *New Jerusalem:*

> “…Kumbukeni zaka ni mbegu...Kila mtu apandacho ndicho avunacho..... Kumbukeni mtakapotoa Bwana atawarudushieni zaidi. Mtajenga nyumba, mtanunua magari na kuwa na pesa tele kuliko watu wa dunia. (uk. 54)

Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanashikilia kwamba, wanawake si wategemezi wa wanaume kutokana na uwezo wao kiuchumi. Wanawake wanaotegemea waume wao kwa mahitaji yao ya kila siku huathirika zaidi baada ya vifo vya waume zao. Wanjiro anatambuliwa kuathiriwa na hali yake ya umaskini baada ya kutumia urithi aliyowachiwa na marehemu mumewe kukidhi mahitaji ya familia ya watoto kumi. Wanjiro anasalia kuishi katika nyumba ya mbao, akitumia taa ya koroboi inayofuka moshi na chakula kwake ni shida kama anavyosema mwandishi:

> Mama yake Patricia sasa alikaa peke yake katika kijumba cha mbao. Maskini alijihurumia…..Taa ya koroboi iliyokuwa imetengenezwa kwa mkebe ilifuka kwa hasira moshi wake ukihinkiza nyumba nzima. (uk. 192)

## 3.5 Watoto na Malezi

Dini huwatambua watoto kama baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa wanandoa na kupata mtoto si jambo la lazima. Utamaduni wa Kiafrika umethamini watoto sana kiasi cha kuwa ni lazima mwanamke kujifungua, hasa watoto wa kiume kwa sababu wao ndio huchukuliwa kuendeleza vizazi. Mwanamke asiyeweza kuzaa hulaumiwa na mumewe huruhusiwa kumtaliki au kuoa mke mwingine ili amzalie watoto. Jambo hili linapingwa na wafuasi wa Ufeminiati wa

Kiafrika kwa kuwa hata mume anaweza akawa na tatizo la uzazi na ndoa haistahili kujengwa kwa msingi wa watoto ila mapenzi na ushirikiano wa wanandoa kama inavyochangiwa na dini.

### 3.5.1 Watoto na Malezi Katika *Maumbile Si Huja*

Suala la malezi ya watoto ni muhimu sana. Mtoto akilelewa vyema huwa na faida kwa familia na jamii yake hivyo basi jamii inahimizwa kuwapa watoto malezi yanayostahili kupitia wazazi. Mwandishi anatambua mambo kadha yanayochangia ukuzaji wa tabia za watoto; mazingira wanamoishi, hali ya wazazi wao na tabia ya mtoto mwenyewe. Haya yote yanachangia hulka za mtoto kama anavyosema Sauda:

> ....kuharibika kwa mtoto hutegemea na vitu vingi kama malezi, hirimu, mazingira, tabia ya wazazi, mapato ya wazazi na tabia au hulka ya mtoto mwenyewe. (uk. 41)

Jamii za Kiafrika zinathamini sana watoto kwa sababu,watoto wa kiume hutambuliwa kama nguzo ya familia kwa kuendeleza kizazi na watoto wa kike huletea familia mali kupitia mahari. Kwa sababu hii, familia hutamani kuwa na watoto jinsia zote mbili. Mwandishi anawasawiri wazazi wasiotosheka na watoto wa jinsia ya kiume na wako tayari kufanya lolote ili wapate watoto wa kike. Amina anatambuliwa kutoridhika na watoto wa kiume alio nao kama anavyosema mwandishi:

> Jambo ambalo lilimkere Amina ni kuwa hana mtoto wa kike...Aliona kuwa hajakamilika mpaka Mungu amjalie mtoto wa kike. (uk. 99)

### 3.5.2 Watoto na Malezi Katika *Paradiso*

Malezi ya watoto ni jukumu la jamii nzima na wazazi huwa walimu wa kwanza kwa watoto wao. Mwandishi anaonyesha jinsi wazazi wa kiume wanatelekeza majukumu yao ya malezi kama inavyotaraijwa na jamii. Mango anatambuliwa kutelekeza jukumu lake la malezi na kuwachia bibi zake majukumu haya. Mango anasawiriwa kuhamia mjini Mombasa na kuwatelekeza wakeze na watoto wake wanaoishi nyumbani Budalangi kama anavyosema mwandishi:

> Mango kuja nyumbani ataletwa na mkasa kama wa matanga au kwa nadra likizo ya Krismasi au labda masuala ya mashamba ambayo yeye mume ilikuwa lazima kuwapo. (uk. 1)

Jamii za Kiafrika huwathamini watoto kwa kuwa ndio wanaoendeleza vizazi na jina la familia husika. Baada ya mtu mzima kuoa au kuolewa ni lazima apate watoto ili atambulike kuwa amekamilika. Watoto wa kiume hupendelewa wakilinganishwa na watoto wa kike. Jamii za Kiafrika humlaumu mwanamke asiye na uwezo wa kupata mtoto pasi na kuzingatia uwezo wa mumewe, dhana ambayo inapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kwa kuwa mume pia anaweza kuwa na shida ya uzazi. Utamaduni wa Kiafrika unampendelea mwanamume kwa kumruhusu kuoa mke mwengine mke wa kwanza asipomzalia watoto. Hata hivyo, kuna wanaume wanaotambuliwa kufanya kinyume na matarajio ya jamii kwa kutooa kutooa mke mwengine japo mke wa kwanza amekawia au ameshindwa kupata mtoto. Kyalo anatambuliwa kutenda kinyume kwa kutomtaliki mkewe wala kuoa mke mwengine kwa kuwa mkewe amekawia kumzalia mtoto. Hii ni kwa sababu anaelewa fika kuwa mtoto ni Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> “Mume wangu nitakuruhusu uoe mke wa pili ili upate kuendeleza kizazi chako.”
> “Sitaoa mke wa pili mbali na wewe. Lengo la kukuoa wewe lilikuwa nipate mshirika kwa hivyo sidhani kama nitafanya kitendo kama hicho..”(uk. 59)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapigania usawa wa kijinsia. Jambo hili limefanikiwa kwa kuwa wanawake si wategemezi wa wanaume tena.Wanawake wanatambuliwa kulea watoto wao kwa hiari bila kulazimisha wanaume waliowazalisha kushiriki katika malezi yao. Awinja, mamake Lydia anatambuliwa kulea wanawe peke yake kwa hiari baada ya kuwapata nje ya ndoa. Hata ingawa ana rafikiye mwanamume, hamtegemei katika ulezi wa wanawe kama anavyosema mwandishi:

> Mamake Lydia, Awinja hakupata kuolewa ila alikuwa na rafiki yake Mgyriama, Kazungu. Huyu Kazungu ndiye aliyemzaa Lydia na baadaye kidogo akamzaa Leah… (uk. 83)
> ......mwanawe pamoja na nduguye aliwakuza yeye tu; kama baba na mama. Ulikuwa mzigo mzito lakini Maulana ndiye aliyemwezesha kuwalea mpaka wakawa watu. (uk173)

## 3.6 Kushikilia Mila na Desturi Chakavu za Kiafrika

Hadi kufikia sasa utamaduni wa Kiafrika umebadilika kutokana na mabadiliko ya kiteknolojia, utandawazi na mkurupuko wa maradhi mbali mbali. Jamii za Kiafrika zinakumbana na changamoto mpya kutokana na nia ya kutaka kushikilia tamaduni na kufumbata usasa. Hali hii inaathiri ushirikiano na uhusiano wa wanajimii.

### 3.6.1 Kushikilia Mila na Desturi Chakavu za Kiafrika Katika *Maumbile si Huja*

Jamii za Kiafrika kupitia zinashikilia kuwa kazi zote za nyumbani ni za mwanamke kwa hivyo, mwanamume hulaza damu na kumwachia mwanamke kazi zote za nyumbani. Wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika wanapendekeza wanandoa wasaidiane katika kutekeleza majukumu ya nyumbani kwa kuwa wanawake hulemewa na kazi hizi ikiwa watashirikishwa katika harakati za kutega uchumi ili kusaidia kukidhi mahitaji ya familia yao. Mwanamke asiyesaidiwa na mumewe anatambuliwa kuwa mtumwa wa mumewe kama anavyoelezea Mgeni:

> "Wanaume wengine ni washenzi. Wategemea wake zao kwa lolote liwali...alisema Mzee Mgeni (uk. 48)

Utamaduni wa Kiafrika unapendekeza ulipwaji wa mahari kama shukrani kwa familia ya msichana kwa malezi mema. Hata hivyo, mahari inadhaniwa kuwa ni malipo kwa msichana na hufanywa kuwa mbadala wa msichana anayeolewa. Mwanamke aliyelipiwa mahari anatambulishwa kama mali ya mumewe na familia yake. Dhana hii ya ulipwaji wa mahari inayomweka mwanamke chini ya mwanamume kama mali yake, inapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika na wanaume wanaotambuliwa kupiga kauli kuwa mwanamke ni mali ya mumewe na familia yake kama anavyosema Omar:

> "Siku za kufanya hivyo zimekwenda maana wanawake walishurutishwa kuvumilia na kupiga moyo konde na kuishi...kwa sababu baba zao walipenda mali mengi na walikuwa kama waliouzwa. Zamani hizo wasichana walikuwa ni vyombo badala ya kuwa wenza." (uk. 80)

Ndoa ni sehemu ya utamaduni wa Kiafrika ambayo humnyima mwanamke uhuru wa kuamua kuolewa wala kujichagulia mchumba dhana ambayo inapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika. Wazo hili limefanikishwa kwa kuwa wanawake na wanume wanatambuliwa kupigania

uhuru wa kujichagulia wachumba na kupinga dhana ya kuozwa kwa jinsia ya kike kwa lazima kama anavyosema Sauda:

> "Mzee Ramadhani alikuja nyumbani akitaka mke wa tatu. Kwa kuwa alitaka kuwapa mali, mama na baba walinishurutisha niwe mkewe...Mzee wa miaka themanini? Aa, siwezi kato siwezi. Afadhali waniuze kwa kijana ikiwa kweli utamaduni wangu wasema wauzeni vijana wa kike kwa yule atafutaye mchumba' (uk. 40)

### 3.6.2 Kushikilia Mila na Desturi Chakavu za Kiafrika Katika *Paradiso*

Utamaduni wa Kiafrika unampa mwanamume uhuru wa kuoa wake wengi ilmuradi awe na uwezo wa kukidhi mahitaji yao. Mwanamume aliyeoa wake wengi huheshimiwa na hupewa nyadhifa katika jamii kwa kudhaniwa kuwa kiongozi mzuri. Mwandishi anawasawiri wanaume wanaopinga kauli hii kwa kupendekeza ndoa ya mke mmoja. Mango anatambuliwa kujutia tendo lake la kuoa wake wengi ishara kuwa tendo la kuoa wake wengi huwa na changamoto nyingi kama anavyosema Mango:

> Zamani tulioa wake wengi sisis kwa kutojua. Lakini sasa kwa ajili ya uchumi na hatari ya magonjwa ni vizuri kwa watu kukaa kwa kuheshimiana na kusameheana (uk. 120)

Kila jinsia inataka kuheshimiwa na kusikilizwa kama inavyochangiwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika. Utamaduni wa Kiafrika unamdhalilisha mwanamke kwa kumnyima uhuru wa kujieleza. Mwanamke anastahili kuvumilia, kunyenyekea na kuheshimu mumewe katika hali yoyote kwa kufuata mwelekeo wa mwanamume hata kama haufai. Hali hii inamfanya kuwa kama mtumwa wa mwanamume na katika harakati za kutaka kujikwamua ndipo migogoro huzuka. Wanawake wanatambuliwa kudhulumiwa na mfumo wa ubabedume unaowanyima uhuru wa kujieleza wala kujiamulia mambo. Rose, mkewe Musa anatambuliwa kupitia dhuluma za kiubabedume kwa kunyimwa uhuru wa kuabudu kama anavyosema Musa:

> "Aaa. Nisikupate unakwenda kanisani. Wala sitaki kuelezwa mambo ya kike mimi. Nikisema hapa hapana wa kunieleza jingine. Kama wataka kuwa jogoo hapa basi sema tuagane". (uk. 65)

Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inapinga mila na desturi zinazoathiri jinsia hasa jinsia ya kike kisaikolojia na kimwili kama kurithiwa, kufanya matambiko, kushiriki katika unywaji pombe na ulaji wa nyama kama ishara ya umoja wakati wa matanga miongoni mwa mila nyingine. Mwandishi anatoa mfano wa wanaume wanaoathirika na mila hizi chakavu kinyume na inavyodhaniwa kuwa ni wanawake tu ndio wanaoathirika kama anavyosema mwandishi:

> Mango alihitajika baadaye afungiwe na marehemu mkewe katika chumba mbali na mtu mwingine yeyote. Hapo angempa marehemu buriani ili asikasirike kwa kufa hali mumewe yuko Mombasa (uk. 93)

## 3.7 Dhuluma na Ukatili

Kwa mujibu wa Chapman (2008) dhuluma ni kitendo chochote kinachoweza kuleta madhara ya kimwili, kimapenzi au kisaikolojia kwa mtu kunyimwa uhuru au kushurutishwa kufanya jambo fulani. Ukatili ni matendo ya kinyama yanayochangia madhara ya kiakili au kimwili.

### 3.7.1 Dhuluma na Ukatili Katika *Maumbile Si Huja*

Jamii za Kiafrika zinamtambua mwanamume aliye na uwezo wa kulipa mahari inayohitajika, mbali na kukidhi mahitaji ya familia. Dini inatambua mume mwenye mapenzi na heshima kwa mkewe. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza ndoa iliyojengwa kwa mapenzi, heshima na uelewano katika utekelezaji wa majukumu ya kijamii. Mwandishi anasawiri wanaume wanaochangia katika unyanyasaji wa wanawake kwa kuwanyima uhuru wa kutangamana na watu wengine mbali na kuwakosea heshima kutokana na namna ambavyo wanasema nao hata baada ya kuwaoa kwa msingi wa dini na utamaduni wa Kiafrika. Wanaume kama hawa wameshikilia mila hizi ili kuwanyanyasa wake zao. Juma anatambuliwa kama mwanamume dhalimu tena katili kwa kumnyima mkewe uhuru wa kutangamana na ulimwengu mbali na kumkosea heshima kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati yao:

> “ Mimi na yatima naona tu sawa. Kila siku nafokewa na kukaliwa kiyatima kwa ajili ya jinsia hii inifanyayo kiumbe duni,” Amina alilalamika
> “ Usiniletee taasubi za kike na siasa za kijinga zisizo na msingi wowote,” Juma alionya na kusimama ili kuranda chumba chake cha fahari (uk. 3)

Matajiri wengi hawana heshima kwa wafanyakazi wao. Kazi wanazofanya haithaminiwi na waajiri wao. Baadhi ya wafanyikazi hudhulumiwa kwa kupigwa, kutusiwa, kukosewa heshima na hata kuachishwa kazi bila arifu. Mwandishi anatoa mfano wa Juma kama tajiri dhalimu kutokana na anavyowafokea wafanyakazi wake, kuwaita majina ya kuchukiza na kuwapiga kalamu bila notisi kama inavyojitokeza katika mawasiliano haya:

> "……. Najua una jambo wewe mwanaharamu! Hata hivyo yafaa utahadhari nami Bwana. Kunidanganya kunaweza kunizonga mpaka nikakufuta kazi. Eeh! Sema. Unataka kalamu mwekundu?" Juma alibwata na kumgeuza Said tofali la barafu. (uk. 5)

Mwanamke wa Kiafrika ananyanyaswa kupitia utamaduni potovu unaosisitiza kuwa anastahili kuvumilia changamoto anazokumbana nazo katika ndoa ili kudumisha ndoa yake. Dini kama ilivyo utamaduni wa Kiafrika, inamtambua mwanamke mwerevu kama yule aliye na uwezo wa kutunza ndoa yake ilhali asiye na uwezo wa kuitunza ndoa yake ni mjinga. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanasisitiza kuwa ni jukumu la kila mwanandoa kutunza ndoa yake. Nadharia hii inawahimiza wanawake kweza watambua uwezo wao na kukataa kukandamizwa na wanaume kwa msingi wa utamaduni uliopitwa na wakati. Mwandishi anatoa mfano wa baadhi ya wanawake wanaopigania uhuru wao kwa kutambua haki zao kama anavyodhihirisha Amina, mwanamke Mwislamu:

> " Sasa naona sivumilii kabisa matendo ya Juma.....Ndugu mpenzi mali si kitu. Kitu ni kuvumiliana na kuheshimiana katika raha na taabu. Sina uhuru. Kama njiwa nimo kizimbani….Kwa kweli nina vitu hivyo na hata zaidi. Lakini ni faida gani ule chakula kizuri, uvae vizuri na ukose uhuru? (uk.47)

### 3.7.2 Dhuluma na Ukatili Katika *Paradiso*

Dini pamoja na utamaduni wa Kiafrika zinatarajia mwanamke kuwa mnyenyekevu na mvumilivu katika maisha ilhali mwanamume anastahili kumwonyesha mkewe mapenzi. Asasi hizi zinachangia dhuluma dhidi ya jinsia kwa kuilazimisha mwanamke kuvumilia changamoto inayopitia katika ndoa na pili na kulazimisha mwanamume kupenda mkewe hata mapenzi yanapokwisha kati yao. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza kuwa wanandoa wanastahili kuishi kwa mapenzi ya kweli kwa uelewano na iwapo uhusiano huu unapitia changamoto ambazo haziwezi kutatuliwa basi, wanastahili kupewa uhuru wa kutengana. Mwandishi anaonyesha jinsi baadhi ya wanawake ni katili kinyume na inavyodhaniwa na jamii kuwa ndio jinsia nyonge na dhaifu na tena ndio huathirika zaidi kutokana na ukatili wa jinsia ya kiume. Ukatili wa jinsia ya kike unajitokeza kwa kutumia uhuru wao kupenda na kupendwa kwa njia isiyostahili. Lona, mkewe Mganga anatambulishwa kama mwanamke katili na dhalimu kwa kutaliki mumewe na kuolewa na mume mwengine kwa kile anachokiita uhuru wa kupenda. Lona hajali athari ya matendo yake kwa

familia yake akiwamo mamake mzazi, anayejaribu kuwapatanisha lakini kwa ujeuri, Lona anakataa kutii kama inavyojitokeza katika mazungumzo kati yao:

> "Hiyo ndoa mimi sitaki," Lona alimkata mama mtu kauli.
> "Sitaki tu. Sina sababu." Lona alisema kwa ukali ambao kwao mamake hakumzoea.
> "Ndiyo ni mimi niliyempenda na ni mimi niliyemkataa.
> Mganga alikuwa amekaa ametulia. Hasongi. Hasemi. Wala hakasiriki.
> Alikaa kama maji mtungini.(uk 35)

Jamii inatarajia mzazi kudumisha maadili kwa kuwa na sifa kielelezo kama vile, uaminifu, imani kwa Mungu, huruma na uzalendo. Ni jukumu la kila mzazi kuhakikisha kuwa watoto wake wanapata mahitaji yao yote na kuwahakikisha haki zao. Mwandishi anawakashifu baadhi ya wazazi wanaochangia kuwa dhulumu watoto wao kwa kukiuka haki zao kutokana na tamaa zao. Mwandishi anatupa mfano wa Amuko wa kuwa mume tena mzazi katili kwa kumnajisi mwanawe na kumtoa ndugu yake kafara ili apate mali kama anavyosema:

> Amuko alikuwa amemtoa ndugu yake kafara kwa minajili ya mali……Amuko alikuwa amemvua binti yake mbichi nguo na kulala naye. Binti yake Asami hakuwa amemjua mwanamume mwingine. Baba yake ndiye aliyemtangulia. (uk. 41)

Matendo ya dhuluma na ukatili huharibu uhusiano kati ya wanajamii, huleta madhara ya kimwili, kiakili miongoni mwa athari nyingine. Kyalo, mumewe Salome anatambuliwa kama mwanamume katili anayemjeruhi Kasisi Musa baada ya kumfumania chumbani pake kama anavyoelezea mwandishi:

> Salome, mkewe alikuwa na mwanamume mle ndani…….Alichomoa swodi yake ya Kisomali na kumdunga kwa ile swodi mara mbili akaanguka chini. (uk. 51)

Viongozi wa makanisa wanaotarajiwa kupigania uhuru wa watoto na hasa wasichana, kujichagulia wachumba, ndio hasa wanachangia dhuluma dhidi ya watoto wasichana kwa kuwalazimisha watoto wao kuolewa na wanaume wasiowapenda jambo linalopingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaosisitiza uhuru wa kupenda na kupendwa. Mwandishi anatoa mfano na kuwakashifu Kasisi Joshua na mkewe Lona kama wazazi katili kwa kumshurutisha mwana wao Nice akubali kuolewa na mhubiri Michael. Tendo hili linamwathiri Nice kimwili na kisaikolojia kwa kupigwa, kutelekezwa na kukaripiwa kama inavyojitokeza katika maongezi haya:

> "Kwa nini mnitafutie, mama? Nice alisema huku ana hasira.
> "Lazima tukutafutie mwanangu kwa sababu tabia yako ni mbaya," alisema baba mtu.
> "Sitaki!
> "Kama hutaki utafute wazazi wengine. Usituite wazazi," Joshua alisema huku ameshika mshipi mkononi na kumrapulia Nice kama hatasikiliza. (uk. 73)

Dini kama ilivyo utamaduni wa Kiafrika, inamtambua mume anayependa mkewe kama nafsi yake. Mume ana jukumu la kumtunza mkewe kwa kuwa ni kiumbe dhaifu na msaidizi wake. Mwandishi anatoa mfano wa wanaume wanaopuuza wito huu kwa kuendeleza dhulumu dhidi ya wanawake. Bjorn Hard, mkaza mwana wa Alice anatambuliwa kama mwanamume katili na dhalimu anayempiga na kumuua mkewe, Nicole. Kifo cha Nicole kinaathiri mamake, Alice kisaikolojia kwa kuwa yeye ni mwanawe wa kipekee kama anavyoelezea mwandishi:

> Bjorn alikuwa amemwoa mwanawe Alice wa pekee, Nicole. Baada ya ugomvi wa nyumbani, Bjorn Hard alimwua;.... Baada ya kifo cha Nicole, Alice alihuzunika kupita kiasi. (uk. 149)

## 3.8 Hitimisho

Katika sura hii tumefafanua baadhi ya changamoto wanazopitia wanawake na wanaume katika kusaka na kutafuta utambulisho wa jinsia ikiwamo kiburi na ubinafsi, kutowajibka, umaskini, mila na destrui chakavu za Kiafrika, watoto, dhuluma na ukatili. Ni kati ya changamoto hizi ndizo zinazotokana na harakati za wanajamii kutekeleza majukumu yao.

Ni wazi kuwa changamoto hizi ni za kawaida katika maisha ya wanadamu na huwa vigumu kuziepuka. Ili kuwe na uhusiano mwema kati ya wanajamii, watu wanastahili kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hizi. Kufahamu chanzo cha changamoto hizi kutasaidia wanajamii kutambua namna ya kujiepusha navyo na kusuluhisha matatizo wanayokumbana nayo ili kudumisha uhusiano mwwma miongoni mwao. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imetuwezesha kuangazia changamoto wananazopitia wanawake katika harakati zao za kutaka utambulisho na kudhihirisha athari zinazotokana na changamoto hizi katika mahusiano yao na wanaume katika mazingira wanamoishi.

# SURA YA NNE

## MABADILIKO YA MIELEKEO KATIKA JAMII KUHUSU UTAMBULISHO WA JINSIA

## 4.1 Utangulizi

Utamaduni wa Kiafrika unashikilia kwamba ushirikiano wa kijamii unategemea mwanamke kuafiki itikadi na kanuni za jamii husika. Utamaduni unampa mwanamke utambulisho kwa msingi wa uana, mila na itikadi za jamii husika. Wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika wanashikilia kwamba, utambulisho wa mwanamke kama mtu binafsi, unastahili kuzingatia mahusiano mema baina yake mwanamume. Mwanamke anatakiwa akatae kudhibitiwa na utamaduni na dini jambo ambalo linapigwa jeki na jinsia ya kiume. Jinsia ya kiume inachangia katika ukombozi wa jinsia ya kike kutokana na ushirikiano wao mwema.

Binadamu wanajitahidi kupigania ukombozi na usawa wa jinsia na kupuuza taratibu na mielekeo iliyowekwa kwa msingi wa utamaduni wa kimapokeo. Jambo hili linachangia changamoto zinazotokana na harakati za kutaka utambulisho wa jinsia kwa kukosa mwelekeo mwafaka. Changamoto hizi zinatishia kuharibu zaidi uhusiano wa wanajamii kama hautashughulikiwa kwa uangalifu. Wataalamu wa elimu jamii kama Benokraitis (1989) na boss (1993) wanasema kwamba, changamoto ni jambo la kawaida katika mahusiano yoyote ila namna ya kuzishughulikia ndiyo inayoweza kuzorotesha au kuimarisha uhusiano huo.

## 4.2 Mabadiliko ya Mielekeo ya Jamii Kuhusu Utambulisho wa Jinsia Katika *Maumbile Si Huja*

### a) Ndoa

Fasihi ni kioo cha jamii kinachomulika na kuangazia hali halisi katika jamii. Jamii hubadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kuzuka kwa teknolojia mpya na mabadiliko ya kisiasa. Mabadiliko haya yanachangia mabadiliko katika asasi ya ndoa kama ilivyowekewa msingi na utamaduni wa kimapokeo. Mabadiliko haya yanaongezea asasi ya ndoa madhila kutokana na usasa unaoendelea kukita mizizi na ukale unaofifia. Kwa mfano, kuwepo kwa mawasiliano finyu kati ya wanandoa, ubinafsi na tamaa unaotokana na hali ya kupenda mali badala ya wanandoa kupendana. Wanandoa wana jukumu la kudumisha ndoa yao kwa kujitolea, kuvumiliana na kuheshimiana.

Ndoa itadumishwa ikiwa mume au mke atamwona mwenzake kama tuzo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kama tunavyoambiwa katika kitabu kitakatifu cha Biblia (mwanzo 2:21-22), Mungu alimuumba Hawa kutoka ubavu wa Adamu jambo ambalo linaashiria kuwa ndoa ya kwanza iliidhinishwa na Mungu na wanandoa ni mwili mmoja. Kwa hivyo, mume anastahili kumpenda mkewe kama nafsi yake. Baadhi ya ndoa za Kiafrika zinakosa mapenzi kutokana na dhuluma wanazopitia wanandoa wa kupigwa na kuteswa.

Ufeministi wa Kiafrika unapigania uhuru wa mwanamke wa kupenda na kupendwa ili kujiondoa katika minyororo ya kimapenzi. Wafuasi wa nadharia hii wanapendekeza mwanamke kuishi katika ndoa yenye mapenzi na uelewano kati ya wanandoa. Ndoa ya Juma na Amina inatambuliwa kukosa mapenzi na heshima ila Juma anapenda mali yake kushinda mkewe jambo ambalo linachangia mkewe kutoka katika ndoa hii kama anavyosema Amina:

> "...Wewe ni nani na wewe ni nini? Juma tu? Na Mawrabu mwenye mali. Sikutaka mali, nilitaka mme. Tena mme mpenzi na mme mwenye utu.." Amina aliuliza, dharau imemjaa usoni...(uk75)

Tendo la ndoa ni muhimu kwani linahusisha hisia za kimwili ambazo wanandoa wanastahili kutimiziana. Hata ingawa mwanamke anataka kutosheleza ashiki yake inayopuuzwa katika baadhi za ndoa za sasa na kufanya ndoa kuwa himaya ya mume, ni jukumu la mke kumfurahisha mumewe kimapenzi. Wanandoa wanastahili kudumisha maadili mema baina yao. Kulingana na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, mwanamke anastahili kutambua kuwa yeye tu ndiye aliye na uwezo wa kutambua kile anachokihitaji. Mwandishi anaonyesha jinsi Amina kama baadhi ya wanawake wanavyopigania haki zake na kupiga dhana kuwa mwanamke ni chombo cha starehe kwa mwanamume ila wote wanastahili kutosheleza hisia kama anavyosema:

> "Ndiyo, ulinioa lakini kwa muda huo wote sikuhisi kama mtu aliyeolewa…..Said ni kufu yangu… Nikiwa naye sina wasiwasi juu ya wanaume wengine. …..Said yu radhi kunipa pendo. Nami niko radhi kumlipa kwa maisha yangu." (uk. 75)

Ndoa ni asasi ya jamii inayonuiwa kujenga uhusiano mpya na kupanua familia. Familia za pande zote mbili hushirikishwa katika mjadala na shughuli zinazohusiana na ndoa. Ushirikiano na uhusiano huu unanuiwa kuleta familia husika pamoja. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza kuwa ndoa ni mkataba wanandoa wanakubaliana kuishi pamoja kwa haiari bila kulazimishwa hivyo basi, jamii ina sehemu kidogo sana ya kuchangia katika maisha yao. Mwandishi anatambua

wananawake wanaodhihirisha ujasiri wao wa kujiamulia mambo yanayohusu uchumba. Tunatambua Sauda kama msichana anayekiuka utamaduni wa kimapokeo wa kuchaguliwa mchumba kwa kutoroka nyumbani baada ya kuozwa kwa mzee wa umri wa babu yake na kwenda mjini kuanza maisha na kijana wa umri wake kama anavyosema:

> "....nyumbani baba yangu alinieleza eti alitaka kunioza kwa Mzee Ramadhan. Mimi nilikatalia mbali pendekezo hilo lisilo mantiki. Hii ndiyo sababu nilitoroka nyumbani na kuja huku. Sasa....... nikapatana na Kinyua akawa msena wangu na tunaishi pamoja. Sauda akayakamilisha maelezo yake. (uk 50)

Wamitila (2002) anasema kwamba, ndoa ni mojawapo ya asasi za kijamii zinazoendeleza unyanyasaji wa jinsia ya kike. Asasi hii imejengwa kwa imani na uwezo mkubwa wa mwanamume ambayo inampa mwanamke nafasi chini ya mumewe kutokana na tendo la ulipaji wa mahari. Jamii za Kiafrika zinatumia mahari kama mnyororo unaomfunga mwanamke kwa mume hata anapopitia mateso, anatarajiwa kuvumilia kwani anapotoroka wazazi wake hulazimishwa kurudisha mahari aliyolipiwa. Jambo hili linapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaopigania ukombozi wa mwanamke kutokana na tamaduni za kale. Mwandishi anatambua baadhi ya wanaume wanaochangia katika vita vya ukombozi wa mwanamke kinyume na ilivyodhaniwa kuwa wanaume ndio wanaochangia dhuluma dhidi ya wanawake na kamwe hawawezi kupigania ukombozi wao kwa kupinga ulipwaji wa mahari kama anavyosema Omar:

> "Siku za kufanya hivyo zimekwenda ndugu. Maana zamani wanawake walishurutishwa kuvumilia na kuupiga moyo konde na kuishi. Hii ilikuwa ni kwa sababu baba zao walipenda mali mengi na walikuwa kama waliouzwa. Zamani hizo wasichana walikuwa ni vyombo badala ya kuwa wenza." (uk. 80)

### b) Dini

Dini ni mojawapo ya asasi za jamii zinazomtukuza mwanamume na kumtweza mwanamke hasa dini za Kiislamu na Kikristo zilizo na mizizi yake katika Mashariki ya kati. Tamaduni za dini hizi zimeshikilia mfumo wa ki- ubabedume zinazoendeleza unyanyasaji wa mwanamke kwa kumpa nafasi chini ya mwanamume. Hazimpi mwanamke nafasi uongozini kama ilivyo dini ya Kiislamu na baadhi ya madhebehu mengine ya Kikristo. Kwa mfano, kanisa la kikatoliki ambalo haliwaruhusu mwanamke kushikilia wadhifa wa uaskofu. Mwanamke anahitajika kumnyenyekea na kumtii mwanamume kama ilivyoandikwa katika Biblia takatifu (Waefeso 5:22 – 25). Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanapigania jamii inayowashirikisha wanawake uongozini bila

kuwabagua kutokana na msingi wa kimaumbile. Mwandishi anawasawiri wanawake kama binadamu walio na uwezo sawa na wanaume katika uongozi kinyume na ilivyodhaniwa kuwa wao ni viumbe dhaifu na hawana akili tambuzi ya kuamua mambo muhimu kama anavyohitajika kiongozi yeyote. Wanaume wanatambuliwa kama washikadau katika harakati za kupigania usawa wa jinsia kama anavyosema Suleiman:

> " Mimi sijui dini nyingine isemavyo lakini kulingana na dini ya Kikristo, wote, wanaume kwa wanawake wanapaswa kuwa sawa katika Agano Jipya. (uk. 82)

Dini ni asasi inayoongoza katika unyanyasaji wa jinsia kimavazi, jinsia ya kike inanyanyaswa kwani dini inatambua wanawake waliovaa mavazi marefu yasiyobana kuwa na maadili wakilinganishwa na wale wanaovaa mavazi mafupi yanayobana. Dini ya Kiislamu ndiyo inayoongoza katika dhana hii kwa kusisitiza aina fulani ya mavazi, kanzu kwa wanaume na buibui kwa wanawake. Wanawake wanatrajiwa kujifunika buibui hata wakati wa jua kali na joto.Teknolojia na biashara imechangia kubadilika kwa mtindo wa mavazi kutokana na uigaji wa aina ya mavazi ya jamii nyingine kutokana na uhuru wa kuvaa kama anavyosema mwandishi:

> ....kulikuwa na mwanamke wa kizungu mzee aliyevalia minisketi, na mmewe ambaye... alivalia *jeans* ya kubanana viatu vya raba. Kundi la wanaume wa asili ya Ki-Asia liliwaangalia kwa kusinywaa na nyuso zao zikawa kama zinazosema, 'nyinyi ndinyi mnaotupujulia maadili na ustaarabu wetu'. (uk. 34)

### c) Utamaduni

Urithi ni hali ya kupokeza mamlaka ya umiliki wa mali au kitu kingine kutoka mtu mmoja hadi mwingine akiwa hai au baada ya kifo chake. Urithi ni kipengele cha utamaduni wa Kiafrika unaochangia upokezaji wa mali na mamlaka kutoka kizazi kimoja hadi kingine akiwamo mwanamke anayetambuliwa kama mali ya jamii. Mwanamke wa Kiafrika anatambuliwa kuwa mke wa jamii na endapo mumewe angeaga dunia, angetunzwa na familia yake kwa kurithiwa. Mamlaka ya uongozi inadhaniwa kumilikiwa na jamii husika hivyo hupitishwa miongoni mwao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mwandishi anazungumzia kubadilika kwa mambo haya kwani kuna baadhi ya wazazi anaowaonyesha kupuuza kuwapa watoto wao urithi kama inavyotarajiwa na jamii kama anavyosema Mzee Mgeni:

> "..Baba alihama.... Ajabu ni kwamba hakunichukua ili kwenda naye. Nikabaki na mamangu.... Ama kwa kweli babangu hakutaka kunirithisha kama mwanawe." (uk. 10)

Utamaduni wa Kiafrika unamtukuza mwanamume kwa kumtambua kama kiongozi wa familia na kumtweza mwanamke kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume. Mwanamke anastahili kufuata mielekeo ya mwanamume hata kama haufai. Mwandishi anatoa mfano wa baadhi ya wanaume wanaopigania na usawa wa jinsia kwa kupinga dhana kuwa mwanamume ni bora zaidi ya mwanamke kama inavyopiganiwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kwamba, jinsia zote ni sawa japo zi tofauti kimaumbile kama inayvvojitokeza katika mawasiliano haya:

> "Lakini mzee utamaduni unasemaje? Nafikiria tukifuata utamaduni mume ndiye kiongozi wa nyumba."
> "Wewe na utamaduni gani ambao unakupa hadhi ya juu kwa mwanamke?" Mzee aliuliza.
> "Kama Mwafrika mwingine, au hukusema tuwe kama Waafrika? Ndivyo, sisi twapaswa kufuata utamaduni wa Kiafrika wa kisasa maanake ndio unaoingiliana na maisha yetu?"(uk. 30)

Kwa muda mrefu jamii za Kiafrika zimekuwa zikiwachagulia watoto wao wachumba hasa wana wao wa kike. Utamaduni wa Kiafrika umemnyima mwanamke uhuru wa kupenda kwa kumchagulia mchumba bila kujali umri wala hisia, bora mume awe na uwezo wa kulipa mahari inayohitajika. Mwandishi anatambua mchango wa wanaume katika harakati za kupiga vita desturi hizi zinazowanyanyasa wanawake kama anavyosema Mzee Mgeni:

> "Mwanangu, sikiza. Siku hizi mambo yamebadilika. Huwezi kumchagulia binti yako mchumba. Tena mchumba asiyempenda. Afaa kuchagua mwenyewe, …Endapo ni mali mwanangu unapaswa kuitengeneza wewe na mumeo ili nyote muifurahie. La sivyo, mwanamume mwenye umri mkubwa atakulisha mchanga huku akidai eti ana tajiriba ya maisha kuliko wewe." (uk. 51)

Jamii za Kiafrika zinamtambua mwanamume aliye na uwezo wa kujenga ndoa kwa msingi wa itikadi za utamaduni husika. Ndoa inamweka mwanamke katika hali chukizi ya kuwa mtumishi wa nyumbani na mtegemezi wa mumewe. Mwandishi anaonyesha baadhi ya wanaume wanaochangia kauli kuwa wanawake wana akili tambuzi kama walivyo wanaume na ili wanawake wajikwamue kutoka katika fikra hii potovu inawategemea wao kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> "...Lililobaki enzi hizi ndugu ni kuishi na mwenzio nyote mkichuma. Hamna haja ya kugeuza mtoto wa mtu na kumfanya mja kazi."
> "Lakini hii itakwepo tu ikiwa baba nao watakoma kuwauza binti zao. Vile vile wanawake nao waanze kuwa na tabia ya kiutuuzima. Yaani wajue kujitegemea," Suleiman alieleza (uk 81)

Ulipaji wa mahari ni moja wapo wa desturi za tamaduni za Kiafrika. Baadhi ya jamii za Kiafrika zinapendelea mwanamume aliye na uwezo wa kulipa mahari kama inavyopendekezwa na familia ya mwanamke kama shukurani kwao kwa malezi ya msichana wao wala si mbadala wa msichana huyo. Mwandishi anawasawiri baadhi ya wanaume wanotumia kigezo hiki cha ulipaji mahari kummiliki mwanamke jambo linalochangia kuharibika kwa uhusiano wa wanandoa na familia kwa jumla. Mwandishi anaonyesha kuwa jinsia ya kiume ndiyo inayoathirika zaidi kama anavyosema Omar:

> "Lakini babake Amina, Bilali, alidai pesa nyingi sana. Nasikia alimwambia Juma ampe shilingi elfu mia mbili....Hata hivyo hakuwa na sudi. Malengo yake hayakutimia kama wasemavyo kuwa usione umelenga ukadhani eti umefuma." Omar alielezea(uk.80)

### d) Elimu

Elimu imechangia katika kuendeleza matabaka ya kijamii kutoka siku za wakoloni ambao waliitumia kutenga na kuhakikisha Mwafrika amesalia katika hali duni kiuchumi. Hii ni kwa sababu wachache waliosoma walikuwa na nafasi ya kupata kazi na kujiinua kiuchumi. Hivi sasa mambo yamebadilika, wazazi wanajitahidi kusomesha wana wao ili watambulike katika ramani ya jamii mbali na kupata ajira ya kuwainua kiuchumi. Baadhi ya familia za Kiafrika zinatambuliwa kuwasomesha wana wao kwa udi na uvumba kutokana na hali yao ngumu kimaisha. Mwandishi anatoa mfano wa familia ya Mzee Magongo Athman kama baadhi ya familia zinazothamini elimu kama inavyojitokeza katika nukuu hii:

> "Mimi nilikuwa nikisoma katika darasa la nne….Mwalimu mkuu alitufukuza shuleni ilitutafute karo. Mimi na ndugu yangu Hassan tulikwenda nyumbani kumshtakia baba yangu hali yetu" (uk. 50)
> "Makombo hakusoma elimu ya kisasa lakini aliwashangaza watu alivyoelewa mizungu ya maisha ....(uk96)

Mambo yanayohusu elimu yamebadilika kwa hali ya juu baada ya Waafrika kugundua umuhimu wa elimu. Jamii za Kiafrika zinatambua kuelimisha wana wao bila kuwabagua kwa msingi wa jinsia kama anavyoeleza Sulieman:

> "......Bibi huyu alikuwa amemimina masomo kwelikweli. Bwana huyo naye alikuwa amebukua kama kadhi mzima..." (uk 80)

### e) Uchumi

Kwa muda mrefu wanamke wa Kiafrika wamedhaniwa kuwa wategemezi wa mwanamume kutokana na hali yake duni kiuchumi. Mwanamume wa Kiafrika anatambuliwa kuwa mmiliki wa nyenzo kuu za kuzalisha mali. Jamii za Kiafrika zinamnyanyasa mwanamke kwa kumtengea nafasi za chini kikazi zisizozalisha mali. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanapigania jamii yenye usawa kwa kuwahimiza wanawake kutambua na kutumia uwezo wao kuzalisha mali ili kujikwamua kutoka chini ya mamlaka ya mwanamume. Mwandishi anasawiri wanawake waodhihirisha uwezo sawa na mwanamume katika harakati za kutega uchumi kama inavyotokea katika nukuu hizi:

> Kinyua aliishi na Kibamba Sauda kama kimada......Kinyua aling'nga'ana na vibarua bandarini kwa kupakua na kupakia mizigo. Sauda aliuza mchicha. Maisha yakaendelea. (uk. 44)
> "…Unaona mwanangu? Wanaume wengine ni washenzi. Wategemea wake zao kwa lolote liwalo…." Alisema Mzee Mgeni. (uk. 49)

### f) Siasa na Uongozi

Waarabu wanadhaniwa kuwa bora kuliko Waafrika kutokana na uwezo wao mkubwa kiuchumi. Wao ndio waomiliki wa nyenzo za kuzalisha mali na nyadhifa za uongozi katika bara Afrika kwa muda mrefu. Mwandishi anaonyesha baadhi ya nchi za Kifrika zinazojitawala baada ya wakoloni kuihama bara hili la Afrika kama anavyosema Mzee Mgeni.

> "…Lakini zamani za Mwarabu mwanangu, Mwarabu alikuwa mtu.
> ..... Hata hivyo yuko wapi? Amezama jii. Hasikiki." (uk. 10)

Bara Afrika bado linashuhudia athari za ukoloni kutokana na ubaguzi unaoendelezwa na Waafrika kwa misingi ya dini na rangi. Ukoloni mamboleo unachangiwa na Waafrika wenyewe kwa kuwadhalilisha wenzao wasio na usuli wa Kiarabu kwani Waarabu walidhaniwa kuwa bora kuliko Waafrika. Waafrika wanatambuliwa kupigania umoja wa Waafrika kwa kukubali hali ya wenzao ilivyo bali si kwa kigezo cha Uarabu kama anavyosema mzee Mgeni.

> "Zamani hatukuwa na masikizano, hii ndiyo sababu Mreno na Mwarabu walituvuna na kututia katika madau.....Sitaki uwe na moyo huo, mwanangu….Ni kwa nini hampendi kujiita Waafrika? Ama unakasumba eti mtu aliye na ngozi nyekundu kama Mzungu, Mhindi na Mwarabu ndiye kielelezo cha mwanadamu bora?" (uk. 13)

## 4.3 Mabadiliko ya Mielekeo ya Jamii Kuhusu Utambulisho wa Jinsia Katika *Paradiso*

### a) Ndoa

Ndoa ni kipengele cha utamaduni wa jamii za Kiafrika. Mwanamume wa Kiafrika ana uhuru wa kuoa wake wengi bora awe na uwezo wa kukimu na kukidhi mahitaji ya familia hiyo. Mwanamume aliyeoa wake wengi ni mtu wa kutajika na hupewa heshima mbali na kupendelewa uongozini. Mambo yamebadilika kwani wanaume ndio wanaojitambulisha kupinga kauli ya kuoa wake wengi kama inavyopendekezwa na utamaduni wa Kiafrika. Mango anatambuliwa kupinga dhana ya kuoa wake zaidi ya mmoja kama anavyoelezea:

> Zamani tulioa wake wengi sisi kwa kutojua(uk. 120s)

Dini inampa mwanamume mamlaka juu ya mwanamke kwa kuwa yeye ndiye mtoa mwelekeo na mwanamke anastahili kufuata kwa unyenyekevu. Mwanamke anadhaniwa kuwa ni kiumbe dhaifu asiye na akili tambuzi inayowezo kutoa ushauri uliokomaa wala kujiamulia mambo. Mwanamke anatambuliwa kuwa na akili tambuzi wa kujiamulia mambo na mwenye uwezo wa kutetea haki yake kwa ukomavu na ukakamavu kama mwanamume. Zuhura, mkewe Mango ni mfano bora anapotetea imani yake ya Uislamu kama anavyosema Zuhura:

> “Katika suala la dini uniache nifanye uamuzi wangu mwenyewe. Maana hata nikienda kanisani kitakachoabudu ni moyo wangu si wa mume wangu.” ....Zuhra hakukatalia mbali ushawishi wa mumewe tu hata Tonje alipomjia alimweleza....(Uk. 23)

Ndoa ni asasi inayoleta uhusiano mpya kati ya familia husika. Familia hizi huhusishwa katika harakati za matayarisho ya sherehe zinazohusiana na ndoa ili kuimarisha uhusiano wao. Mwandishi anazitaja baadhi ya ndoa zisizohusisha familia zao katika harakati hizo kwa kuelewa kwamba, ndoa ni mkataba wa watu wawili ila si jamii nzima. Ndoa hizi zinatambuliwa kushuhudia changamoto chache mno kutokana na upendo, heshima na uelewano wa wanandoa husika. Ndoa ya Mango na Sakina inatambuliwa kutofuata taratibu za kidini wala za kitamaduni ila wanaishi kwa furaha kama mume na mke kama anavyosema mwandishi:

> Mango bado alimweka Sakina. Sasa alitangaza kuwa Sakina alikuwa mkewe. Sakina hakuona lolote litakalo mfanya amwache Mango. Sakina ndiye mwanamke aliyempenda naye akampenda. Sakina alijua jinsi ya kumwangalia. Alimwangalia vizuri kwa maneno na kumkongowea arudipo nyumbani. (uk. 38)

Mwanamume anadhaniwa kuwa na uwezo wa kukimu na kukidhi mahitaji ya familia yake. Wanaume wanatambuliwa kutelekeza majukumu yao kama wazazi na kuwatwika watoto wao majukumu ya kikumu familia zao. Mango anatambuliwa kutelekeza majukumu yake jambo ambalo linamlazimu mwanawe Michael, kubeba mzigo wa kukidhi mahitaji ya famila yake yote kama anavyosema mwandishi:

> Michael alipoanza kumsaidia Njite akawa akifanya kazi kidogo. Alipokuwa anampa pesa kidogo naye akwa anamtumia mamake kidogo. Mama alifurahi sana. Apondi aliona kuwa hata kama mume hakumthamini amefanikiwa kumpata mwana ambaye ndiye nyota ya kumiliki mji wa Mango. (uk. 28)

Utamaduni wa Kiafrika unampendelea mwanamume kwa kumpa uhuru wa kupenda na kupendwa na kumnyima mwanamke uhuru huo. Wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika wanaopigania uhuru wa mwanamke wa kupenda bila kuzuiliwa na tamaduni chakavu za Kiafrika. Wanasisitiza kuwa mwanamke anastahili kuwa huru wa kujichagulia mchumba, kukaa au kutoka katika ndoa inayomdhulumu kama anavyokubaliwa mwanamume. Lona anatambuliwa kudhihirisha uhuru wake wa kupenda kwa kutoka katika ndoa yake ya kwanza na kuingia katika ndoa ya pili na kasisi Joshua kama anavyosema Mganga:

> “ Lona ana hiari ya kupenda yeyote. ..Sina chuki naye. Nitamwacha. Sitachukua chochote. Hata mtoto nitamwachia...” Waliondoka....Lona alibaki ndani ya nyumba na Joshua (uk. 35)

Katika baadhi za jamii za Kiafrika ni mwiko mwanamume kufanya kazi za nyumbani kama upishi na ulezi. Mwanamume anayefanya hivi hudhaniwa kulogwa na mkewe na hukosa heshima miongoni mwa wanaume wenzake na jamii nzima. Ufeministi wa Kiafrika unapigania usawa wa jinsia kwa kusisitiza wanandoa wasaidiane kazi kwa mapenzi, heshima na uelewano wala si kwa ushirikina na lazima. Mwanamke anatambuliwa kutumia ushirikina ili kumthibiti mwanamue kwa mapenzi ya uwongo. Adema anatambuliwa kutumia ushirikina ili kupumbaza mumewe kwa mapenzi ya uwongo kama anavyosema Adema:

> “ Hivi karibuni ataanza kufuata upepo kama bendera. Wangu alijifanya mjoji nilimkomeza. Nikirudi nyumbani yuko hukoo. Jikoni anakoosha vyombo hadi nikimweleza aache. Akiniona nikiingia ni baridi, anasema tu “*Mummy! Mummy! Mummy! Mummy!*” Leo yuko chini ya nyaya zangu.” (uk. 107)

Kwa kuwa wanandoa hupewa hadhi katika jamii, ni matumaini ya kila mwanajamii kuolewa au kuoa. Mtu aliyeoa au kuolewa ndiye anayetambuliwa kukamilika na jamii husika. Kigezo hiki kinawanyima binadamu uhuru wa kujiamulia kuoa au kutooa. Wanajamii wanatenda kinyume na matarajioa ya jamii kwa kuishi bila kuoa wala kuolewa kwa hiari. Awinja, mamake Lydia anatambuliwa kama mwanamke anayeamua kuishi bila kuolewa kwa hiari japo ana watoto kama anavyosema mwandishi:

> Mamake Lydia, Awinja hakupata kuolewa ila alikuwa na rafiki yake Mgyriama, Kazungu. Huyu Kazungu ndiye aliyemzaa Lydia na baadaye akamza Leah. (uk. 83)

Patricia pia ni mwanamke mwengine anayetambuliwa kuishi bila mume kwa hiari na kuwalea peke yake bila baba kama anavyosema Patricia:

> "…… Hata nikizaa mtoto nitamwangalia mimi mwenyewe kama ninavyowaangalia wale wengine." (uk. 183)

Isitoshe, wanaume nao wanatambuliwa kuishi bila wake kwa mfano, Mganga kama anavyosema mwandishi:

> Japo mama yake alimhimiza aoe hakuona haja....Hakutaka shughuli yoyote na mwanamke. (uk. 72)

Ndoa ni asasi ya kudumu na talaka si jawabu ila tu kama mke au mume ni msherati basi panakuwa na sababu thabiti ya talaka. Mwandishi anasawiri mwanamume kama nguzo ya ndoa kutokana na sifa ya usamehevu. Mwanamume anatambuliwa kuwa sifa ya usamehevu na upendo anazotumia kudumisha ndoa yake na talaka si jawabu kamwe. Kyalo, mumewe Salome anatambuliwa kama nguzo ya ndoa yake kwa kumsamehe mke wake baada ya kumfumania na mume mwengine kama inavyojitokeza katika mazungumzo haya:

> "Utanisamehe Kyalo?" Salome aliuliza.
> "Sitakusamehe." Kyalo alisema
> "Kwa nini *Daddy*?"
> "Kwa sababu nilikusamehe usiku ule"(uk. 59)

Katika jamii za Kiafrika, mambo ya mapenzi na ndoa huthibitiwa na mwanamume. Mwanamume hutarajiwa kuanzisha mawasiliano kwa kutoa pendekezo lake la kimapenzi ambayo huweza kufikia ndoa. Ni nadra sana mwanamke kupendekeza mabo yanoyo husu mapenzi na ndoa na anapofanya hivyo, hudhaniwa kuwa msherati. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza kuwa

mwanamke awe huru wa kupendekeza nia ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamume bora awe anampenda. Lydia anatambuliwa kutenda kinyume na matarajiao ya jamii kwa kujipendekeza ili aolewa na Michael baada ya kugundua kuwa yeye ndiye anayefaa kuliko wanaume ambao amewahi shirikiana nao kimapenzi kama anavyosema mwandishi:

> Katika Michael Lydia aliona mume wa baadaye. Lakini vipi? Yeye Michael hakusoma hadi chuo kikuu kama Lydia…. Alikuwa na tatizo jingine nalo ni kuwa Michael alikuwa anamdokezea hataki kuoa….Atamsimbika vipi hadi akubali?...Ingawa Lydia alikuwa na rafiki Luseno alikuwa mlevi wa kupindukia. Luseno pia alikuwa mwalimu lakini hakufaa mume….Michael alionekana mume mwenye matumaini mkubwa hata kama elimu yake ilikuwa duni. (uk. 110)

### b) Dini

Dini inasisitiza binadamu kuwa na imani kwa Mungu. Binadamu anatambuliwa kutenda kinyume na matarajio ya jamii kwa kutafuta usaidizi kutoka kwa waganga wa kienyeji kwa kukosa imani kwa Mungu. Familia ya Michael inatambuliwa kutafuta usaidizi wa Kabwere, mganga wa kienyeji, Michael anapougua kama anavyosema mwandishi:

> ...Walisubiri ushauri wa Kabwere. Hapo ndipo walipotegemea kupata kufungua fundo lililomfunga Michael kumnyima kula, kusoma na raha wazionazo wana wa rika lake...(uk 17)

Unafiki umeenea miongoni mwa waumini ukiongozwa na viongozi wa dini. Lona, kasisi katika kanisa la New Jerusalem anatambuliwa kushiriki ushirikina ili kutatua shida zinazomkumba kinyume na matarajio ya kijamii. Lona anatambuliwa kama mnafiki kwa kutumia jina la Mungu ila anategemea uwezo wa uganga kama inavyoelezea mwandishi:

> Lona alijiona mshindi katika vita hivi.... aliamini Mungu hawezi kukusaidia hali umekaa tu. Lazima upange mikakati. Mikakati kama hiyo yapatikana kwa Angelina… (uk. 113)

Dini ni asasi inayotarajiwa kujenga umoja, upendo na amani miongoni mwa wanajamii kupitia viongozi wake. Uhusiano wa waumini unatambuliwa kuzorota kutokana na wivu na tamaa inayokithiri miongoni mwao kama anavyoelezea mwandishi:

> Zuhra hakuamini uchimvi wa makanisa pale Mombasa. Mwezi uliopita watu kumi walitiliwa sumu katika mchuzi wa nyama. Hao watu wote walikufa bila kusalimika mtu mmoja. Mwaka moja mbele mama Julia amefanyiwa dawa akashikwa na wazimu….Leo Mango amefanyiwa dawa. Kisa na maana ni uongozi na hiyo sadaka. (uk. 61)

Viongozi wa dini wanatarajiwa kuwa vielelezo na kutoa mwelekeo mwafaka katika jamii. Hata hivyo, wanatambuliwa kuchangia kuzorota kwa maadili kinyume na matarajio ya jamii kutokana na matendo yao ya usherati, ushirikina, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya kama inavyojitokeza katika nukuu hizi:

> ......walipiga soga kuhusu vitimbi vya Michael kunaswa katika utandu wa mapenzi. Hawakuamini....Ni nini kilichomharibikia akatia guu katika bwawa kama hili? Bwawa la tope, bwawa la maangamizi na bwawa la kishetani. (uk. 153)
> Wivu, husuda na tweatwea zilijengeka katika makanisa…polisi wakafika pale *New Jerusalem*. …walipata mihadarati ya aina ya *hashish, heroine*, bangi na mihadarati mingine. (uk.198)

Dini imeonekana kumpendelea mwanamume kwa kuwapa nafasi za uongozi na kumnyima mwanamke nafasi sawa na mwanamume. Mwanamke anatambuliwa kuongoza vitengo mbalimbali katika baadhi ya madhehebu kwa kudhihirisha uwezo uongozi kwa mfano, kanisa la Kianglikana, *Assemblies of God* na mengineo mbali na kushikilia nyadhifa za ukasisi. Kasisi Lona anatambuliwa kama mwanamke kasisi katika kanisa la New Jerusalem kama anavyosema mwandishi:

> Lona sasa ndiye aliyepachukua mahali pa Michael. … Joshua aliona kakamilika. (uk. 79)

### c) Utamaduni

Utamaduni wa jamii una jukumu la kuipa jamii husika mwelekeo unaokuza maadili mema miongoni mwa wanajamii. Teknolojia mpya, elimu na biashara inachangia kuzorota kwa tabia za watu kwa kuiga mienendo na tabia za kigeni. Utamaduni wa Kiafrika unasisitiza mambo ya mapenzi na ndoa kushughulikiwa kwa siri na taadhima kuu. Mwandishi anawabeza baadhi ya watu wazima wanaofanya mambo kinyume na matarajio ya jamii kwa kushiriki katika mambo ya mapenzi waziwazi na hata kugunduliwa na watoto. Mango anatambuliwa kama mzazi asiye na heshima kwa watoto wake kwa kushiriki katika mambo yanayohusu mapenzi hadharani tena bila heshima kama anavyosema mwandishi:

> ...alikuwa amewekwa na hawara aiitwaye Sakina. (uk. 1)
> … Michael ndiye aliyekuwa akitumwa na babake kumletea salamu.
> ..alikwisha mwambia kuwa yeye Sakina ni mamake. Michael alimheshimu..Kila wakati akienda kumwona alimwita mama. (uk. 13)

Utamaduni wa kiafrika unasisitiza ubikira wa mtoto wa kike na kupuuza ubikira wa mtoto wa kiume kabla ya ndoa. Mtoto wa kiume anatambuliwa kudumisha ubikira wake akilinganishwa na toto wa kike kinyume na matarajio ya jamii. Hivi sasa ni vigumu kupata msichana bikira kwa kuwa vijana hujiingiza katika mapenzi na kushiriki ngono kabla ya kuolewa. Lydia anatambuliwa kushiriki ngono kabla ya kuolewa akilinganishwa na Michael ambaye anatambuliwa kutunza ubikira wake hadi anapooa wake kinyume na matarajioa ya kijamii kama anavyosema mwandishi:

> Usiku baada ya harusi ulikuwa wa pekee kwa Michael. Katika mambo ya mapenzi Michael alikuwa limbukeni. Tangu alipokuwa chipukizi hapo Kisauni hakupata kufanya mapenzi yakampelekea katika kujamiana……Lakini walivyosema wahenga kinolewacho hupata. Lydia alimnoa…Lydia, japo hakuwa kiruka njia alikuwa kaonja hii aali mara kadhaa. Hakuona lolote geni. (uk. 118)

Malezi ni kipengele cha utamaduni kinaojumwisha utunzaji na uelekezaji wa mtoto. Hapo awali malezi ya mtoto ulikuwa jukumu la jamii nzima ambao ulifanikishwa kutokana na ushirikiano na uhusiano mwema kati ya wanajamii. Jamii inatambuliwa kutelekeza jukumu la jamii la malezi kutokana na uhusiano mbaya kati ya wanajamii jambo ambalo linachangia kuzorota kwa maadili kama yanavyojitokeza katika mazungumzo kati ya Bwana Njenga na Nice:

> Bwana Njenga alikutana naye mjini *New York* alipokuwa katika shughuli zake za ukasisi. "Habari," alimwanza Njenga
> "Hi" Nice alijubu....
> "Naweza kusema jambo nawe?"
> "Speak to me? About what?" Nice alisema….
> "Kitu kidogo."
> "Ok." Nice alimpa idhini....Nice alimtazama Jenga....
> "Well nilitaka kukuuliza unakaa wapi? Unaa… Yaani nilitaka umkubali Yesu." "Sikiza. Baba yangu ni mhubiri. Hakufaulu kuniokoa. Wewe hutafaulu. Ninakoishi na nikifanyacho yakuhusu vipi?" (uk 128)

### d) Elimu

Jamii za Kiafrika zinatilia maanani elimu ya mtoto wa kiume na kupuuza elimu ya mtoto wa kike. Mwandishi anatambua baadhi ya familia zinazoshinwa hata kufunza mwana wao wa kiume tena wa kwanzo kwa kukosa kutambua umuhimu wa elimu. Kinyume na matarajio ya jamii, Mango anatambuliwa kama mzazi asiyezingatia masomo ya watoto wake na kusingizia hali yake umaskini kama kizuizi kama anavyosema mwandishi:

> Michael alikuwa amerudi shuleni. Baada ya kufaulu mtihani wake wa darasa la nane hakujiunga na shule ya upili… Japo alipita vizuri baba yake alikosa karo ya kumlipia hata Shimo la Tewa ambayo ndiyo shule yake ya ndoto (uk. 21)

Jamii za Kiafrika zinapendelea mtoto mvulana kwa kumpa nafasi ya kusoma. Mtoto wa kike anadhaniwa kutokuwa na uwezo wa kufanya vyema katika elimu hasa masomo kama Fizikia na Hisabati yanayodhaniwa kuwa ya kiume. Watoto wa kike wanatambuliwa kuwa na uwezo sawa na watoto wa kiume katika masomo kwani, wamebobea katika sekta ya elimu na kufanya vizuri hata zaidi katika masomo yanayodhaniwa kuwa ya kiume. Kwa mfano, Lydia na Patricia ni wasichana ambao wamebobea katika sekta ya elimu na kufanya vizuri zaidi katika masomo yanayodhaniwa kuwa ya wavulana kama inavyojitokeza katika nukuu hizi:

> Lydia alikuwa amekamilisha masomo yake katika Chuo Kikuu cha Kenyatta..... Baada ya Kisauni Primary alijiunga na Coast Girls pale Mombasa na baadaye akaingia chuoni. (uk. 83)
> "Yaani ninashangaa msichana aweza kufundisha masomo magumu kama hayo......Nilikuwa ninafikiria masomo kama hayo ni ya wanaume tu. Kumbe siku hizi mambo yamebadilika sana." Michael alisema. (uk.100)

### e) Uchumi

Jinsia ya kike imekuwa ikipambana na hali ngumi kiuchumi kwa kukosa nyenzo za kuzalisha mali. Utamaduni wa Kiafrika umetengea wanawake majukumu magumu, ya kibaguzi na yasiyozalisha mali yakilinganishwa na ya wanaume. Hali hii imeifanya jinsia ya kike kuwa mtegemezi wa jinsia ya kiume kwani mhitaji hana chaguo. Mwandishi amefaulu kusawiri jamii iliyo na usawa wa kijinsia kama inavyopiganiwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika kwa kuwachora wanawake kama watega uchumi. Wanawake wanatambuliwa kupiga vita dhana ya kuwa wao ni viumbe tegemezi na kujihusisha na shughuli za kuzalisha mali inayowawezesha kukimu mahitaji ya famila zao. Apondi anajitambulisha kama mwanamke anayetegemea juhudi zake kukimu na kukidhi mahitaji ya familia yake peke yake kama anavyosema mwandishi:

> ....Apondi ni mama aliyelima kama tingatinga katika mashamba ya watu kujikimu yeye na wanawe. (uk.90)

Kwa muda mrefu mwanamume amesawiriwa kukosa imani na mwanamke kuhusu mambo ya pesa. Mwandishi amekiuka dhana hii kwa kuonyesha kuwa mwanamume anaimani kwamba mwanamke anaweza kuzalisha na kutunza mali mbali na kusaidia nayo familia yake kinyume na ilivyodhaniwa. Mwandishi anamsawiri Sakina kama baadhi ya wanawake walio na sifa hizi na

kwa sababu hii, Mango anatambuliwa kumpa nusu ya malipo yake ya uzeeni ili aanzisha nayo biashara ya famila yao kama anavyosema mwandishi:

> Sakina ndiye mwanamke aliyempenda. Sakina alijua jinsi ya kumwangalia…….Alipokuwa katika kitivo cha dhiki alikuwa mwepesi. Wakati mwingine hata kama hatasaidia alionyesha huruma za dhati. Nusu ya malipo ya Mango ya bandarini yalipewa Sakina. Sakina alianzisha kiduka cha kuuza kanda za video. Ni mwanamke aliyejua kuteka uchumi. Mango hakuwa na wasiwasi. (uk. 38)

Barbara (1993) anasema kuwa wanawake wanaajiriwa katika vitengo vya chini sana kutokana na ukosefu wa elimu. Kuna wanawake wanaoshikilia nyadhifa za juu uongozini wakilinganishwa na wanaume. Wanawake wanatambuliwa kutokuwa na idadi kubwa katika sekta ya elimu na ajira kwa kuwa nyadhifa za uongozi zimetengewa wanaume jambo ambalo linapingwa na wafuasi wa Ufeministi wa Kiafrika. Kutokana na mchango wa wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, wanawake sasa wanatambuliwa kushikilia nyadhifa mbalimbali uongozini kutokana kufauli kwao katika sekta ya elimu. Patricia anatambulishwa kama mwanamke anayeshikilia wadhiwa wa juu uongozi baada ya kuhidimu vizuri katika masomo kama anavyosema mwandishi:

> Patricia hajui amshukuru vipi Maulana kwa maisha yake ya sasa. Sasa yeye ni mwalimu mwandamizi wa shule ya *South B Academy*...kama mwalimu mkuu hayuko anaendesha shule (uk. 224)

Mwanamke mwengine ambaye anatambuliwa kuajiriwa kutokana na kielimu aliyonayo kinyume na matarajio ya jamii ni Lydia ambaye ni mwalimu wa shule ya upili kama anavyoelezea mwandishi:

> Lydia alikuwa mwalimu wa *Alliance Girls*. Baada ya Kisauni *Primary* alijiunga na *Coast Girls* pale Mombasa na baadaye akaingia chuoni. (uk. 83)

### f) Siasa na Uongozi

Masuala ya usawa wa jinsia katika siasa na uongozi yalianza katika miaka ya 1789 – 1795 kama anavyosema Mirikau (2011) katika utafiti wake anaposema kwamba, jitihada hizi za kutafuta usawa ulianza nchini Ufaransa wakatai wa mageuzi ya *Msimbo wa Napoleon.* Wanawake waliandamana kupinga kauli kuwa wana akili dhaifu hivyo basi hawawezi kuwa viongozi bora. Jitihada hizi zao zimechangia bara la Afrika kupiga hatua kwa kuwapa wanawake nafasi sawa katika uongozi na siasa kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Lona anatambuliwa kushikilia

nyadhifa za uongozi wa nchi na kujitosa katika siasa uwanja uliodhaniwa kuwa ya wanaume kama anavyosema mwandishi:

> Hakuna tena kilichomtisha Lona. Tayari amemdhibiti mumewe. Alidhibiti uchumi. Aliwadhibiti waumini. Sasa alidhibiti siasa za nchi. Maana hata rais wa nchi alimfahamu. Si muhali kumwona kumwona akitumika siku za holidei akiomba au kama amekaa na wakubwa wa serikali….(uk. 131)

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua mabadiliko yanayotokana na utambulisho wa jinsia katika kupigania ukombozi na usawa wa jinsia katika jamii wanamoishi. Swala la ukombozi na usawa unastahili kuhusisha jinsia zote ili ifanikiwa, jinsia ya kike ikiwa katika mstari wa mbele kwa kuwa ndiyo imenyanyaswa na kudhulimiwa kwa muda mrefu.

Mambo ambayo tumeangazia ni pamoja na ukombozi na usawa katika sekta ya siasa na uongozi. Mabadiliko yanashuhudiwa ambapo wanawake wanatambuliwa kujitosa katika siasa kutokana na ushawishi wao katika serikali. Wanaume wanasawiriwa kuwahusisha wanawake katika maongezi ya kisiasa ili kuwafahamisha kuhusu mfumo wa uongozi wa nchi husika. Jinsia inatambuliwa kuwa na uwezo sawa kiuchumi kwani wanawake wamedhihirisha uwezo wao kwa kupigania nyenzo za kuzalisha mali zilizodhibitiwa na wanaume.

Jamii imetambua haja ya kuwa na usawa wa jinsia katika kutoa maamuzi na ushauri ili kuwa na jamii iliyojengeka kimaendeleo. Wanawake sasa wanatambuliwa kuwa na uhuru wa usemi na kutoa mchango wao kuhusu maendeleo na matatizo yanayowakumba. Wanaume wanatambuliwa kupinga tamaduni chukizi zinazowakandamiza wanawake kama ulipwaji wa mahari na kuozwa kwa mtoto msichana kwa lazima.Tumeweza kudhihirisha mabadiliko katika majukumu ya wanajamii kwani si ya kipaguzi bali yanategemea tajiriba na uwezo wa mtu binafsi. Mabadiliko haya yanatokana na juhudi za wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika wanaopigania usawa na ukombozi wa jinsia katika jamii za Kiafrika.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumetoa mahitimisho ya utafiti wetu kwa kutoa muhtasari wa yale yote ambayo tumeshughulikia kwa kurejelea madhumuni na maswali ya utafiti huu. Tumeangazia ufaafu wa nadharia katika utafiti wetu kisha tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

### 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Katika sura ya kwanza tumechunguza masuala yanayohusiana na utafiti wetu. Tumeshughulikia tatizo la utafiti ambapo tumegundua pengo ambalo limetokana na tafiti za awali zilizoshughulikia masuala ya jinsia ya kike na kupuuza masuala ya jinsia ya kiume. Ni kutoka an pengo hili ndipo tumeamua kushughulikia masuala ya jinsia ya kike pamoja na jinsia ya kiume kwa kujikita katika kazi za mwandishi John Habwe za *Mumbile si Huja* na *Paradiso.*

Katika kazi hii tulinuia kushughulikia madhumuni matatu. Kwanza, tulinuia kubainisha jinsi asasi za jamii kupitia tamaduni zake zinavyoathiri mazingira ya utambulisho wa jinsia ambayo tumeshughulikia katika sura ya pili. Tumetoa fafanuzi mbalimbali za ndoa kama vile, ndoa ya kitamaduni, ndoa ya kidini na ndoa ya kikatiba. Tumefafanua dini za Kikristo na Kiislamu ambazo ndizo zimeenea na kutambulika zaidi katika jamii za Kiafrika. Tumewapa utambulisho jinsia kulingana na sifa na tajiriba zao wala si kulingana na matakwa ya jamii. Pili, tulinuia kuangazia namna jinsia za kike na kiume zinavyoathirika kutokana na changamoto zinazopitia kufuatia harakati za kutaka kujitambua na kutambuliwa na jamii na haya tumeyashughulikia katika sura ya tatu. Baadhi ya changamoto zinazowaathiri wanajamii ni pamoja na dhuluma na ukatili, kutowajibika, kiburi na ubinafsi, umaskini, watoto na malezi na kushikilia mila na desturi chakavu za kale. Tatu, tulidhamiria kudhihirisha mabadiliko ya mielekeo ya jamii kupitia fasihi kama nyenzo muhimu inayochangia mabadiliko hayo na haya tumeyaangazia katika sura ya nne. Kinyume na ilivyodhaniwa kuwa wanaume ni jasiri na wenye uwezo wa kujitetea, jinsia hii imetambuliwa kuathirika zaidi kwa kushikilia mila chakavu za kale zinazowapendelea. Kutokana na utafiti wetu tumeangazia utambulisho wa jinsia ya kike na kiume kuwili; utambulisho hasi na

utambulisho chanya. Kwa kuwa tafiti nyingi za hapo awali zilishughulikia masuala ya jinsia ya kike na kupuuza masuala ya jinsia ya kiume, tumebaini kuwa, ili harakati za kupata ukombozi wa jinsia ya kike zifanikiwe, ni muhimu kuhusisha jinsia ya kiume kama washikadau katika harakati hizi. Kutokana na wazo hili ndipo tuliamua kushughulikia jinsia za kike na kiume kwa pamoja tukirejelea kazi za John Habwa za *Maumbile si Huja* na *Paradiso*.

Tumetoa fafanuzi juu ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo ingetuongoza katika utafiti wetu. Tulitumia nadharia hii kwa sababu kazi ambazo tumeshughulikia zimeandikwa katika mazingira ya Kiafrika ambayo zinauhalisia mwingi na baadhi ya jamii za Kiafrika. Imetuwezesha kudhihirisha jinsi asasi za jamii za Kiafrika zinavyoathiri utambulisho wa jinsia na kuangazia namna jinsia zinavyoathirika kutokana na changamoto zinazopitia katika harakati za kutaka utambuisho. Nadharia hii imekuwa na manufaa katika utafiti wetu kwa kuwa inasisitiza usawa wa kijinsia na kupinga utamaduni unaodhulumu wanajamii. Aidha, tumeitumia kwa kuwa ndiyo inayopendekeza njia za kukabiliana na changamoto zinazotokana na utamaduni chakavu za kale.

## 5.3 Matokeo ya Utafti

Tumegundua kuwa jinsia zote zinaathirika kutokana msimamo wa kidini unaokinzana na wa kitamaduni kwa mfano, dini inapendekeza ndoa ya mke mmoja ilhali utamaduni wa Kiafrika unapendekeza ndoa ya wake zaidi ya mmoja. Jamii za Kiafrika zinampa hadhi mwanamume aliyeoa wake wengi kwa kumpendelea uongozini. Changamoto inatokana na nia yao ya kutaka kushikilia utamaduni wa kimapokeo wa kuoa wake wengi na mwelekeo wa kidini unaopigania ndoa ya mke mmoja. Jinsia ya kiume imesalia katika hali ya upweke kwa kupuuzwa na baadhi ya makundi yanayopigania ukombozi wa jinsia ya kike kwa kudhaniwa kuwa na uwezo wa kujitetea. Kwa sababu hii, uhusiano wao umeathirika vibaya kutokana na mikwaruzano kati yao inayochangiwa na mabadiliko ya mielekeo ya jinsia ya kike kwa msingi wa Ufeministi wa Kiafrika ilhali wanaume wamesalia kufuata mwelekeo wa kimapokeo.

Jamii imetelekeza majukumu yake hasa ya malezi jambo ambalo limechangia kuzorota kwa maadili. Wazazi wanatambuliwa kuchangia kuzorota kwa maadili kwa kuwa mfano mbaya kwa watoto wao. Watoto wamepotokwa zaidi kwa kufuata tamaduni za kigeni kutokana na kuipuka

kwa teknolojia. Hili limechangiwa na hali ya kukosa mwelekeo thabiti kwani, utamaduni ulionuiwa kuwapa huo mwelekeo umepingwa vikali kwa kudhaniwa kuwa ndio chanzo cha dhuluma kwa jinsia. Dhana ya wanajamii kupigania uhuru, haki na usawa unasawiriwa visivyo kwa kuwa vita hivi vimetumiwa kukiuka kanuni za maisha za kijamii. Ili kuwe na jamii iliyo na mwelekeo ni vyema kuwe na sheria zinazoiongoza jamii husika.

Jinsia zote zinatambuliwa kuathiriwa na hali ya umaskini kinyume na ilivyodhaniwa kuwa wanaume wanamiliki nyenzo za kuzalisha mali. Ili kujikwamua kutokana na hali ya umaskini, baadhi ya watu wametambuliwa kushiriki maovu kama vile, kutoa jamaa zao kafara, kushiriki usherati, ushirikina na hata kuingia katika ndoa isiyotambuliwa. Wanawake wamedhihirisha uwezo sawa na wanaume wa kutega uchumi ili kukimu familia zao kinyume na walivyofikiriwa kuwa wategemezi wa wanaume. Jinsia inatambuliwa kutobagua kazi kwa msingi wa maumbile. Wanaume wanatambuliwa kufanya kazi za kinyumbani zinazodhaniwa kuwa za wanawake na wanawake vilevile, wanatambuliwa kufanaya kazi ngumu na chafu zinazodhaniwa kuwa za wanaume.

Tumegundua kuwa jamii imetambua umuhimu wa elimu kutokana na faida zake kwa hivyo, imewapa watoto wote nafasi sawa ya kusoma. Mtoto wa kike amedhihirisha uwezo sawa na mtoto wa kiume katika masomo kwa kusoma hadi chuo kikuu mbali na kufanya vizuri zaidi katika masomo yanayodhaniwa kuwa ya wavulana kama vile, Fizikia na Hisabati. Ili mwanamke aweze kujitegemea, ni lazima awe na elimu na uwezo kiuchumi. Maendeleo ya jamii inahitaji wanajamii wenye elimu na uwezo mkubwa kiuchumi. Kutokana na kupanda kwa hali ya maisha, wanawake wanastahili kushirikishwa katika sekta ya uzalishaji mali ili waweze kukidhi mahitaji ya familia zao kama inavyostahili.

## 5.4 Mapendekezo

Ni matumaini yetu kuwa utafiti huu utawapa mwongozo mwema wasomaji. Tunatambua na kukiri kwamba, utafiti huu unahusu sehemu ndogo tu japo muhimu. Katika utafiti huu tumeshughulikia utambulisho wa jinsia ya kike na kiume. Tumechunguza jinsi asasi za jamii zinavyoathiri utambulisho huu, changamoto zinazotokana na harakati za jinsia kutaka utamabulisho na mabadiliko katika mielekeo ya jamii.

Tunatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye;

(i) Utambulisho dhalimu wa jinsia ya kiume.

(ii) Mchango wa asasi ya utamaduni katika kuimarisha maadili katika jamii.

## MAREJELEO


Arege, T. (2006) *Mwongozo wa Pango*: Nairobi: Vide Muwa Publishers

Bal, M. (1997) *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (2nd edition). Toronto: University of Toronto Press

Barbara, E. (1993) *Let's Discuss Women's Rights*, Englana: Wayland Publishers

Benokraitis, N. V. (1989) *Marriage and Families: Changes, Choices and Constraints.* Englewood Cliffs, New Jersey: Prentice Hall.

Boss, P. (1993) *Family Stress Management.* Newbury Park, California: Sage Publications.

Chacha, W. C (2013) 'Taswira ya Mwanamke katika tamthilia ya *Nguzo Mama na Mama Ee'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Chapman, G. (2008) *Desperate Marriages. Moving towardsHope and Healing in Your Relationship.* Chicago: Northfield Publishing.

De Genova, M. K. (2008). *Intimate Relationships, Marriage and Families, Seventh Edition.* New York: McGraw Hill.

Eagleton, M. (1991) *Feminist Litrary Criticism.* New York: Longman Inc.

Holy Bible (1984) *New International Version:* International Bible Society – Africa

Habwe, J. (1995) *Maumbile Si Huja.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

________ (2005) *Paradis.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Hegedon, R. (1983) *Sociology.* Lowa: W. M. C. Brown Company Publishers.

Karinge, J. W. (2013) 'Usawiri wa Ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani*?' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Katola, E. (2006) 'Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili.' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kipyegon, P. E. (2013) 'Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika *Natala na KifoKisimani.'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kohen, W. J. (1993) *Women in Society.* New York. London and Routledge; Marshall Cavendish.

Lugano, R. (1989) 'Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi.' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Magare, F. A. (2002) 'Uhakiki wa Tamthilia ya *Amezidi* Kama kazi ya Kiubwege.' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Magoma, N. H. (1997) 'Mwamko wa Mwanamke katika Tamthilia Nne za Penninah Muhando.'

Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Maina, V. (2005) Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi za Shaaban Robert, Utenzi wa Haki na Adili,' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Maingi, H. G. (2011) Upembezwaji wa Mwanamke kama Udokezo wa Nafasi ya Mwanamke Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Maobe, O. J. (2011) 'Ukombozi wa Mwanamke katika Riwaya za Habwe,' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mbaabu, I. (1985) *Utamaduni wa Waswahili.* Nairobi: Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Mirikau, S. A. (2011) ' Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Wamitila, K. W.' Tasnifu Ya Uzamili, Chuo Kimuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Mlacha S. A. K. (1991) '*Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels,* Katika *Jarida ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Juz, 58,* Kur 54 – 61 Dar es Saalam: TUKI

Mosoti, Z. M. (1993) 'Maudhui katika Tamthilia Nne za Emmanuel Mbogo.' Tasnifu ya Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Msokile, M. (1993) *Msingi wa Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: EAEP Ltd

Muffin, R. F. (1991) *Novel, Novelist and Readers, Towards a Phenomenological Sociology Of Literature.* New York: State University of New York

Muhando, B. H. (2011) 'Nafasi ya Dini katika Ndoa.' Tathmini ya *Utengano* na *Paradiso*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Musyoka, F.M. (1996) 'Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao.' Tasnifu ya Uzamili Katika chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwita, B. M. (2005) 'Dhima ya Ichingero za Wakuria Kusawiri Taswira ya Mwanamke.' Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ndung'u, N. (1996) 'Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katana Mkangi: *Ukiwa, Mafuta na Walenesi.'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishawa)

Njogu na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Obure, E. M. (2012) 'Dhuluma Dhidi ya Vijana wa Kike katika Tamthilia za *Natala* na *Rosa*

*Mistika.'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kiku cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Onyoni, J. K. (2012) 'Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za *Natala* na *Mama Ee.'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairob. (Haijachapishwa)

Steady, F. C. (1981) *Reflecting the Politics of Sisterhood*. New York; African World Press.

Strobel, M. (1979) *Muslim Women in Mombasa; 1890 – 1975.* New Haven and London: Yale University Press.

Timammy, R. and Swaleh, A. (2013) 'Characterization and Construction of Gender Identity in Habwe's *Maumbile Si Huja* in International Journal of Education and Research Vol. 1No. 9.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi  Phoenix Pulishers

Wolf, V. (1929) *A Room of One's Own.* London: Penguin Books

Wollstonecraft, M. (1972) *A Vindication of the Right of Women.* Boston: Peter Edes

York, J. na Wenzake (1991) '*We are the Feminist that Women have Warned us About'*Katika *A Reader in Feminist Knowledge*.